# Nipashe

Alhamisi Juni 27, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579955

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Upinzani wapinga hedhi kuwa chanzo cha mapato

UKURASA 3




UKURASA 13

# Korosho zaibua mvutano bungeni

**MBUNGE** ataka zichomwe moto kisa?... Waziri Bashungwa acharuka, Naibu Spika aingilia kati... *Endelea ukurasa wa 2*



Innocent Bashungwa



Peter Msigwa

## Daktari feki akamatwa nyumbani akitibu watu

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**TWAWEZA YADAI KUKWAMA KWA KUKOSA KIBALI NBS**

TAASISI ya Utafiti ya Twaweza imesema imefanya utafiti mara tano ambao umekwama kutangaza kutokana na kukosa...

UKURASA WA 3

**KONGAMANO LA FURSA UWEKEZAJI DODOMA**

KONGAMANO kubwa la uwekezaji linaanza leo mkoani Dodoma, ambalo litatumika katika kutangaza fursa na vivutio vya uwekezaji vilivyopo...

UKURASA WA 4

**HESLB YATAJA TAREHE DIRISHA MIKOPO 2019/20**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSB) imesema kuwa Jumatatu ijayo itafungua dirisha la uombaji mikopo yake kwa njia ya mtandao kwa mwaka wa masomo...


## Jaguar matatani kauli za ubaguzi

UKURASA 25

**MICHEZO** MSENEGAL ALIYEIUA STARS AMNG'ATA 'SIKIO' MSUVA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Twaweza yakwama kwa kukosa kibali NBS

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Utafiti ya Twaweza imesema imefanya utafiti uliofanyika mara tano ambao umekwama kuitangaza kutokana na kukosa kibali cha Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Aidan Eyakuze, alisema taasisi yake inaendelea kufanya utafiti mbalimbali kama kawaida licha ya kukosa kibali cha kuzitangaza.

Alisema sheria ya sasa inawataka watafiti kuwasilisha utafiti huo NBS kabla ya kuutangaza, lakini licha ya kuupeleka muda mrefu bado hawajapata kibali cha kuutangaza.

"Wanasema wataalamu wao wanaupitia na kuufanyia uchambuzi kwa muda sasa bado tunasubiri kibali chao kwa sababu sheria inatubana si kama zamani tulipokuwa tukitangaza wenyewe baada ya kukamilika," alisema.

Kuhusu kushikiliwa kwa hati yake ya kusafiria, Eyakuze alisema ni miezi 11 sasa imepita, lakini kila anapofuatilia Idara ya Uhamiaji wanasema kwamba bado wanapeleleza kupata ukweli kuhusu uraia wake.

Alisema ameshindwa kusafiri kwenda nje ya nchi kikazi na mara kadhaa amekuwa akiwaandikia barua kutaka kujua hatima ya hati hiyo na jibu ni kwamba upelelezi haujakamilika mpaka sasa.

"Mimi ni raia wa Tanzania, nimezaliwa Mwanza wazazi wangu wote ni Wahaya na nilipata hati ya kwanza ya kusafiria nikiwa na miaka minane nakumbuka ni mwaka 1977 na tangu hapo sijawahi kuitumia vibaya hivyo nasubiri uchunguzi wao utawaambia nini," alisema Eyakuze.

Utafiti wa mwisho kutangazwa na Twaweza ulikuwa wa Julai 6, mwaka jana na wiki mbili baadaye hati ya kusafiria

INAENDELEA UK. 8

# Korosho zaibua mvutano bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KAULI ya Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Peter Msigwa, ya kutaka korosho zichomwe moto kwa madai kwamba zimeoza, jana ilimfanya Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashugwa, kucharuka kama mbogo, akimtaka Mbunge huyo kuthibitisha maneno yake.

Bashungwa na Msigwa walivutana kwa dakika kadhaa wakati mbunge huyo wa Chadema alipokuwa akichangia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019/20.

Wakati anachangia, Msigwa alisema serikali ya awamu ya tano imekuwa ikijinasibu kwamba inamjali mkulima mnyonge, wakati maisha yake yanazidi kuwa magumu.

"Serikali imekuwa ikisema inamjali mtu mnyonge, kimsingi mtu mnyonge kwa Tanzania ni mkulima na kwa bahati mbaya serikali hii imewaletea adha na kuwavuruga wakulima wa korosho. Sasa mmeanza kuwavuruga wakulima wa pamba," alisema Msigwa.

Baada ya kutamka maneno hayo, Waziri Bashungwa alisimama na kutamka 'Taarifa Naibu Spika' (Dk. Tulia Ackson) na baadaye kuruhusiwa kutoa taarifa yake akisema anayoyazungumza Msigwa si ya kweli kwa vile serikali haijawavuruga wakulima wa korosho na korosho ya Tanzania iko vizuri na ina ubora wa hali ya juu.

"Nimpe taarifa, serikali haijawavuruga wakulima wa korosho na korosho yetu bado ni bora. Tumeandaa kitabu na ubora wa korosho upo vizuri na tunataka kuiambia dunia kwamba korosho ya Tanzania ni bora.

"Wewe (Msigwa) ndiyo unawavuruga wakulima na si serikali, tutangulize uzalendo kwanza," alisihi Bashungwa.

Baada ya taarifa hiyo, Msigwa aliendelea kuchangia mjdala huo akidai kwamba taarifa ya Waziri Bashungwa haipokei na kwamba wamepeleka bei za kinyonyaji na uporaji kwa wakulima wa korosho.

"Taarifa yake siipokei, hizi ni bei za kinyonyaji nyie mmepeleka bei ya uporaji. Mshauri Rais hizi korosho bora mkazichome tu kwani zinaoza na zitaharibu soko la baadaye, hizi zichomeni moto," alitamka tena Msigwa.

Dakika chache tena baada ya maelezo hayo, Waziri Bashungwa akimtaka Msigwa kuthibitisha kauli yake kwamba kuna korosho zimeoza.

"Amesema korosho ya wakulima wetu imeoza na mimi nimetoka huko na nimetembea ghala kwa ghala, korosho yetu ni bora, naomba athibitishe kama imeoza kweli, kama haijaoza achukuliwe hatua kali, kwani mimi nimeiona ipo katika hali nzuri na yeye (Msigwa), athibitishe kwamba korosho imeoza," alisisitiza waziri huyo.

Kutokana na mvutano huo, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson alisimama na kutoa maelekezo yake akisema: "Kwa muktadha huo huo, nadhani Mheshimiwa Msigwa hoja yake ilikuwa kwenye korosho iko maghalani inunuliwe. Sasa Mheshimiwa Msigwa nyoosha mchango wako vizuri."

Akiendelea kuchangia, Msigwa alisema wabunge wapo kwa ajili ya kuwatetea wananchi na kudai kwamba kodi nyingi zinamfanya mkulima apunjwe.

"Ningeomba nieleweke sisi ni wabunge tupo kuwatetea wananchi tupo hapa kuwasemea wananchi. Hizi kodi zinamfanya mkulima apunjwe na hizi zinamfanya mtu wa mwisho anayekuwa anaumia ni mkulima. Kama kweli mnawajali wanyonge mngewakumbuka wakulima wa pamba, mngewakumbuka wakulima wa mahindi," alisema Msigwa.




Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akimpongeza mwandishi wa kitabu cha "Viwanda: Moving Tanzania Forward", Prof. Teddy Maliyamkono, baada ya kukizindua kitabu hicho mjini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Daktari feki anaswa akitibu watu nyumbani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Abdallah Bushiri (42) mkazi wa Igodima jijini Mbeya kwa tuhuma za kufanya kazi ya utabibu kwa kutibu magonjwa ya wanawake bila kuwa na taaluma ya udaktari.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Kituo Kikuu cha Polisi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema mtuhumiwa alikamatwa Juni 24, mwaka huu, nyumbani kwake.

Kamanda Matei alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa baada ya baadhi ya wananchi kutoa taarifa kwa jeshi hilo kuhusu shughuli anazofanya na akawekewa mtego uliowezesha kukamatwa na kupekuliwa.

Matei alisema baada ya kupekuliwa nyumbani kwake, daktari huyo feki alikutwa na vifaa tiba na dawa mbalimbali ambazo zinamilikiwa na serikali zikiwa na nembo ya Bohari ya Dawa (MSD) na nembo inayoonyesha kuwa ni mali ya serikali.

"Baada ya kumhoji, tulibaini kuwa hana taaluma yoyote ya udaktari lakini pia yuko na baadhi ya vifaa na dawa ambazo baadhi ni za serikali, zina nembo ya MSD na GoT (serikali ya Tanzania). Lakini pia baadhi ya wananchi walikuja kulalamika kuwa mtu huyo alishachukua fedha zao zaidi ya Sh. milioni mbili," alisema Kamanda Matei.

Alisema baadhi ya vitu alivyokutwa navyo mtuhumiwa huyo kuwa ni pamoja madaftari 119 yenye taarifa za wagonjwa aliowahi kuwatibu, vipimo 15 vya kupimia mkojo, dawa za kusafishia vidonda, kipimo cha malaria ambacho kinapatikana MSD na vifaa vingine.

Pia alisema mtuhumiwa alikutwa na dawa za ganzi chupa tatu, nyembe 26 za kufanyia upasuaji ambazo alikuwa anazitumia, picha za mionzi na themomita moja ambavyo vyote alikuwa anavitumia kwenye matibabu.

Alisisitiza kuwa baada ya taratibu kukamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Mganga Mkuu wa Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala, aliwataka wananchi kuacha kwenda kutibiwa kwa watu ambao hawana taaluma ya udaktari kwa madai kuwa hali hiyo inaweza kuhatarisha maisha yao. Aliwataka pia wananchi kutoa taarifa za watu wote wanaojifanya madaktari na kutoa huduma huku wakiwa hawana taaluma ya utabibu kama alivyofanya daktari feki aliyenaswa.

HABARI KITAIFA

# Upinzani wapinga hedhi kuwa chanzo cha mapato

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, imeelezea kushangazwa kwake na kupinga kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye taulo za kike kuwa chanzo cha mapato, huku ikisema haikubaliani na kitendo cha serikali kufuta msamaha wa kodi na kurejeshwa kwa VAT.

Msemaji Mkuu wa kambi hiyo kwa Wizara ya Fedha na Mipango, David Silinde, alisema ni jambo la ajabu kwamba bajeti ya serikali sasa inategemea matatizo ya wanawake kukusanya kodi hasa kuweka kodi kwenye taulo za kike.

Silinde alikuwa akiwasilisha maoni ya kambi hiyo kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019.

Silinde ambaye ni Mbunge wa Momba (Chadema), alisema muswada huo ukiangaliwa kwa umakini katika mapendekezo yanayohusu kodi ya ongezeko la thamani, Sura ya 148 hakuna sehemu inayosema au kutekeleza takwa hilo la serikali.

"Matokeo yake sasa, serikali imepitia katika sheria ya mapato kwa kuongeza kodi kwa wawekezaji wanaotengeneza taulo za kike. Watumiaji wa taulo za kike ni mama zetu, wake zetu, dada zetu na watoto wetu ambao wanazitumia kwa ajili ya kujihifadhi.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haiungi mkono kutumia hedhi kama chanzo cha mapato ya serikali. Kifungu hiki kinapendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kifutwe na serikali itimize wajibu wake wa kuhakikisha wanufaika wa taulo za kike wananufaika wenyewe, badala ya wafanyabiashara.

Wajibu huo ni wa serikali na kamwe haiwezekani kushindwa kutekelezwa kwa wajibu wa serikali ikiwa ni kwa gharama za hedhi ya wanawake wa Tanzania," alisema.

Pia alisema kambi hiyo inasisitiza kusisitiza kufutwa kwa kifungu kinachoruhusu utozaji wa kodi kwenye nywele bandia na rasta za bei mbaya, ikitaka serikali kutafuta vyanzo vingine vya mapato vinavyotokana na rasilimali zilizopo nchini.

Alisema pia ni jambo la ajabu kwamba bajeti ya serikali inategemea nywele bandia, kwa mantiki ya kawaida ikitokea wanawake wote wakaamua kunyoa nywele zao na wasivae tena nywele bandia mapato hayo hayatapatikana.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tunaliona jambo hili kama si sawa kwa sababu ni mapato yanayotarajiwa kupatikana kutoka kwa mama zetu kwa sababu tu wao ni wanawake na watumiaji wakubwa wa nywele bandia," alisema.

**MUSWADA HAUNA GENI**

Katika hatua nyingine, kambi hiyo imesema muswada huo wa sheria kwa kiasi kikubwa hauna jambo geni kutokana na serikali kushindwa kutambua vyanzo vipya vya mapato, badala yake imekuwa ikifanya kwa miaka yote.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, bado inaamini na inaishauri serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vya ujenzi, taulo za kike, nywele bandia na kwenye tiketi za ndege kwa safari za ndani ya nchi ili kuwawezesha wananchi kupanda ndege zilizonunuliwa kwa kodi zao," alisema Silinde.

Vile vile, aliongeza: "Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaendelea kuishauri serikali kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara nchini, kujenga mazingira rafiki kwa sekta binafsi na kutengeneza mazingira ambayo yatawawezesha wadau wa kodi na kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

"Hatuwezi kutarajia maziwa mengi kwa ng'ombe usiyemlisha majani ya kutosha."

## Kongamano la fursa uwekezaji Dodoma

**Na Beatrice Moses**

KONGAMANO kubwa la uwekezaji linaanza leo mkoani Dodoma, ambalo litatumika katika kutangaza fursa na vivutio vya uwekezaji vilivyopo kwenye wilaya zote saba za Mkoa wa Dodoma kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, katika taarifa kwa vyombo vya habari, alibainisha lengo la kongamano hilo ni uwapo wa fursa zitakazotangazwa ni uamuzi wa Rais John Magufuli kuhamishia Makao Makuu ya Nchi mkoani Dodoma Septemba, 2019.

"Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma tunaendelea kutoa shukrani za dhati kwa mheshimiwa Rais kwa uamuzi alioufanya na tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema ili aendelee kutuongoza kuelekea kujengea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025," alisema Mahenge.

Alisema Rais Magufuli ndiye anayetarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo lenye kauli mbiu "Dodoma, Fursa Mpya kwa Uchumi wa Tanzania, Wekeza Dodoma, Tukufanikishe" ambayo inatanabahisha nafasi ya Dodoma kwa sasa katika mustakabali wa uchumi na utawala wa nchi.

Dk Mahenge alibainisha kuwa licha ya kuwa na fursa lukuki zitokanazo na ujio wa Makao Makuu ya Serikali Mkoa wa Dodoma umebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi mahsusi.

"Mifugo na mandhari ya kuvutia kwa utalii, zipo pia fursa zingine kama vile za madini na wanyamapori. Mkoa wa Dodoma una sifa kadhaa zinazofanya uvutie kwa uwekezaji, sifa hizo ni pamoja na uwepo wa ardhi iliyotengwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uwekezaji," alisema.

Aliyataja maeneo ambayo wanakaribisha wawekezaji katika kilimo cha zabibu, alizeti, ufuta, pamba na karanga, mtama, mihogo na matunda na mboga.

Dk. Mahenge alisema pia kuna fursa kwa wawekezaji wa mifugo ya mbalimbali kama vile ng'ombe, mbuzi na kondoo, kuku na bata, samaki, nyuki na viwanda mbalimbali na ujenzi, husussan wa nyumba za makazi, kibiashara na ofisi.

Tpb Bank Grow with us

TPB BANK PLC

UZINDUZI WA TAWI JIPYA TPB KARAGWE



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki ya TPB Dkt. Edmund Mndolwa akimkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Kagera Brigedia Jenerali Marco Gaguti kwenye hafla ya uzinduzi wa tawi jipya la benki hiyo Wilayani Karagwe. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Karagwe Godfrey Mheluka, na kulia ni Mkurugenzi wa Teknohama na Uwezeshaji wa benki ya TPB Jema Msuya, na Meneja wa tawi la Karagwe Godfrey Banza



Mgeni rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Kagera Brigedia Jenerali Marco Gaguti akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili kwenye hafla ya uzinduzi wa tawi jipya la benki ya TPB Wilayani Karagwe. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki ya TPB Dkt. Edmund Mndolwa



Mkuu wa Mkoa wa Kagera Brigedia Jenerali Marco Gaguti akikata utepe kuashiria ufunguzi rasmi wa tawi jipya la benki ya TPB Wilayani Karagwe. Pamoja nae ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki ya TPB Dkt. Edmund Mndolwa, Mkurugenzi wa Teknohama na Uwezeshaji wa benki ya TPB Jema Msuya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Karagwe Godfrey Mheluka



Mkuu wa Mkoa wa Kagera Brigedia Jenerali Marco Gaguti akionyesha kadi yake mpya ya ATM mara baada ya kufungua akaunti kwenye tawi jipya la benki ya TPB Wilayani Karagwe. Nyuma yake ni Mkuu wa Wilaya ya Karagwe Godfrey Mheluka na Mkurugenzi wa Teknohama na Uwezeshaji wa benki ya TPB Jema Msuya. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki ya TPB Dkt. Edmund Mndolwa



Francis Kishenyi akipokea zawadi ya mteja bora kutoka kwa mgeni rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Kagera Brigedia Jenerali Marco Gaguti. Hii ilikuwa kwenye hafla ya uzinduzi wa tawi jipya la benki hiyo Wilayani Karagwe.



Mteja kutoka kikundi cha OKONYENZILE akipokea zawadi ya kikundi bora kutoka kwa mgeni rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Kagera Brigedia Jenerali Marco Gaguti wakati wa uzinduzi wa tawi jipya la Karagwe

215297302

## JPM amteua Kamishna mpya TIRA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Dk. Mussa Juma, kuwa Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema uteuzi huo umeanza Juni 25, 2019.

Kabla ya uteuzi huo, Dk. Juma alikuwa Mkuu wa Idara ya Bima katika Kitivo cha Bima na Hifadhi ya Jamii cha Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Dk. Juma anachukua nafasi ya Dk. Baghayo Saqware, ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

# HESLB yataja tarehe ya dirisha mikopo 2019/20

**Na Romana Mallya**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HELSB) imesema kuwa Jumatatu ijayo itafungua dirisha la kuombaji mikopo yake kwa njia ya mtandao kwa mwaka wa masomo 2019/2020.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa bodi hiyo, Abdul-Razaq Badru, dirisha hilo litafungwa rasmi Agosti 15.

"Maombi yote yatafanywa kupitia mtandao utakaopatikana kupitia www.heslb.go.tz dirisha litakapofunguliwa, wanafunzi wanashauriwa kuhakikisha wanakamilisha nyaraka muhimu zinazotajwa katika mwongozo wa utoaji mikopo na ruzuku kwa 2019/2020 unaopatikana katika tovuti ya HESLB www.heslb.go.tz," Badru alieleza katika taarifa hiyo.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa nyaraka na maelezo mengine ya ufafanuzi pia yanapatikana katika kitabu kidogo cha maswali na majibu 26 kuhusu uombaji mkopo kinachopatikana katika tovuti hiyo.

"Nyaraka muhimu ni pamoja na nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mwombaji wa mkopo iliyothibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) au Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA).

"Nakala nyingine ni cheti cha kifo cha mzazi wa mwombaji mkopo iliyothibitishwa na Rita au ZCSRA na barua ya Mganga Mkuu wa Mkoa (RMO), Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO) au Mganga wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji, Wilaya, Manispaa au Jiji inayothibitisha ulemavu wa mwombaji mkopo au mzazi wake na barua kutoka kwa taasisi iliyofadhili masomo ya sekondari au stashahada ya mwombaji mkopo," Badru alifafanua.

Katika taarifa hiyo, mkurugenzi huyo pia alisema bodi inafanya mawasiliano na Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili wanafunzi waliomaliza kidato cha sita na stashahada mwaka huu na wameshajiunga na jeshi hilo kwa ajili ya mafunzo, wapewe utaratibu bora kuwawezesha kuwasilisha maombi kwa njia ya mtandao.

"Mfumo wa uombaji mikopo kwa njia ya mtandao utakaofunguliwa Jumatatu ijayo, haumlazimishi mwombaji kuwa na matokeo ya kidato cha sita, mwombaji atapaswa kuwa na namba ya mtihani wake wa kidato cha nne tu," Badru alieleza zaidi katika taarifa yake hiyo.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alitoa wito kwa waombaji wa mikopo watarajiwa kusoma mwongozo uliotolewa na kuandaa nyaraka zote muhimu zinazohitajika kuthibitisha uhitaji wao kabla ya kuingia katika mfumo wa uombaji.

"Uzoefu unaonyesha kuwa mwombaji mkopo anaweza kutumia dakika 30 kukamilisha maombi yake katika mfumo ikiwa ana nyaraka zote muhimu," Badru alisema.



Wahamiaji haramu kutoka nchini Ethiopia waliokamatwa katika pori la kijiji cha Lugono wilayani Mvomero mkoani Morogoro, pamoja na waliokamatwa kwa tuhuma za kuwasafirisha wahamiaji hao wakiwa chini ya Askari wa Kikosi cha Uhamiaji mkoani humo. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Wabunge wataka uzalendo utekelezaji bajeti 2019/20

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WABUNGE wameuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 unaohalalisha kuanza kwa matumizi ya bajeti ya serikali iliyopitishwa na Bunge juzi, huku baadhi yao wakisisitiza bila moyo wa uzalendo na uadilifu kwa maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ukusanyaji wa mapato unaweza kuwa na doa.

Mbunge wa Sumve (CCM), Richard Ndassa, akichangia mjadala kuhusu muswada huo, alisema TRA inatakiwa kusimamia ukusanyaji wa mapato ili fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali katika bajeti ya mwaka 2019/20.

Juzi, Bunge lilipitisha bajeti kuu ya serikali ya Sh. trilioni 33.1 kwa mwaka mpya wa fedha wa 2019/20 baada ya wabunge 297 kuipigia kura ya wazi.

Ndassa alisema: "Tumepitisha bajeti ya Sh. trilioni 33.1 lakini nawasihi sana wenzangu maana ili tukusanye Sh. trilioni 33 ni lazima wafanyakazi wa TRA wawe na moyo wa uzalendo.

"Shati jeupe likiwa na doa hutalivaa tena. Niwaombe wafanyakazi wa TRA na BoT (Benki Kuu ya Tanzania) muwe wasafi na usafi uonekane ndani ya mioyo yenu kwani TRA ni kama moyo wa binadamu," aliongeza na kusisitiza TRA isipokusanya fedha vizuri itakuwa kazi bure.

Mbunge wa Ileje (CCM), Janeth Mbene, aliishauri serikali ilinde viwanda vya ndani kwa kuondoa baadhi ya tozo.

Alisema Tanzania kuna ardhi nzuri lakini haitumiki vizuri, hivyo akaitaka serikali kuitumia kwa kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora kwa kuwa kimekuwa kikitoa ajira nyingi kwa Watanzania.

Akionyesha hisia zake kuhusu namna sekta binafsi inavyoangaliwa na baadhi ya watu, Mbene alisema: "Bado tuko nyuma katika biashara, wengi hawajui biashara, mtazamo wao ni hasi kwa sekta binafsi. Tusione vibaya kuajiri watu ambao wanatoka sekta binafsi.

"Suala la taulo za kike ningependa sana kutoa angalizo zile zinazotoka nje, lazima nazo zitolewe ushuru, nataka kutoa ushauri kwa kipindi cha mpito ndani ya hii miaka miwili ihakikishe inawezesha upatikanaji wa taulo za kike kwa kuitumia MSD," alisema Mbunge huyo

Naye, Mbunge wa Moshi Mjini (Chadema), Japhary Michael, alisema kwa sasa wanaolipa kodi ni wachache, hivyo TRA inatakiwa kuhakikisha wafanyabiashara wakubwa na wafanyakazi wanalipa kodi.

"Wanaolipa kodi hawazidi milioni 2.5 kuna watu hatujawaingizwa katika mfumo wa kulipa kodi ambao ni wafanyabiashara wakubwa pamoja na wafanyakazi. Maoni yangu ni vizuri tutazame kwa picha pana namna gani tunasaidia ili mzigo huu usibaki kwa watu wachache.

Kwa upande wake, Mbunge wa Malindi (CUF), Ally Saleh, alihoji ni kwanini wabunge mpaka sasa hawajapewa mpango mkakati.

"Uchumi una nguzo zake ni lazima uzifuate bila kuzifuata huwezi kufanikiwa tupo hapa kupitisha bajeti kwa lazima tunataka kujenga uchumi lakini ni lazima uwe unatabirika.

"Lazima kwenye nchi kuwe na utulivu na ushindani halali, kwenye upande wa kodi kuna misingi ya kikodi lazima isikusanywe kwa bughudha. TRA wajisafishe waonekane kama ni wakusanya kodi na uwe na utamaduni wa kukusanya kodi.

Hii ya vilainishi nahisi inaibeba Air Tanzania ila iwe 'fair' angalau inaweza kuboresha," alisema.

Hata hivyo, Mbunge wa Kilindi (CCM), Omari Kigua, alisema TRA inatakiwa kutoa elimu pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kukusanya kodi ili wafanyabiashara waweze kuilipa.

"Kodi ndiyo kila kitu, moja ya sifa ya kodi lazima kuna mambo mawili ilipike kirahisi na walipaji wakubali kuilipa haya yanaweza kufanyika kwa kutoa elimu pamoja na kuweka utaratibu mzuri.

# HABARI KITAIFA



Muuza samaki wa jijini Dar es Salaam akitembeza bila ya kufunika ili kuzuia vumbi na wadudu kutua juu yake na kusababisha maradhi kwa wateja. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Sheria mpya yaifuta rasmi TFDA

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MAREKEBISHO ya Sheria ya viwango yaliyopelekwa bungeni, yamehamisha majukumu ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), inayosimamia masuala ya chakula na vipodozi kwenda Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Sasa, TFDA itabadilishwa jina rasmi na kutambulika kama Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema sehemu ya saba ya sheria hiyo inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Viwango, sura ya 130.

Kufutia hatua hiyo, sasa TBS itachukua jukumu la kuunganisha utaratibu wa usajili wa majengo, usajili wa bidhaa, udhibiti wa bidhaa za ndani na udhibiti wa bidhaa kutoka nje.

"Marekebisho ya Sheria ya Viwango, sura ya 130 ili kuhamisha majukumu ya kusimamia masuala ya chakula na vipodozi kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ambayo inasimamia majukumu hayo kwa sasa."

"Sehemu ya nane kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura ya 219 ili kuondoa TFDA jukumu la kusimamia chakula na vipodozi."

Aidha, Dk. Kijaji, ameeleza kuwa marekebisho hayo yanapendekeza kubadilisha jina la Mamlaka ya 'Tanzania Foods and Drug Authority' ili kuwa Tanzania Medicines and Medical Devices Authority (TMDA).

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo wa Fedha, TMDA itaendelea na kusimamia dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuongeza ufanisi katika eneo hilo.

Pia, muswada huo unakusudia kuzifanyia marekebisho sheria tisa zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru na tozo kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali ili kuweka mfumo wa kodi ambao ni tulivu na unaoratibika.

## Treni 3 za mizigo zaja

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Reli (TRC), Masanja Kadogosa, amesema wanatarajia kuingiza treni za mizigo tatu zenye uwezo wa kubeba tani 10,000 mwezi ujao.

Kadogosa alisema hayo jana katika ziara ya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliotembelea miradi ya mikakati ya mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

"Tupo katika hatua za mwisho za ununuzi wa treni za mizigo na abiria ambazo muda wowote baada ya ununuzi kukamilika zitaanza safari," Kadogosa alisema.

Alibainisha kuwa treni hizo zitafanya safari zake kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro na Morogoro hadi Makutupola mkoani Dodoma, maeneo ambayo ujenzi wa reli ya kisasa unaendelea.

Alisema mradi wa ujenzi wa reli hiyo kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika kwa asilimia 54 wakati kipande cha Morogoro hadi Makutupola umekamilika kwa asilimia 13.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Julius Ndyamkama, akizungumza katika ziara ya wajumbe hao kuhusu mradi wa Terminal III, alisema umekamilika na wanatarajia Julai 22 hadi 31 kuanza kuhamisha ndege kwa awamu.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mara, Samwel Nambatatu, aliwaomba wananchi kumuunga mkono Rais John Magufuli kwa hatua anazozichukua kuimarisha uchumi wa nchi.

Mwenyekiti wa Mkoa wa Kusini Unguja wa CCM, Ramadhan Abdalah Ally, alisema katika miaka mitatu na nusu ya Rais Dk. Magufuli, ameshamaliza utekekezaji wa ilani.

## UDSM kufundisha Kiswahili Ethiopia

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimesema kinatarajia kuanza kufundisha Kiswahili Ethiopia Septemba mwaka huu kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini humo.

Hatua hiyo imetokana na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Rais John Magufuli na serikali ya nchi hiyo juu ya matumizi ya Kiswahili nchini humo alipofanya ziara ya kikazi.

Naibu Makamu Mkuu-Taaluma wa UDSM, Prof. Bonaventure Rutinwa, alieleza mpango huo jijini Dar es Salaam jana, akibainisha kuwa programu za kufundisha zitaanza Septemba mwaka huu katika ngazi ya cheti, stashahada na shahada katika Chuo Kikuu cha Addis Ababa. "Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitatoa na kudahili wakufunzi wa Kiswahili, kitaandaa mitaala ya kufundisha Kiswahili na kutoa vitabu vya kufundishia Kiswahili kama lugha ya pili," Prof. Rutinwa alisema. Aliongeza kuwa UDSM kitatumia wataalamu wake walioko katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili pamoja na walimu wa Kiswahili wenye sifa stahiki za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni.

Alisema UDSM kitaandaa idadi ya kutosha ya wahadhiri na walimu wa kufundisha lugha hiyo ili kukidhi mahitaji kwa viwango vya juu. Lugha ya Kiswahili imekuwa ikikua kwa kasi katika baadhi ya nchi za Afrika. Pia, tayari baadhi ya nchi za Ulaya zimeanza kufundisha Kiswahili katika vyuo vyake.

Baadhi ya nchi ambazo tayari zimeshaanza kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na mitaala shuleni ni Afrika Kusini na katika vikao vya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) imekuwa ikitumika kama lugha rasmi ya mawasiliano.

Rais Magufuli alipofanya ziara nchini Namibia hivi karibuni, alitoa zawadi ya vitabu vya kusoma na kufundishia lugha ya Kiswahili kwa Rais wa nchi hiyo, Dk. Hage Geingob, walipofanya mzungumzo katika Ikulu ya Windhoek.

Vilevile, Mei 26, mwaka huu, Rais Magufuli alifanya mazungumzo na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, Ikulu jijini Pretoria na akamkabidhi zawadi ya vitabu vya kusoma na kufundishia lugha ya Kiswahili kutoka UDSM.


VisionFund TANZANIA

**VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED**

**VACANCIES**

VisionFund Tanzania Microfinance Bank Ltd (VFT MFB) formerly known as SEDA is a fast growing and reputable Micro Finance Bank (MFB), has a loan book of Tshs. 24 billion and 54,000 customer base, more that 5,000 of them being small holder farmers. VFT is seeking to employ dynamic and committed Tanzanian young men & women who have passion for people's economic development to fill in the vacant positions detailed here below:

**Work reference no 9 -**

**Position : Head of Risk and Compliance**
**Reporting to : Chief Executive Officer**

**Responsibility:**
- Identify risks, prioritize and measures current and foreseeable risks
- Ensures that Risks are kept within the scope
- Develop clear annual Risk objectives for VFT MFB
- Asses and identify risks areas of implementing audit findings, regulators concern and other bodies.

**Main tasks**
1. Heads & Supervisors Risk and Compliance Department
2. Identify risks, prioritize and measures current risks
3. Ensures that Risks are kept within the scope
4. Develop clear annual Risk objectives for VFT
5. Asses and identify risks areas of implementing audit findings, regulators concern and other bodies.
6. Develop Risk Policy for VFT and Compliance standard
7. Responsible for AML/CFT cases and ensure proper handling of the case
8. Trains and orient staff on AML and CFT awareness
9. Work with Board Credit and Risk Committee
10. Responsible for developing and implementing of Compliance Monitoring Plan.
11. Conducting training to VFT-MFB staff on bank policies and procedures, legal and regulatory requirements, as well as consumer protection

**Education/Experience**
- Master /Post graduate in Business Administration, Finance, Risk Management
- Bachelor Degree in marketing, Business Administration/Law/Accounting, Risk Management
- Very good knowledge of oral & written English
- Very good analytical & reporting skills
- 5 years' experience in credit management
- 3 years' experience in supervisory role

**Special / Personal Abilities**
- Highly developed sense of reliability and correctness
- Very good communication skills and an effective trainer
- Innovative and analytical
- Very good planning skills
- Must have above average skills in using Micro Soft office applications
- Must be a self-starter, highly motivated, organized, and detail-oriented
- Committed Christian

**About our working environment & remuneration**

VisionFund Tanzania Microfinance Bank has a calm and harmonious working environment where employees are highly valued. Good work is recognized and rewarded accordingly and there is an opportunity to grow professionally and spiritually.

**Mode of Application**

Application letters stating the position applied with photocopies of certificates and CV's with three referees should be sent EITHER online to **vftHRstaff@vftz.co.tz** OR through the postal address below.

**The Chief Executive Officer, VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited**
**P.O. Box 1546, Arusha. TANZANIA.**

The application to reach VFT-MFB not later than two weeks after the first appearance of this advertisement

N.B. Only short-listed candidates will be contacted

**Disclaimer**

VisionFund Tanzania Microfinance Bank would like to inform the general public that it has not engaged any consultant/agent to conduct recruitment on its behalf

215295702

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wachakachuaji wa vipimo ununuzi mazao wabanwe

**MOJA** ya changamoto kubwa ambazo zimekuwa zikijitokeza na kuwakwaza wakulima pamoja na sekta nzima ya kilimo, ni wanunuzi wa mazao kutumia vipomo vilivyochakachuliwa.

Hali hiyo imekuwa ikiathiri wakulima, kwa sababu wanapunjwa na kunyonywa na wanunuzi, ambao lengo lao ni kujinufaisha kwa kupata faida kubwa.

Sababu za kuwapunja hazieleweki, lakini kinachoonekana ni kuwa huko nyuma mamlaka zetu hazikuwa zinasimamia kwa umakini, hivyo baadhi ya wanunuzi wasio na nia njema kuitumia fursa hiyo kufanya utapeli huo.

Usimamizi na utaratibu wa shughuli zote za ununuzi wa mazao unahitaji kuongozwa na sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali kutoka wizara, bodi za mazao na mamlaka nyingine, ikiwamo Wakala wa Vipimo (WMA).

Bila mambo hayo kutumika, matokeo yake ni kuwa wakulima wa mazao mbalimbali hususan ya biashara kama pamba, tumbaku, korosho, chao, kahawa na mengine ununuaji wake utakuwa na matatizo, na watakaopata shida na kuathirika ni wakulima.

Katika kutekeleza majukumu yake, WMA umewakumbusha wanunuzi wa mazao ya tumbaku, ufuta na pamba kutumia vipimo sahihi, vinginevyo watakabiliwa na kifungo cha miaka mitano jela na faini ya Sh. milioni 100.

Hayo yalisemwa na Meneja wa WMA Mkoa wa Katavi, Phanueli Matiko, wakati wa kukagua mizani itakayotumika katika msimu wa mazao hayo, ambapo alisema wakala huyo yuko macho kuhakikisha wakulima wa mazao hayo wanapata kipato kulingana na kile walichokizalisha.

Alisema Sheria ya Vipimo Sura Na. 340 na mapitio yake ya mwaka 2002 imeboreshwa na imekuwa kali na endapo mnunuzi atajihusisha na uchezeshaji wa vipimo. Aidha alisisitiza kuwa endapo mtuhumiwa atakamatwa na kosa kwa mara ya pili na kuendelea na akikutwa na hatia mahakamani, adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi milioni 100 au kifungo kisichozidi miaka mitano (5) au vyote kwa pamoja.

Kadhalika, mtuhumiwa akikamatwa na kukiri kosa lake, papo hapo atatozwa faini kati ya Sh. 100,000 hadi milioni 20 kulingana na makosa aliyotenda.

Matiko alisema sheria hiyo inakwenda mbali zaidi kwani endapo mtuhumiwa atakataa na kufikishwa mahakamani kwa kosa la kwanza, atatozwa faini isiyopungua Sh. 300,000 na isiyozidi milioni 50 au kifungo cha miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Alisema hadi juzi, WMA imeshafanya ukaguzi wa vipimo mbalimbali vitakavyotumika kununulia mazao, ambapo kwa ufuta pekee jumla ya mizani 31 imehakikiwa katika wilaya za Mlele (11), Tanganyika (12) na Mpanda mizani (8).

Katika ununuzi wa tumbaku jumla ya mizani 35 imehakikiwa na kati ya hiyo, 18 imehakikiwa katika Wilaya ya Mlele, 17 Wilaya ya Tanganyika.

Kwa kutambua changamoto za vipimo na athari kwa wakulima wetu, tunaishauri WMA kuhakikisha inazitumia sheria zilizopo hususan za adhabu dhidi ya wanunuzi wote wa mazao wanaokiuka sheria ili watozwe faini, vifungo na wale ambao wataendeleza ukaidi wafungiwe kabisa kununua mazao.

Serikali isikubali kuwapa mwanya wa kuendeleza unyonyaji na wizi dhidi ya wakulima na taifa kwa ujumla. Tunaamini kuwa kuliweka sawa suala hili, kutaweka mazingira rafiki ya ununuzi wa mazao.

Pia wakulima watahamasika kwa kuzalisha mazao zaidi na kuchangia katika ujenzi wa viwanda na kuipeleka nchi yetu katika uchumi wa kati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





### Muungwana Lazima Nilonge

## Adhabu ya viboko kufutwa shuleni inawezekana

Na Joseph Mwendapole

**VIBOKO** shuleni vifutwe au viendelee ili kudhibiti nidhamu ya wanafunzi ni mjadala ambao bado unaendelea kwenye mikutano na majukwaa mbalimbali.

Serikali yenyewe haijakataza rasmi adhabu ya viboko shuleni ingawa inasema mwalimu anayemwadhibu mwanafunzi afanye hivyo kwa staha na kwa kufuata kanuni na sheria.

Kwa muda mrefu serikali imekuwa ikisita kuondoa kabisa adhabu ya viboko kama wadau wengi wanavyolalamika kwamba vimekuwa vikitumika kuwadhalilisha na wakati mwingine kuumiza wanafunzi.

Pengine ni kwa hofu kwamba kuondoa kabisa viboko shuleni kunaweza kusababisha mmomonyoko wa maadili kwa maana kwamba wanafunzi wanaweza kuwa na viburi na wakawa hawadhibitiki.

Wadau wanaotoa hoja ya kufutwa kwa viboko nao wanakuja na hoja zao kwamba kuna ushahidi unaoonyesha kwamba mwanafunzi anaweza kudhibitiwa shuleni bila hata chembe ya viboko.

Wadau hao walitoa mifano ya baadhi ya shule hapahapa Tanzania ambazo wanafunzi wake hawachapwi viboko lakini bado wana nidhamu ya hali ya juu.

Baadhi ya wadau wana maoni kwamba mwalimu anaweza kutumia mbinu mbalimbali kudhibiti tabia ya mwanafunzi bila kutumia nguvu ya viboko.

Wakizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyoandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), wanafunzi wengi walionyesha kutokubaliana na suala la viboko shuleni.

Wanafunzi hao walisema adhabu za viboko si suluhisho la kurekebisha tabia za wanafunzi na kushauri utafutwe utaratibu mpya wa kuwakuza kwenye maadili mema. Enock Haule ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Benjamin Mkapa alisema adhabu zinazotolewa shuleni zinakwaza wanafunzi na baadhi yao wameamua kuacha shule na kuingia mtaani.

"Mimi nina ushahidi wa rafiki yangu ambaye alikuwa anapigwa mara kwa mara na mwalimu wa nidhamu hivyo alivyoona shule imekuwa kama mateso aliamua kuachana na shule na sasa yuko mtaani," alisema.

Wanafunzi wa shule nane za sekondari na msingi za jijini Dar es Salaam, ambazo ni Tuliani, Tandika, Kibasila, Benjamin Mkapa, Saku, Makumbusho na Shule ya Msingi Mikocheni walishiriki maadhimisho hayo.

Kwa kuwa baadhi ya walimu wamekuwa wakiitumia vibaya nafasi ya kuwarekebisha wanafunzi kwa kuwapa adhabu zilizopitiliza, Muungwana anaona kuna haja kwa serikali kuondoa kabisa adhabu za viboko na kutafuta mbadala wake.

Wenzetu walioendelea wamekuwa na namna nyingi za kumwadhibu mtoto bila kumchapa viboko lakini adhabu hiyo ikawa kubwa kwake kiasi kwamba hawezi kurudia kosa lake. Kuna adhabu ambazo zimekuwa zikitumiwa na nchi za Magharibi kama kumnyima mwanafunzi fursa ya kwenda kucheza wakati wa mapumziko au kwenda matembezi ya shule ambazo humfanya mtoto kujihisi mpweke na aliyetengwa na jamii anamoishi.

Baadhi ya wadau wanasema adhabu laini kama hizo zimekuwa zikitolewa kwenye mataifa mengi na wamefanikiwa kuwa na wanafunzi wasikivu na wenye maadili mema bila kuwa na viboko kabisa.

Kama kuna nchi zimefanikiwa kuachana na adhabu za viboko na adhabu ngumu na kuweka utaratibu wa kumwadhibu mwanafunzi kwa kutumia mbinu mbalimbali bila shaka na Tanzania hilo linawezekana.

Ni kwa mantiki hiyo Muungwana anaona kuna umuhimu wa kuachana na adhabu za viboko kwani baadhi ya walimu wamekuwa wakitumia mwanya huo vibaya.

Kwamba wamekuwa wakitumia mwanya huo kuwaadhibu wanafunzi adhabu kali na wakati mwingine kuwajeruhi na kuwaacha na ulemavu, ukiwamo ulemavu wa maisha.

Matukio ya walimu kujeruhi wanafunzi yamekuwa yakiripotiwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari kila siku na baadhi ya wanafunzi wamepoteza maisha kwa kuadhibiwa na walimu wao hivyo hoja za wanafunzi kwa mtazamo wa Muungwana zina mashiko.

## MJADALA/BARUA

# Kero hii ya kuvuta sigara hadharani ikomeshwe

**Mhariri Pole na majukumu ya kila siku**

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyonayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo.*

*Tabia hii inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*

*Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa utafiti toka vyanzo mbalimbali vya kiafya, inabainishwa kwamba moshi wa sigara unapomfikia mtu asiyevuta, humuathiri zaidi kiafya kuliko hata huyo mtumiaji mwenyewe.*

*Bahati mbaya zaidi hata pale wananchi wenzetu hawa wavutaji wanapokanywa ama kunasibiwa waache kuwakera wenzao, baadhi yao huziba masikio na wengine hutoa majibu yasiyofaa.*

*Ninaomba mamlaka zinazohusika zisaidie kulimaliza tatizo hili sasa kwa kuchukua hatua za kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaozidi kuvuta sigara sehemu za wazi ama za umma.*

**Lalida Bukuzu- Songea**

## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Wenye sifa changamkieni uboreshaji wa daftari hili




**Na Sabato Kasika**

KAZI ya kuboresha Daftari la Kudumu la Mpigakura inatarajiwa kuanza mwezi ujao, ili kuwapa fursa Watanzania ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 na zaidi kuingizwa katika daftari hilo.

Uboreshaji huo pia utakwenda sambamba na kurekebisha taarifa za wapigakura, kuhamisha taarifa za waliohama, kuwaondoa waliopoteza sifa na kutoa kadi mpya kwa waliozipoteza na zilizoharibika.

Hiyo ni kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), Dk. Athuman Kihamia, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kila Mtanzania mwenye sifa aweze kushiriki katika kuchagua viongozi anaowataka.

Dk. Kihamia alikaririwa na vyombo vya habari akisema hayo wiki iliyopita kwenye semina kwa wahariri na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Nec, kumefanyika uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapigakura baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, uliolenga kuweka vituo katika maeneo yaliyokubalika na pia kuweka angalau kituo kimoja katika kila mtaa au kijiji kwa kuzingatia umbali na idadi ya watu eneo husika.

Tume hiyo inafanya hivyo ili kuhakikisha kila mwenye sifa anaandikishwa na pia anashiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, hivyo kinachotakiwa ni kila mhusika kujitokeza mara uboreshaji huo utakapoanza.

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ni hitaji la Kikatiba ndio maana Nec inafanya hivyo.

Ni muhimu basi wenye sifa za kupiga kura kujitokeza kwa wingi ili waandikishwe.

Nec inasema Kanuni ya 15 (2) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari chini ya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa sura ya 292 inatambua majengo ya umma na yale ya wazi yanayofikika kwa urahisi kuwa ndio yanayotumika kuboreshea daftari.

Hivyo kuanzia wapigakura wapya, wasiokuwa na kadi za awali, ambao taarifa zao hazipatikani, taarifa zao zitatafutwa ndani ya mfumo na kama hazipatikani, wataandikishwa upya wakiwamo walipoteza kadi au kuharibika.

Maelezo hayo yanaonyesha kuwa hakuna Mtanzania mwenye sifa za kupiga kura atakayeachwa bila kuandikishwa, hivyo kinachotakiwa ni wahusika kufuata maelekezo yaliyotolewa na Nec.

Wafuate maelekezo ya kujiandikisha katika daftari hilo wakitambua kuwa hiyo ni fursa pekee ya kupata haki ya msingi kushiriki uchaguzi mkuu baadaye mwaka ujao na kumchagua kiongozi wanayeona anafaa.

Ninagusia suala hili kwa sababu kumekuwapo na changamoto mbalimbali miongoni mwa Watanzania, na hasa kufanya mambo kwa mazoea na mwisho wa siku wanajikuta wakikwama.

Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya watu hata kama wana nafasi ya kufanya jambo fulani ambalo wameelekezwa kulifanya ndani ya wiki moja, mwezi au miezi kadhaa, kusubiri hadi siku ya mwisho.

Mtindo wa aina hiyo imesababisha baadhi yao kukwama na kujikuta wakibaki hawana namna ya kufanya, kwa vile muda waliopewa umekwisha na hakuna mwingine tena.

Kuna mfano mingi ikiwamo wa kujiandikisha kwa ajili ya vitambulisho vya uraia.

Baadhi ya watu wakati huo walikwama baada ya kusubiri hadi siku ya mwisho na kujikuta wakikosa na sasa ndio wanahangaika kuvitafuta.

Kwa tabia kama hiyo huenda mara zoezi la kuandikisha wapigakura katika daftari hilo litakapoanza, wanaweza wakawepo watu watakaosubiri hadi siku ya mwisho na kujikuta wakikosa nafasi hiyo.

Wenye mtindo huo ni vyema wakatambua kuwa kusubiri hadi dakika ya mwisho kunaweza kuwakosesha haki yao ya kuchagua viongozi wanaowataka, kwa vile hawatakuwa na vitambulisho vya Nec. Nec imepanga kuweka vituo vya kuandikisha wapigakura katika maeneo yaliyokubalika na pia kuweka angalau kituo kimoja katika kila mtaa au kijiji kwa kuzingatia umbali na idadi ya watu wa eneo husika.


Kwa maana hiyo inasogeza vituo karibu na wahusika, hivyo ni muhimu kila mtu kujitokeza kwa wakati.

Kikubwa zaidi ni kwamba makosa ya kujiandikisha zaidi ya mara moja au kusahaulika katika daftari hilo kama ilivyojitokeza mwaka 2015 yasijirudie kwani yanaweza kuleta shida na kuzusha mijadala.

Hayo yakitokea, baadhi ya wanasiasa wanaweza kudai kwamba kuna uchakachuaji, ingawa wakati mwingine yanaweza kuwa ni makosa ya kibinadamu.

Hivyo kuepusha hilo ni muhimu basi kuongeza umakini katika uandikishaji.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED






Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya TPB, Dk. Edmund Mndolwa (wa sita kutoka kulia) akikabidhi mifuko ya saruji na mabati kwa ajili ya Shule ya Msingi Rumanyika iliyoko wilayani Karagwe. Wengine katika picha ni walimu, wanafunzi na viongozi mbalimbali wa wilaya hiyo na maofisa wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji Ramadhani atoa neno kuhusu uchaguzi

**Na Beatrice Shayo**

JAJI Mkuu mstaafu Agustino Ramadhani, amesema sio kila tatizo linalojitokeza katika uchaguzi husababishwa na kubatilishwa kwa matokeo au uchaguzi kurudiwa.

Jaji Ramadhani aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akifungua mkutano wa mafunzo kwa mawakili kuhusu mashauri ya uchaguzi ulioandaliwa na Kituo cha Utetezi wa Mtandao wa Haki za Binadamu nchini (THRDC),

"Kuna mafunzo yanayohusu kesi baada ya uchaguzi madai kwa yule aliyeshindwa kwenda mahakamani. Kuna kanuni nyingi sana za uchaguzi na uchaguzi unaendeshwa na binadamu kutakuwa na tatizo hapa na pale, lakini sio kila tatizo linaweza likafanya uchaguzi ule ukabatilishwa," alisema.

"Wanavyojiweka tayari na wanapofanya mafunzo yao jinsi ya kuendesha kesi mahakamani baada ya uchaguzi wanatakiwa kujua sio kila tatizo ni kupelekwa mahakamani inabidi kuangaliwe, je, hili ndio limemsababishia kushindwa au sio?" Alisema.

Pia alisema kwenye mashauri ya kesi za uchaguzi kuna tatizo katika upande wa mawakili, kulikuwa na kesi 134 zaidi ya robo tatu zilitupwa kwa sababu hazikufuata vigezo vya mashauri ambayo yanapaswa kwenda mahakamani.

Jaji Ramadhani alisema ni muhimu kwa mawakili kujiandaa vizuri sasa ili wanapokwenda mahakamani kusiwe na mashauri mengi yanayotupwa katika mchakato wa awali wa kupelekwa shauri mahakamani.

Aidha, Jaji Ramadhani amesema kuna umuhimu wa kuzingatia misingi ya haki za binadamu na mikataba mbalimbali ya kimataifa.

Naye Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema kuwapo kwa mawakili ni faida kwa taifa na mstakabali wa masuala yote ya sheria na utawala bora.

"Jopo hili ni endelevu tumeanza mwakani na mafunzo hayo yanawajengea uelewa katika mashauri yao kujua jinsi gani ya kusimamia mashauri ya uchaguzi," alisema.

Alisema wamekutana kwa siku mbili na wataanza kujifunza sheria za uchaguzi na namna ya kuendesha mashauri ya uchaguzi.

Vile vile, alisema baada ya hapo watachukua kundi jingine na kuwafundisha, lengo ni kuwa na mawakili ambao watasimamia mashauri hayo.

"Sio mawakili wanaonekana wale wale ndio wanasimamia kesi hizo. Kazi ya mawakili ni kuwatetea wananchi kupitia mahakama, hivyo wanatakiwa kujua mbinu na mikakati yote ya kutetea haki kupitia mahakama," alisema.

Naye Fransis Mlowe wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) alisema mafunzo hayo yatasaidia kujenga jopo kubwa la mawakili katika mikoa yote ambao watakuwa wapo tayari kwenda kuwasaidia wananchi.

Alisema wadau wanapojitokeza kuelimisha masuala ya sheria inasaidia kuwaongezea uelewa na kujua jinsi gani ya kuendesha mashauri ya kesi za uchaguzi kwa kuwa uchaguzi unakaribia.






# Twaweza yakwama kwa kukosa kibali NBS

INATOKA UK. 2

ya Mkurugenzi huyo ilishikiliwa na idara hiyo.

Hivi karibuni, Msemaji wa Idara ya Uhamiaji, Ali Mtanda, aliliambia gazeti hili kuwa bado wanaendelea kushikilia hati ya kusafiria ya Mkurugenzi huyo kwa muda usiojulikana.

Hati hiyo ilishikiliwa tangu Julai 24, mwaka jana na Idara hiyo ikisema kwamba inachunguza uraia wake.

Mmoja wa maofisa wa Twaweza ambaye aliomba jina lake lisitajwe, aliliambia Nipashe hivi karibuni kuwa wamejitahidi kuifuatilia hati hiyo kwa muda mrefu, lakini wameshindwa kupata majibu na kuelezwa uchunguzi unaendelea.

Alisema wamekuwa wakiandika barua mbalimbali wakiomba kupatiwa hati hiyo, lakini Idara hiyo imekuwa ikiwajibu kuwa inaendelea na uchunguzi ingawa hawasemi watakamilisha lini.

"Sisi tuna ofisi zingine Kenya na Uganda ambako alipaswa kwenda mara kwa mara kwa ajili ya shughuli za kiofisi, lakini amekwama kutokana na hati hiyo kuendelea kushikiliwa na Uhamiaji," alisema.

Alipotafutwa kuzungumzia suala hilo, Meneja Mawasiliano wa (NBS), Said Ameir, aliitaka Twaweza itaje tafiti hizo ili aweze kufuatilia na kutoa majibu badala ya taasisi hiyo kulalamika kupitia vyombo vya habari.

"Wataje hizo tafiti ni zipi na ni ngapi ili tufuatilie maana mimi sina taarifa za tafiti zao kukwama hapa NBS," alisema Ameir.

# Pwani kuwa kitovu cha uchumi

**Na Elizabeth Zaya,** PWANI

SERIKALI imetenga Bandari Kavu ya Kwala mkoani Pwani kusaidia kupunguza msongamano wa mizigo kwa Bandari ya Dar es Salaam.

Mkuu wa Mkoa huo, Evarist Ndikilo, alisema jana kuwa Pwani imepewa maelekezo na serikali kutenga eneo lenye hekta 120 kwa ajili ya kupokea makontena ya mizigo ili yasafirishwe maeneo mbalimbali ikiwamo nje ya nchi.

Alisema wameanza kutengeneza bandari hiyo na kwa awamu ya kwanza imetekelezwa kwa asilimia 60 na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

"Hili eneo litapokea makontena na wenye mizigo wataifuata bandarini hapo kwa ajili ya kusambaza maeneo mbalimbali na litakuwa kitovu cha uchumi kwa nchi, " alisema.

Mhandisi Ndikilo alisema kutokana na umuhimu wa eneo hilo, aliomba Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kuwapatia ekari 300 kwa ajili ya ujenzi wa mji mdogo wa Kwala na uwekezaji.

Pia aliwaalika wawekezaji kwenda kuwekeza kwa sababu mji huo utapangwa kulingana na matumizi kutokana na mwingiliano wa watu.

Ndikilo alisema katika mkoa wa Pwani pia kutatengwa eneo la maegesho makubwa ya magari eneo la Chalinze na Bandari.

Alitaja sifa za bandari hiyo kuwa ni kitovu cha uchumi, kuwapo na bomba la gesi asilia kwa sababu kwa sasa wako kwenye mazungumzo na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kwa ajili ya kuwawekea.

Hata hivyo, katika eneo hilo wanatarajia kujenga kituo cha polisi na daraja ili kuimarisha ulinzi na usalama.

# Bandari kinara zilizopitisha bidhaa za wanyamapori

**Na Salome Kitomari**

BANDARI za Dar es Salaam, Zanzibar na Mombasa ya Kenya kwa kipindi cha mwaka 2007 hadi 2017 zilitajwa kuwa kinara wa kupitisha na usafirishaji wa bidhaa za wanyamapori kwenda barani Asia.

Kwa mujibu wa mfumo wa takwimu wa kufuatilia biashara ya meno ya tembo, kwa kipindi hicho tani 403 zilikamatwa ikiwa ni sawa na tembo 54,460 waliouawa.

Aidha, asilimia 72 ya tembo na kakakuona walisafirishwa kwa meli na kiasi kidogo kilimakatwa kutokana na kukosekana ufuatiliaji wa kina na kukamata wanaohusika.

Mfumo huo umeonyesha kuwa mahitaji ya bidhaa za wanyamapori barani Asia ni tishio kwa wanyamapori kama faru, tembo na kakakuona barani Afrika.

"Kila mwaka kuna kuwa na matukio ya ujangili wa wanyamapori wanaoondoshwa na kusababisha upotevu wa mabilioni ya dola za Marekani kwa nchi zinazoendelea, ikiwamo mapato kwa nchi husika, huku fedha nyingi za nchi maskini zikitumika kupambana na majangili na mtandao wa ujangili wa wanyamapori," ilibainisha.

Nipashe ilitembelea Bandari ya Dar es Salaam hivi karibuni, uongozi ulieleza ugeni wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), waandishi wa habari wa Tanzania na Thailand, kuwa kuna scana nane ambazo kwa wakati huo sita zilikuwa zinatumika na nyingine ni za zaida.

Walisema scana hizo ni za kisasa na zina uwezo wa kutambua chochote kwa picha kilichopo kwenye makontena, na kwamba zinafanyakazi kila siku kwa saa 24.

Naye, Mkuu wa kitengo cha udhibiti wa makontena wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kilichopo Bandari ya Dar es Salaam, Emmanuael Msambwa, alisema takwimu za dunia zinaonyesha kuwa kontena milioni 720 husafirishwa kwa mwaka bila kukaguliwa na asilimia mbili pekee ndiyo hukaguliwa.

"Tunapata taarifa za kuingizwa kwa kontena lakini ni ngumu kupata taarifa za usafirishwaji wake, lakini hali inabadilika kutokana na hatua zinazochukuliwa kila siku," alisema.

Alisema kontena hizo za dunia nyingi zinamilikiwa na watu wenye mtandao mkubwa duniani na wenye fedha nyingi, na hubeba bidhaa za wanyamapori na maliasili kwa ajili ya masoko ya Asia.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Msaidizi wa Kuzuia Ujangili nchini, Robert Mande, aliwaambia waandishi wa habari kuwa serikali ya awamu ya tano imepambana na ujangili kwa kiasi kikubwa kwa kusambaratisha mtandao wa ujangili ambao ulikuwa haukamatiki.

Alisema kwa sasa kila kanda kuna vikosi kazi vya kupambana na ujangili ambavyo vinajumuisha mamlaka zote za nchi, ambazo hukamata na kuchukua hatua hata kwa viongozi wa juu ambao awali walikuwa hawaguswi.

Alisema changamoto kubwa kwa sasa ni mtandao wa watu walio kwenye ngazi ya maamuzi serikalini na kwenye siasa kujihusisha na biashara hiyo, na kwamba wameimarisha mbinu za kuwakamata na hatua zinachukuliwa.

"Mtaalamu akijiingiza kwenye rushwa kughushi inaitwa "white color crime' tumegundua ndilo tatizo kubwa kuliko lote, ushiriki wa wataalamu maeneo mbalimbali ndiyo unasababisha uhalifu kuendelea na kuwa mgumu kupambana nao," alisema.

Naye, Mwanasheria wa Shirika la Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Wanyamapori Tanzania (Traffic), Linah Clifford, alisema Tanzania inatajwa kuwa vizuri kwenye kuhukumu wanaokutwa na hatia ya kuhusika na ujangili wa maliasili na wanyamapori.

Kesi zilizotikisa za watu ambao walikuwa hawakamatwi ni iliyohukumiwa mwaka 2017, ya Boniface Maliango maarufu kama Shetani, aliyehukumiwa miaka 12, ambaye anadaiwa kuua tembo zaidi ya 1,000 na kuwa na mtandao wa ujangili katika nchi mbalimbali za Afrika.

Nyingine mwaka 2018 ni ya raia wa China Yang Feng Glan maarufu kama Malaika wa Tembo, alihukumiwa miaka 17 jela kwa kuwa mfadhili mkuu wa mtandao wa ujangili Afrika, ambayo ilisambaratisha mtandao wa ujangili.




Wakazi wa jijini Dar es Salaam wakipita kwenye njia ya waenda kwa miguu eneo la Mwenge, ambalo hata hivyo, sehemu ya njia hiyo imevamiwa na wamachinga. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waziri aeleza changamoto ya uzalishaji wa maziwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema licha ya kuwapo kwa mifugo ya kutosha nchini, bado uzalishaji wa maziwa si wa kuridhisha na kuifanya serikali kutumia zaidi ya Sh. bilioni 30 kila mwaka kwa ajili ya kuagiza maziwa nje.

Kutokana na changamoto hiyo, amewataka wadau na taasisi mbalimbali zikiwamo za dini kuwekeza viwanda vikubwa na vidogo vya kuchakata maziwa ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa ndani ya nchi badala ya kuendelea kuagiza toja nje ya nchi.

Ulega alisema hayo katika Kongamano la Elimu Mvomero mkoa wa Morogoro la kuwajenga wananchi na pia kuhamasisha jamii za wafugaji kufuata ufugaji wenye tija.

Alisema mchango wa mifugo kitaifa ni mkubwa, kwani kwa sasa inachangia pato la taifa kwa asilimia saba, na jukumu moja wapo la wizara ni kusambaza teknolojia sahihi za ugufaji bora ili kuongeza uzalishaji wenye tija na hivyo kuchochea uwekezaji katika sekta ya mifugo.

"Leo tunaagiza maziwa mengi sana kwa mwaka tunatumia chini ya Sh. bilioni 30 kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi tena ni ya unga wakati maziwa ya wafugaji yamejaa sehemu mbalimbali na hapa Morogoro, hakuna wa kuyanunua na yanamwaga," alisema Naibu Waziri Ulega. Aliwataka wafugaji wabadilishe mfumo wafuge kisasa ili ng'ombe wa maziwa waweze kutoa maziwa mengi na kupata faida kubwa itakayowainua kiuchumi pamoja na kuliingizia taifa mapato.

Naye Askofu Jacob Ole Mameo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Morogoro, alisema jamii ya wafugaji wa Kimasai ndani ya mkoa huo ipo nyuma katika masuala ya elimu za hasa watoto wa kike.

Askofu Mameo alisema licha ya serikali kuhimiza suala la elimu, pia kanisa hilo linafanya juhudi ya kuielimisha jamii hiyo ili iweze kutambua umuhimu wa elimu kwa kuwasomesha watoto wao.

# Watoto 1,171 wajifungua

**Na Marco Maduhu,**

SHINYANGA

WATOTO 1,171 walio chini ya umri wa miaka 18 wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamebainishwa kujifungua kutokana na tatizo la mimba na ndoa za utotoni.

Hayo yamebainishwa juzi na Ofisa Muuguzi kutoka Hospitali ya Wilaya ya Kahama, Nyanjura Mjuberi, kwenye kikao cha Shirika la Agape na Kiwohede cha kufunga rasmi mradi wa elimu ya afya ya uzazi na ujinsia kwa vijana, na kuukabidhi rasmi serikalini ambao ulilenga kutokomeza tatizo la mimba na ndoa za utotoni.

Alisema takwimu za watoto hao kujifungua ni za miaka mitatu mfululizo, ambapo mwaka (2017) walijifungua 664, (2018) 416, na (2019) kuanzia Januari hadi Machi wameshafika 91, na kuwataka wanaume kuachana na tabia ya kuwabebesha ujauzito watoto pamoja na kuwaozesha ndoa za utotoni.

"Mtoto mdogo anaposhika ujauzito ni hatari sana kwa afya yake ambapo viungo vyao vya uzazi vinakuwa havijakomaa, na wengi wao hujifungua kwa njia ya upasuaji, hivyo naomba elimu iendelee kutolewa kwa jamii juu ya madhara ya kufanya mapenzi na watoto wadogo," alisema Mjuberi.

"Pia nalipongeza Shirika hili la Kiwohede ambalo lilikuwa linatekeleza mradi wake wilayani Kahama wa kutoa elimu ya afya ya uzazi na ujinsia kwa vijana, ambao umetusaidia kupunguza idadi ya watoto kuja kujifungua watoto wenzao kwenye hospitali yetu, tofauti na hapo awali kama nilivyobainisha takwimu," aliongeza.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape, John Myola, akiwakilisha pia na Shirika la Kiwohede, alisema mashirika hayo mawili yalikuwa yakitekeleza mradi wa elimu ya afya ya uzazi na jinsia kwa vijana tangu 2017 na kukoma Juni mwaka huu, ambapo Agape walikuwa Shinyanga Vijijini na Kiwohede wilayani Kahama.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Rashidi Mfaume, akimwakilisha Katibu Tawala wa mkoa huo, Albert Msovela, alipongeza mashirika hayo kwa kazi ambayo wanaifanya ndani ya jamii, na kuahidi kuyaendeleza mapambano ya kutomeza kabisa mimba na ndoa za utotoni.

# Hatima madereva malori wasio na mikataba ya ajira Jumatatu

OFISI ya Waziri Mkuu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inatarajia kutoa tamko ndani ya siku mbili kuhusu hatua gani zitachukuliwa kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, kwa madereva wa malori na mabasi wasio na mikataba ya ajira.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Tunduma (Chadema), Frank Mwakajoka.

"Serikali iliahidi kufanya marekebisho na kuboresha mkataba wa ajira wa madereva uliokuwapo tangu mwaka 2015, je, serikali ina mpango gani wa kuharakisha jambo hili ili wafanyakazi hao wapate mikataba ili kuepusha migomo ambayo imekuwa ikitokea mipakani?" Alihoji.

Mavunde alijibu kuwa serikali inakuja na mpango mkakati ambao hatua ya kwanza ni kuwataka wamiliki wote wa mabasi na malori ambao watakwenda Sumatra kuomba leseni ya usafirishaji kuhakikisha kwamba wanawasilisha na mikataba ya wafanyakazi.

"Hili ni eneo la kwanza kuhakikisha madereva wanakuwa na mikataba na serikali imekuja na mkakati tofauti kwa kuwa tuliona kuwa uliopo ulikuwa una mianya ya utekelezaji wake," alisema.

Mavunde alisema kwa mkakati huo uliowekwa ni kwamba kila dereva wa nchini atakuwa na mkataba wake na watahakikisha kuwa kila mmiliki wa chombo cha usafiri anafuata masharti ya sheria kama kifungu cha 14 kinavyosema cha sheria za ajira na uhusiano kazini.

"Nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba si maneno tu bali mkakati umeshawekwa vizuri na tumekaa na Jeshi la Polisi na muda si mrefu kuanzia Julai mosi mwaka huu wataona cheche za wizara," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itasimamia na kuhakikisha madereva wa malori na mabasi wanapata mikataba ya ajira ili kuboresha maslahi yao na kuongeza ufanisi katika utumishi wao kazini.

Mavunde alifafanua kuwa katika kushughulikia haki na maslahi ya madereva nchini Tanzania, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto zinazowakabili madereva, ambapo Mei 2, mwaka 2015 aliyekuwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, aliagiza iundwe kamati ya kudumu ya kutatua matatizo katika sekta ya usafirishaji chini ya uenyekiti wa katibu mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Uchukuzi.

Alisema kamati ndogo chini ya uenyekiti wa iliyokuwa Wizara ya Kazi na Ajira iliundwa kwa ajili ya kushughulikia, hakuna mkataba wa ajira wa madereva.

"Serikali kwa kushirikiana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi madereva na viongozi wa umoja wa wamiliki wa vyombo vya usafirishaji nchini, waliufanyia marekebisho na kuuboresha mkataba wa ajira wa madereva ulikuwapo," alisema.

Alisema mkataba ulioboreshwa uliidhinishwa na wadau katika kikao kilichofanyika Juni 23 mwaka 2015 na ilikubalika kwamba mkataba huo uanze kutumika rasmi Julai mosi mwaka 2015.

Aidha, alisema masharti yamewekwa kwamba kila mmiliki wa basi au lori anayeomba leseni ya usafirishaji toka Sumatra ni lazima awasilishe mikataba ya ajira ya madereva wake ambayo imehakikiwa na maofisa kazi wa maeneo husika.

Alibainisha Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kusimamia majadiliano baina ya vyama vya wafanyakazi, madereva na umoja wa wamiliki wa vyombo vya usafirishaji, ili kuwawezesha kufikia mwafaka wa viwango vya posho za safari na kujikimu wakati madereva wanaposafiri ndani na nje ya nchi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoa tamko la serikali kuhusu kauli ya Mbunge wa Starehe nchini Kenya, Charles Kanyi Njagua maarufu kwa jina la Jaguar, bungeni jijini Dodoma, juzi. **PICHA: OWM**

## Serikali yafafanua sampuli minofu samaki Ziwa Rukwa

BUNGE limeelezwa sampuli za minofu ya samaki zilizochukuliwa katika Ziwa Rukwa zinaendelea kuchakatwa ili kujua kiwango cha zebaki na risasi katika minofu hiyo.

Sambamba na hilo, pia kuangalia kiasi hicho kama kipo ndani ya viwango vinavyokubalika na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Lupa (CCM), Victor Mwambalaswa.

Mbunge huyo alisema miaka ya karibuni samaki aina ya Ngege katika ziwa hilo wamepungua sana ukubwa na inatokana na uchimbaji wa dhahabu Wilaya ya Chunya na Songwe ambao mara nyingi ulihusisha zebaki.

Akijibu, Ulega alisema miaka ya nyuma samaki hao walikuwa wakubwa kutokana walikuwa hawakabiliwi na changamoto zinazowakabili sasa.

"Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), mwaka huu katika Ziwa Rukwa ilibainika kuwa kuna udumavu wa upungufu katika ziwa hilo na hasa samaki wa jamii hiyo," alisema.

Aidha, alisema ndege aina ya Oreochromis rukwaensis ni wa asili katika ziwa hilo, wamepungua zaidi kulingana na ndege aina ya Oreochromis esculentus ambao wamepandikizwa.

"Udumavu na upungufu wa samaki katika ziwa hilo unasababishwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uchafuzi wa mazingira utokanao na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu," alisema.

Alitaja shughuli hizo kuwa ni kuongezeka kwa mifugo inayotegemea ziwa kupata maji na malisho pembezoni, kilimo kisichofuata taratibu karibu ama pembezoni mwa ziwa, uchimbaji madini ya dhahabu ambapo zebaki hutumika kuchakata.

"Pia ongezeko la matumizi ya petroli katika machimbo ya dhahabu ambapo petroli hiyo yaweza sababisha madini ya risasi kuingia ziwani," alisema.

Pamoja na hayo, alisema uvuvi haramu ambao wavuvi hutumia makokoro na nyavu zisizoruhusiwa na usiozingatia taratibu za kulinda rasilimali za uvuvi na mazingira unaendelea kushamiri katika eneo hilo.

"Uvuvi huo unahusisha makororo na nyavu zisizoruhusiwa kama vile matumizi ya vyandarua," alisema.




**Habari zote na Godfrey Mushi,** DODOMA

## 400 walipwa bil. 2.6/- kupisha ujenzi barabara

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, amesema wananchi 433 wamelipwa fidia kiasi cha Sh. milioni 2,608.6 ili kupisha ujenzi wa mradi wa barabara ya Makutano-Sanzate yenye urefu wa kilometa 50.

Kwandikwa alitoa kauli hiyo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Serengeti (CCM), Marwa Chacha, ambaye alisema barabara inayojengwa kuunganisha Mkoa wa Mara na Arusha inasuasua sana.

"Ujenzi unasuasua kwani tangu ilipoanza kujengwa 2013 mpaka leo hata kilometa 50 hazijakamilika. Je, serikali ina makakati gani dhidi ya ukamilishaji wa barabara hii?" Alihoji.

Alihoji pia ni lini wananchi waliofanyiwa tathmini watalipwa fidia zao.

Kwandikwa alisema barabara inayounganisha mikoa hiyo yenye urefu wa kilometa 452 kutoka Makutano juu (Musoma)-Natta- Mugumu-Loliondo hadi Mto wa Mbu ilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kukamilika mwaka 2013.

Aidha, alisema baada ya kukamilika kwa usanifu, ujenzi wa barabara hiyo umeanza kwa awamu ambapo kilometa 50 kutoka Makutano hadi Sanzate na kilometa 49 kutoka Wasso-Sale Junction unaendelea. Hata hivyo, alikiri kuwa mkandarasi amechelewa kukamilisha kazi kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali.

"Pamoja na changamoto hizo, Wizara kupitia Tanroads imeshachukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mkandarasi anamaliza kazi iliyobaki kwenye barabara ya Makutano-Sanzate inayotarajiwa kukamilika mwezi Septemba mwaka huu," alisema.

Alisema sehemu ya pili ya Sanzate-Natta yenye urefu wa kilometa 40 ipo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi.

"Upande wa Mkoa wa Arusha, kilometa 49 kutoka Wasso hadi Sale ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea," alisema.

Alisema wananchi wote waliofanyiwa uthamini wanaendelea kulipwa fidia zao kabla ya kazi kuanza.

"Mpaka sasa waathirika nane wamefidiwa kiasi cha Sh. milioni 12.8 kwa mradi wa Wasso-Sale kilometa 49. Katika mradi wa Makutano-Sanzate kilometa 50 wananchi waliolipwa fidia ni watu 433 kwa jumla ya Sh. milioni 2,608.5," alisema.

# Wataalamu wanyamapori watakiwa kuwekeza maeneo yaliyosahaulika

**Novatus Makunga,**
ARUSHA

WATAALAMU wa wanyamapori wametakiwa kuelekeza nguvu za utafiti katika maeneo ambayo yamesahauliwa na yenye utajiri mkubwa wa viumbe hai yaliyoko magharibi na kusini mwa Tanzania.

Wito huo ulitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, wakati akifungua mkutano wa nne wa pamoja wa wanasayansi kuhusu utafiti wa maliasili kupitia mradi ujulikanao kama African Bio Services, unaoendelea mjini hapa jana.

Profesa Mkenda alisema kuwa kwa muda mrefu kazi zao zimekuwa zikijikita zaidi katika maeneo ya uhifadhi yaliyo maarufu hususani ya ukanda wa kaskazini mwa nchi.

"Ninawataka watafiti na jumuiya ya wahisani sasa kubadilisha mwelekeo kwa kusaidia na kufadhili miundombinu itakayowezesha kufanyika kwa utafiti kwa maeneo ya kusini mwa nchi," alisema.

Profesa Mkenda aliwataka watafiti wa wanyamapori kuelekeza nguvu zao katika maeneo ya kipaumbele, yakiwamo ya uchumi wa jamii, migogoro kati ya binadamu na wanyamapori na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, alipongeza matokeo ya utafiti yaliyopatikana katika miaka minne ya mradi wa African Bio Services yakiwamo ya kukusanya taarifa mbalimbali ya kisayansi na kuhifadhiwa katika Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori nchini (Tawiri) ya Tanzania na taasisi kama hiyo ya Kenya.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa Tawiri, Dk. Simon Mduma, alisema kuwa mradi huo umekuwa na matokeo ya mafanikio kwa kuchangia kuimarisha ukusanyaji wa utafiti wa kisayansi, mafunzo na uboreshaji wa miundombinu ya utafiti. "Msingi wa mradi ni kuunganisha bioanuwai, ikolojia na huduma katika ikolojia ya Serengeti-Mara na kuwa na mkakati ambao unatoa mwelekeo bora na wa uhakika wa eneo hilo muhimu si kwa Afrika Mashariki pekee bali kwa dunia nzima," alisema.

African Bio Services ni mradi wa utafiti katika eneo la ikolojia ya Serengeti-Mara ukiwa na malengo ya kushughulikia mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la watu na matumizi ya ardhi ambayo yanaathiri bioanuwai na maisha ya watu, alisema Mduma.

Mradi huo wa miaka minne ulizinduliwa mwezi Juni mwaka 2015 ukidhamiwa na Umoja wa Ulaya (EU) kwa kiasi cha Euro 9,891,770, aliongeza.

Zaidi ya wataalamu wa wanyamapori 200 kutoka ndani na nje ya nchi wanakutana jijini Arusha kwa lengo la kupokea majumuisho ya kazi za utafiti zilizofanyika katika kipindi hicho cha miaka minne.



Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite, Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, Victor Kunyara, akizungumza na madalali na wanunuzi wa madini ya tanzanite jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# H'shauri Arusha kujenga wodi wazazi miezi saba

**NaCynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imeanza ujenzi wa wodi ya wazazi na watoto itakayogharamu Sh. bilioni 1.3.

Kazi hiyo ya ujenzi inayofanywa na kampuni ya ujenzi ya BQ ya Dar es Salaam, inafanyika kwenye Hospitali ya Wilaya iliyopo Engutoto, inatarajiwa kukamilika kwa miezi saba.

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, Meya wa Jiji la Arusha, Kalisti Lazaro na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya BQ, Mhandisi John Bura, mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro.

Akizungumza baada ya utiaji saini, Kaimu Mhandisi wa Jiji la Arusha, Samweli Mshuza, alisema jengo hilo ambalo ujenzi wake umeanza juzi, utachukua miezi saba na litakuwa ni ghorofa moja.

Alisema kazi hiyo ni mwendelezo wa ujenzi wa majengo ya hospitali hiyo ya wilaya, ambayo tayari jengo la wagonjwa wa nje (OPD), lenye ghorofa moja limeshakamilika na sasa linatoa huduma.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa kampuni ya BQ, Mhandisi Bura, aliwahakikishia viongozi kuwa ujenzi huo utakamilika ndani ya muda na anatarajia na kwamba kazi itakabidhiwa, Januari mwakani.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqaro, alisema, ujenzi wa hospitali hiyo, utapunguza msongamano wa wagonjwa wanaopata huduma kwenye Hospitali ya Mkoa ya Mount Meru.

Alisema upatikanaji wa dawa kwenye hospitali za serikali, vituo vya afya zahanati katika Wilaya ya Arusha ni asilimia 98.

Aidha, alisema majengo mengine yataendelea kujengwa kulingana na upatikanaji wa fedha na tayari huduma nyingine, zimeshaanza kutolewa, kwenye jengo lililokamilika.

Daqaro, alisema hiyo ni historia tangu uhuru, Wilaya ya Arusha ilikuwa haina hospitali ya wilaya na pia kwenye mipango iliyopo nia ilikuwa kujenga kituo cha afya cha kata ya Olasiti.

Aliongeza kuwa muda hautaongezwa, hivyo mkandarasi huyo awahakikishie kuwa anakamilisha ujenzi ndani ya muda uliowekwa.

Kwa upande wake Meya wa Jiji la Arusha, Kalisti Lazaro, alisema ujenzi huo, unafanywa kwa fedha za ndani na akatoa wito kwa wananchi kuendelea kulipa ushuru, tozo na kodi mbalimbali kwa kuwa manufaa yanaonekana.

Alisema atahakikisha jengo hilo linakamilika na hivyo kuweka historia ya kuwa meya wa awamu ya tano, ambaye alijenga hospitali ya wilaya.

# Tasaf makao makuu yaweka kambi Longido

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

MRADI wa kusaidia kaya maskini umekusudia kuwasaidia wanufaika wa miradi ya kupunguza umaskini kukuza uchumi wa jamii zao ili ziwe na maendeleo endelevu.

Jamii hiyo ya kaya masikini, katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido mkoani Arusha, itawezeshwa ili iweze kujitegemea hata pale mradi utakapofikia kikomo.

Akifungua mafunzo kwa wanufaika wa mradi huo unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) jana kwa wakazi wa Longido, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye ni Mkuu wa Idara ya Mifugo, Nestory Dagharo, alisema halmashauri inawalengwa 5,641 wanaonufaika na mradi wa kusaidia kaya maskini.

Alisema wilaya hiyo ina vijiji 49 lakini hadi sasa ni vijiji 27 ndiyo vilivyopo kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini, huku wanawake wanufaika na fedha hizo ni 3,296 na wanaume 227.

Dagharo alisema halmashauri hiyo ina vikundi 249 vinavyonufaika na miradi mbalimbali ya Tasaf na vimepiga hatua, katika nafasi ya kuweka na kukopa pamoja na kumudu mahitaji muhimu ya familia zao.

"Wamefikia hatua ya kuweka Sh. milioni 56 na hata sasa Sh. milioni 34 zimetolewa kama mkopo, hii ni hatua nzuri, mliofanikiwa kupata mafunzo haya nendeni mkawasaidie ambao hawajapata," alisema.

Alieleza kuwa hata vile vikundi ambavyo havipo, kwenye mpango wa Tasaf, hii ni fursa kwao kujifunza, alisema Dagharo. Mkuu wa Idara ya Mawasiliano inayeshughulikia malalamiko kutoka Tasaf, Makwinja Dismass, alisema ili kaya hizo ziweze kujikwamua na umaskini, ni wajibu wao kuwa na mikakati ya kutumia ruzuku ya msingi na yenye masharti pamoja na kujitengenezea ajira na vyanzo vya mapato.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha kaya hizo zinafikia hatua za kujimudu zenyewe kwenye elimu ya watoto, matibabu kwa bima na kuhakikisha lishe bora inapatikana na kupata milo mitatu kwa siku.

Alisema mafunzo haya ni ya siku tano na kwamba kuanzia leo maofisa watatembelea vijiji vilivyopo, katika mpango huu kuona namna wanavyo endesha miradi yao. Alisema kuwapo kwa vikundi vya ufugaji kuku, ng'ombe, mbuzi na kondoo pamoja na kilimo cha mboga kutawasaidia walengwa hao kukuza ya Olasiti.

Alisema ni muhimu kuwapa elimu ya namna watakavyoendesha miradi waliyoibuni kwa tija ili iwe endelevu.

Estomi Paul mtaalamu kutoka Halmashauri ya Longido, alisema changamoto kubwa inayowakabili ni matumizi ya lugha, pamoja na walengwa wa miradi ya Tasaf kutohudhuria vikao maalumu kwa maelezo wanataka kulipwa.

"Tunakwenda vijijini tunaitisha vikao, lakini hawatokei, ila ukitangaza vikao vya kupokea fedha hakuna anayekosa. Lugha ya vijijini ni Kimaasai nayo ni changamoto kwetu," aliongeza.

Mratibu wa Tasaf wilayani hapa Lobulu Saruni alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa shughuli zinazotekelezwa na taasisi hiyo na kwamba wilayani Longido vijiji 27 vitanufaika.







Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akimsikiliza Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) wilayani Hai, Cedrick Pangani, alipomtembelea ofisini kwake kwa ajili ya kutoa ripoti ya shughuli za mbio za Mwenge pamoja kupanga mikakati ya kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi kugombania mwili kuanza kusikilizwa kesho

**Na Mary Mosha,** MWANGA

MWILI wa kapteni mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Hussein Abdalah Seushi(65), umeendelea kuhifadhiwa kwa siku 11 katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, kusubiri uamuzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mwanga.

Kesi dhidi ya ndugu wa Seushi na mke wa marehemu imetajwa katika mahakama hiyo ya wilaya, kwa mlalamikaji Hashim Seushi kuomba haki ya kuuzika mwili huo, huku mlalamikiwa Mariam Msuya ambaye ni mke wa marehemu akipinga.

Kesi hiyo ya madai namba moja ya mwaka 2019, itaanza kusikilizwa kesho Juni 28, 2019 kati ya Hashim Abdalah Seushi ambaye ni mleta maombi dhidi ya Mariam Msuya ambaye ni mjibu maombi kuleta maelezo ya upande wa utetezi.

Kesi hiyo iliyopo chini ya Hakimu, Mariam Lusewa wa Mahakama ya Wilaya ya Mwanga, ilitajwa na kutoa nafasi kwa upande wa wajibu maombi kuleta maelezo yao.

Hakimu Lusewa aliutaka upande wa utetezi kupitia kwa wakili wao, Mhendeli Msaki kujibu maombi kutoka kwa wakili wa mleta maombi, Caessar Shayo ili kesi isikilizwe kesho.

Hata hivyo, kabla ya kutajwa kwa kesi hiyo, hakimu alitaka kujiridhisha kama mke wa marehemu Seushi, Mariam Msuya anaufahamu wa kina kinachoendelea katika mahakama hiyo.

Kutokana na mahojiano hayo, hakimu alihoji upande wa mleta maombi, kama kuna pingamizi lolote ambao haukuwa nalo hivyo upande wa mjibu maombi wametakiwa kupeleka maelezo yao Juni 28 mwaka huu.

# Viongozi waagizwa kuwasaidia wajane

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amewataka viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kusaidia wajane baada ya kufiwa na waume zao ili wapate haki.

Akizungunza na Nipashe ofisini kwake alisema katika mkoa wa Kilimanjaro wajane wengi wamekuwa wakinyanyaswa, kudhulumiwa mali zao na kutelekezwa mara baada ya waume zao kufariki, hali inayosababisha migogoro isiyokwisha kwenye familia.

Alisema wajane wengi wanapoteza haki zao baada ya waume kufariki hivyo hubaki na visasi, huzuni na ongezeko la watoto wa mitaani na wanaoishi kwenye mazingira magumu pia magonjwa kutokana na msongo wa mawazo au unyanyasaji wa watoto kingono.

"Nawaagiza viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kusimamia na kutetea haki za wajane wenzi wao wanapofariki ili kupunguza migogoro na dhuluma kwa wajane na watoto," alisema Mkuu wa Mkoa. Mghwira alisema, umefika wakati kinamama kuwa na sauti moja ya kukemea ukatili, ukeketaji na kurithiwa wajane mara baada ya waume kufariki hali ambayo inaleta ongezeko la mitafaruku ya familia na kukwamisha maendeleo.

Aliwaeleza viongozi hasa wa wilaya na mkoa wahakikishe wanafanya kazi ya usuluhishi wa migogoro, kutoa elimu kwa wananchi ili kuondokana na mila na desturi za ukandamizaji wa wanawake.

"Nawaomba viongozi wa dini kuombea amani, kuwapa wananchi wa mkoa huu matumaini mapya kwa kuwapa ushauri, nasaha za kuachana na vinyongo vilivyosababishwa na kudhulumiwa mali kwa muda mrefu," alisema Mghwira.

Alieleza kuwa vinyongo na hasira na mambo yanayofanana na hayo husababisha magonjwa mbalimbali ikiwamo saratani.

Faustina Msaki, ambaye amefiwa na mwenza alikiri kuwepo kwa ukatili kwa wajane mara baada ya wenzi wanapofariki na kuiomba serikali kukemea jambo hilo kwa vitendo bila kupokea rushwa kwa wenye nacho.

"Tunaiomba serikali mbali na kushiriki kwenye vikao vya familia na kutoa elimu, lakini pia mahakama zetu zisimamie sheria haki na usawa bila kumtizama mwenye nacho," alisema Elisaria Masawe mwenye miaka 61.

Aidha, kwa upande wake Mkurugenzi wa Shirika la Kutetea Haki na Msaada wa Kisheria (Kwieco) mkoani Kilimanjaro, Elizabeth Minde, alisema ikiwa Mkuu wa Mkoa, sanyari na watendaji wake watasimamia kwa vitendo changamoto zanazowakabili wajane zitapungua.

Alieleza kuwa wataweza kusaidiwa kwa haraka na tatizo la watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira magumu linaweza kuwa historia mkoani Kilimanjaro.

# CCM yacharuka wanasiasa kuwapa mimba wanafunzi

**Na Mary Mosha,** HAI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, kimekemea vitendo vya baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa wanaowakatisha masomo wanafunzi kwa kuwapa ujauzito.

Akizungumza na wanahabari ofisini kwake Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Hai, Laurence Kumotola, alisema siasa ni kioo cha jamii kwani maisha ya kila siku yanategemea uwepo wa tasnia hiyo.

Alisema endapo itaonekana wanasiasa wanafanya uovu kama kuwapa mabinti mimba, huchafua hata wanasiasa wengine ambao wapo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Hayo yanajiri baada ya mwanasiasa mmoja wilayani Hai hivi karibuni kushikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumpa ujauzito mwanafunzi wa Sekondari Malile wilayani hapo.

"Tunaiomba serikali na vyombo vyake vyote kuchukua hatua kali kwa wote wanaofanya vitendo hivyo na kwamba CCM Wilaya ya Hai, imechukizwa na kitendo hicho, kwa kuwa ni sehemu ya watu wanaowakatisha masomo wanafunzi kwa kuwapa mimba.

Aidha, Kumotola aliwaomba viongozi wa dini kulaani vitendo hivyo vibaya na kukemea matukio ya kuwapa mimba, kubaka na kuwalawiti watoto wakiwamo wanafunzi na kukatisha ndoto zao za kuendelea na masomo na kuwa na maisha bora.

"Badala ya kiongozi kuwaongoza wanafunzi ili waweze kupata elimu ambayo itawasaidia kimaisha, anakuwa sehemu ya kushiriki kuwarubuni na kuwanyanyasa kingono, hiki ni kitendo ambacho hatuwezi kukivumilia," alisema Kumotola.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Hai, Salome Zephania, awali akitoa taarifa ya matukio ya ukatili kwa watoto kwa kipindi cha Junuari 2018 hadi Mei 2019, kuna matukio ya ukatili 451 dhidi ya watoto.

Alisema waliobakwa walikuwa wasichana 58, wavulana waliolawitiwa ni 24 wakati wasichana walikuwa 23 na kwamba ni jambo ambalo halikubaliki.

"Inasikitisha kuona matukio ya mimba za utotoni na ubakaji yanafanywa na viongozi kwenye jamii zetu hili ni jambo la hatari na ni lazima wote tulikemee na tusilipe nafasi katika jamii inayotuzunguka," alisema Salome.

ama
ALHAMISI JUNI 27, 2019
AFYA NA MAZINGIRA




**Wanafunzi wafuatwa waliko kupewa darasa la kisukari**

Ukurasa 17



TFDA inavyopigana kumnusuru mlaji kutoka chakula chenye hatari ya sumu

Ukurasa 20



Ukurasa 16

**Picha kamili maradhi ya kisukari, mgonjwa anavyojinasua hatarini**

# Mapambano ya mifuko plastiki yameanza, daladala, mitaani bado mtihani mkubwa



Ukurasa 14



Mtu akiwajibika. **PICHA: MTANDAO.**

# Kufanya kazi saa nyingi chanzo cha kiharusi

**Na Mwandishi Wetu**

KUFANYA kazi kwa bidii kunaelezwa katika maeneo mengi 'kunalipa.' Lakini, watafiti wamefuatilia na kubaini kwamba, pia ina uhusiano wa karibu na mgonjwa na maradhi ya kiharusi.

Watafiti hao wanasema, iwapo mtu atafanya kazi kwa zaidi ya saa 10 kila siku na akitumikia hiyo kwa wastani wa siku 50 kwa mwaka, naingia katika hatari ya kupatwa na kiharusi. Pia, kuna ufafanuzi kwamba utendaji huo wa kazi ukiendelea kwa wastani wa mwongo mzima wanazidi kuwa karibu na tatizo hilo.

Hata hivyo wadau kutoka Chama cha Wenye Kiharusi wa Uingereza, wanasema ili mtu apatwe na kiharusi, ana mengi ya kufanya kujiweka mbali na janga hilo, kama vile kujitahidi kula vizuri na kufanya mazoezi.

Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Angers cha nchini Ufaransa, walifuatilia takwimu kama za umri wa wahusika, tabia ya uvutaji sigara, na kugundua zinachangia hali hiyo.

Wasomi wa Chama cha Wagonjwa wa Moyo wa Marekani katika jarida lao la kitabibu linalohusu afya, linasema wanaotumika muda mrefu kwa hesabu iliyotolewa ya mwaka mmoja, wana hatari ya robo yao (29%) kudhurika na wanaotumika kwa miaka 10, hatari inakaribia nusu yao (asilimia 45%).

Mtaalamu wa kiharusi, Dk. Richard Francis anasema: "Kuna mengi ya kufanyika, hata vitu vidogo vinavyoondoa hatari ya kiharusi, hata kama unafanya kazi kwa muda mrefu.

"Kula chakula bora, kupata muda wa mazoezi, kuacha sigara na kupata muda sahihi wa kulala, itakuletea mabadiliko makubwa kiafya."

MAZINGIRA

# Mapambano ya mifuko plastiki yameanza, daladala, mitaani bado mtihani mkubwa




Ujasiriamali ukiendelea katika mazingira yaliyo machafu.

**Na Beatrice Moses**

MARUFUKU ya utumiaji, uuzaji, uagizaji na utengenezaji wa mifuko ya plastiki nchini iliyoanza Juni Mosi mwaka huu, katika nadharia ya matarajio yake ni kulifanya jiji la Dar es Salaam kung'ara kwa usafi.

Kuna mengi yaliyoendana na hilo, ikiwamo kwa wanunuzi na wauzaji 'tutafungia nini bidhaa zetu.' Hapo nako kuna mjadala mrefu.

Ni wastani wa wiki nne sasa, hali imekuwa tofauti na matarajio katika uhalisia wa usafi na utunzaji wa mazingira kwa jumla.

Sababu hasa kwa kuwa baadhi ya watu walikuwa wakiitupa ovyo mifuko hiyo, huku wengine wakiitumia kama vyoo mbadala kwa kujisaidia haja kubwa na ndogo, kisha kufunga na kuitupa.

Pengine ni kutokana na kwamba bei ya mifuko hiyo ilikuwa ni rahisi ikilinganishwa na mbadala.

Hatua ya serikali kupiga marufuku matumizi na biashara za mifuko hiyo ya plastiki kwa kuwa, haiozi hata inapofukiwa ardhini, pia kuhatarisha maisha hadi hatua ya vifo kwa baadhi ya wanyama waliomeza vipande vyake, inaelezwa kuwa changamoto.

Ni mambo ambayo yaliyokwishafanyika utafiti na kuthibitika matokeo yake.

**MABASI MACHAFU**

Ni simulizi inayorejesha kwenye tukio la ndani ya daladala jijini Dar es Salaaam, linalofanya kazi kati ya Buguruni na Muhimbili, ambako abiria aliyekuwa amekaa katika kiti cha nyuma, alipaza sauti kumhoji kondakta kuhusu chupa iliyokuwa imejaa mikojo ndani ya gari.

Kondakta huku akiitika kwa kutetemeka, alijibu kwamba "watakuwa ni wapiga debe' ndiyo wamefanya uchafu huo."

Katika utetezi wake huo, kondakta alisema yeye na dereva wake waliacha gari kwenye maegesho, kisha wakaenda kula chakula cha mchana.

> **"Kanuni ya tisa inatoa msamaha kwa baadhi ya vifungashio vya plastiki kwa ajili ya huduma za afya au ambavyo vinatumika kwenye kufungashia bidhaa za viwandani au sekta ya ujenzi au sekta ya kilimo au vyakula au usafi na udhibiti wa taka," imeelezwa katika taarifa hiyo.**

Hapo kulizuka zogo kidogo, abiria wakiwa wamekerwa na kile kitendo hicho, wapo waliowaonya kwa lugha na ushauri, kwamba wajitahidi kuwa makini na usafi wa gari lao, kwa kuwa ndiyo ofisi yao.

Ni tukio ambalo si mara ya kwanza kulishuhudia. Ilikuwa mara ya pili kushuhudia chupa ya mkojo ndani ya daladala, katika jiji hilo.

Ilikuwa daladala inayofanya safari, wakati huo ikitoka Tandika kwenda Mbezi. Binafsi nilikaa kiti cha mbele, nikavuta gazeti lililokuwa jirani, nilipojaribu kulivuta kwa nia ya kulisoma, nikakutana na chupa ya plastiki iliyojaa mkojo.

Hayo ni ya usafiri jijini. Katika upande wa safari ndefu, kuna wakati katika safari ya basi kutoka Dar es Salaam, kwenda Mwanza, basi hilo mali ya kampuni moja kubwa ya usafiri katika njia hiyo halikujaa sana.

Ilinishangaza abiria aliyehama kiti chake na kuja nyuma ambako kiti jirani hapakuwapo mtu. Alitoa mfuko wake wa keki 12, ambazo maarufu zinauzwa bei ya Shilingi 100 kila moja, akazila zote na kutupa ndani ya basi taka zote za vifungashio, zitokanazo na chakula chake.

Nilipomhoji kulikoni anatupa chini, ilhali kuna pa kutupia, akijibu "kondakta yupo atazoa." Naam! Ndio picha ya ustaarabu mwingine ndani ya magari.

Ni kawaida, abiria wa safari ndefu na fupi, wapo abiria wanaotupa ovyo taka kama vibunzi vya mahindi, vifungashio vya karanga, korosho na biskuti na maganda ya chungwa na miwa.


Vyombo vya kuhifadhi taka vilivyopo kwenye daladala hizo vingi vimewekwa kama pambo au kukwepa kuchukuliwa hatua na mamlaka husika, lakini ukweli ni kwamba havitumiki inavyotakiwa.

Changamoto ya kukosekana vyoo katika baadhi ya maeneo yanayotumiwa na wafanyabiashara ndogo ndogo, malipo makubwa kwa matumizi ya vyoo hivyo nayo huchangia kwa kiasi kikubwa uchafunzi wa mazingira.

Maeneo ya biashara nako hayako salama. Kuna matukio mengi ya wafanyabiashara na hasa wanaume, wameendeleza tabia ya kujisaidia haja ndogo kwenye chupa, kisha wanazificha kwa namna wanavyoweza.

Mfano hai ni katika Kituo cha Mabasi cha Mbezi, jijini Dar es Salaam, katika Barabara ya Morogoro, ambako kuna huduma ya vyoo, shilingi 500 kwa haja

**Inaendelea Uk. 15**



Taka za

MAZINGIRA

# Mapambano ya mifuko plastiki yameanza, daladala, mitaani bado mtihani mkubwa

Inatoka Uk. 14

zote kwa mujibu wa matangazo yaliyobandikwa, ikidaiwa ni bei kubwa.

Wakazi jirani wanasema, imechangia baadhi ya abiria au wafanyabiashara kuamua kujisaidia katika maeneo yasiyostahili na kusababisha harufu mbaya ya mkojo na mazingira yasiyovutia.

"Mtu mwingine anaweza kuona gharama hiyo ni ndogo, lakini kwa mfanyabiashara ndogo ukiwa mnywaji mzuri wa maji, unaweza kujisaidia haja ndogo hata mara nne kwa kutwa, kwa hiyo hapo unazungumzia kutumia jumla ya shilingi 2,000 kwenda chooni tu bado kula na nauli," anasema Maimuna Salum mmoja wa wafanyabiashara hao.

**HATARI KIPINDUPINDU**


Taarifa za hivi karibuni ziko wazi kwamba kuna wagonjwa sita walifariki dunia na wengine 361 wamethibitika kuugua ugonjwa wa kipindupindu, ikitajwa kiko Tanga na Dar es Salaam.

Ni sehemu ya tamko la Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, katika taarifa yake kuhusu magonjwa ya kipindupindu, dengue na ebola.

Licha ya kuzuka kipindupindu katika baadhi ya maeneo kila mwaka jijini hapa, bado kuna mazingira yanayoonekana kutowashtua baadhi ya wakazi, kutokana na mwenendo na tabia zao.

Utiririshaji maji machafu yenye kinyesi cha binadamu katika maeneo kadhaa, umekuwa ukifanywa kutoka kwenye vyoo, hasa vilivyopo jirani na mifereji au mito.

Matunzo ya mazingira kimsingi, ni jukumu la watu wote, wakiwamo watoto hasa ambao tayari wana umri wa kwenda shule na waliopo shuleni, kwa ujumla. Serikali kupiga marufuku mifuko hiyo, iliungana na





Wakazi wa Mbezi Mwisho, Dar es Salaam, wakishiriki Siku ya Usafi Duniani, kwa kusafisha mazingira yao.

nchi nyingine zaidi ya 60 duniani, zikiwamo majirani wa Kenya na Rwanda, pia ughaibuni; China, Italia na Ufaransa.

Ni hatua iliyoungwa mkono na wananchi kadhaa na wadau wa mazingira, kupitia vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii. Baadhi waliandika ujumbe wa kuipongeza serikali.

Mnamo Juni 14 mwaka huu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ilitoa taarifa kwa wananchi ikiwajuza kuhusu Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki za Mwaka 2019, kuwa imeanza kutekelezwa kuanzia tarehe Mosi Juni 2019.

Ilitumia nafasi hiyo kutoa onyo kwa baadhi ya wazalishaji na wasambazaji waliobadilisha mifuko laini ya plastiki isiyokuwa na mishikio na kuitumia kama vibebeo vya bidhaa.

"Kanuni ya tisa inatoa msamaha kwa baadhi ya vifungashio vya plastiki kwa ajili ya huduma za afya au ambavyo vinatumika kwenye kufungashia bidhaa za viwandani au sekta ya ujenzi au sekta ya kilimo au vyakula au usafi na udhibiti wa taka," imeelezwa katika taarifa hiyo.

> **"Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ina utahadharisha umma kuwa ni makosa kisheria kubadili matumizi ya vifungashio hivyo kuwa mifuko ya kubebea bidhaa," imeelezwa.**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limetajwa kuwa linaandaa viwango vya vifungashio, ambavyo vitaainisha kiwango cha unene na uwekwaji wa lakiri na kutambulisha bidhaa iliyofungashwa kabla ya kuuzwa.

"Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ina utahadharisha umma kuwa ni makosa kisheria kubadili matumizi ya vifungashio hivyo kuwa mifuko ya kubebea bidhaa," imeelezwa.

Pia, kuna adhabu stahiki zitakazotolewa kwa watengenezaji, waingizaji, wasambazaji na watumiaji wa vifungashio vya plastiki vilivyozalishwa ama kuingizwa nchini na kutumika kama vibebeo vya bidhaa.

Katika eneo hilo la vifungashio kwenye maeneo ya biashara, kumekuwapo changamoto kwa baadhi ya wafanyabiashara hasa wa nguo, ambao badala ya kuvitupa pipani, wanaviacha vikisambaa ovyo kusababisha mazingira ya maeneo husika kuonekana machafu.

Kabla ya serikali kupiga marufuku mifuko hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda, alishawahi weka utaratibu wa kuhakikisha asubuhi ya siku ya Jumamosi inatumika kwa ajili ya usafi katika maeneo mbalimbali ya makazi na biashara.

Ni mtazamo wote unaoangukia katika dhana ya kuweka jiji katika mazingira ya usafi na kuwa mbali na magonjwa.




plastiki zilivyosambaa. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

AFYA

# Picha kamili maradhi ya kisukari, mgonjwa anavyojinasua hatarini

## Hizi hapa mbinu salama zinazofaa kutumika




**Na Lucy Johnbosco**

KISUKARI ni nini? Madaktari na wataalamu wa afya, wanaieleza kuwa ni maradhi yatokanayo na mtu kuwa na kiwango cha juu cha sukari kilichoko kwenye damu.

Inaelezwa, kiwango cha sukari kwa kawaida iwe katika wastani wa kipimo cha kiafya: 4-8 na endapo kongosho likashindwa kuzalisha kichocheo kiitwacho insulin, kwa kawaida kinasababisha ugonjwa wa kisukari.

Insulin ni aina ya kichocheo chenye kazi ya kuyeyusha sukari inayoingia mwilini na kupelekwa katika damu na inapotokea kichocheo hicho kikakosekana katika mwili, ndipo inakuwa mwanzo wa tatizo, kwa maana ya kila sukari inayoingia mwilini inapelekwa kwenye damu pasipo kuyeyushwa. Hapo ndipo ugonjwa wa kisukari unaanza.

**AINA ZAKE**

Ni vyema kufahamu, kuna aina ngapi ya ugonjwa huu wa kisukari? Ni vitu gani vinavyoweza kusababisha kongosho kushindwa kuzalisha kichocheo kinachoitwa insulin?

Katika kutafsiri maradhi hayo ya kisukari, yana sura za aina tatu: Aina ya kwanza au 'Type One Diabetes' ni ile ambayo huwapata zaidi watoto wadogo wenye umri wa kati hadi kufikia utu wa ujana wa miaka 25.

> **Ndani ya aina hiyo ya kisukari, tiba yake kuu ni matumizi ya vidonge na kubadili mfumo wa maisha, hasa katika ulaji na kufanya mazoezi.**

Mtoto anapozaliwa na ulemavu katika kongosho, linaloshindwa kuzalisha kichocheo cha insulin, matibabu au tiba ya aina hiyo zaidi ni kwa njia ya sindano za insulin.

Kitaalamu, maana yake ni kwamba, mgonjwa mwenye aina hiyo ya kisukari huwa anapaswa kutumia sindano hizo katika maisha yake yote. Kazi ya sindano hizo, ni kusaidia kuyeyusha sukari na kushusha kiwango cha sukari kilichoko katika damu yaa mhusika.

Aina ya pili ya kisukari au 'Type Two Diabetes', inawapata watu wazima kuanzia umri wa kati wa miaka 25 mpaka uzee. Hiyo ni ya kurithi, kutoka mtiririko wa kifamilia, hasa watangulizi wana historia ya ugonjwa wa kisukari.

Hiyo inajenga tafsiri ya kuwapo uwezekano mkubwa kwa wanafamilia, kwa maana ya watoto kupata kisukari.

Pia, ulevi wa pombe na sigara kupita kiasi, nayo inatajwa kuleta kisukari aina ya pili; unene wa kupitiliza, umri na mfumo wa maisha, vyote vinachangia uwezekano wa mmoja kupata aina hiyo ya kisukari.

Ndani ya aina hiyo ya kisukari, tiba yake kuu ni matumizi ya vidonge na kubadili mfumo wa maisha, hasa katika ulaji na kufanya mazoezi.

Pia, kuna aina ya tatu ya kisukari, ambayo huwapata kinamama wajawazito. Tiba yake ni sindano za insulin na dalili zake zinafanana na alivyo mgonjwa mwenye unene uliopitiliza (kisukari aina ya tatu).



Baadhi ya vyakula vinavyoshauriwa kulinda mwili dhidi ya maradhi ya kisukari.

Mara zote, msongo wa mawazo, kukosa muda wa kupumzika, ulevi wa pombe, uvutaji sigara uliopitiliza kiasi, kutofanya mazoezi ya viungo na mwili kwa ujumla, vyote vinasababisha kongosho kushindwa kuzalisha kichocheo cha insulin na kuleta kisukari.

**VYANZO VYA KEMIKALI**

Pia, kuna sababu za kikemikali na baiolojia, nazo ziko katika mlolongo wa vyanzo vya kisukari. Hapo kuna suala la matumizi ya dawa pasipo ushauri wa kidaktari.

Inaelezwa, baadhi ya dawa za binadamu zina athari katika kongosho la mwanadamu na kuchangia ishindwe kuzalisha insulin, huku ikiwa ni chanzo cha sumu katika chakula ua kitaalamu 'food poison.'



Kilniki ya kisukari ikiendelea katika hospitali kuadhimisha Siku ya Kisukari Duniani.

Sababu za kibaiolojia zinaangukia katika kurithi na ujauzito. Kipindi mwanamama ni mjamzito, mwili wake hutengeneza kichocheo ambavyo vinakwamisha ufanyaji kazi wa kichocheo cha insulin.

Hapo humfanya mama mjamzito kupata ugonjwa wa kisukari. Aina hiyo kitaalamu inajulikana 'Gestational Diabetes' au kisukari cha kipindi cha ujauzito.

Dalili zake, huwa zinafanana, ingawaje sio rahisi kujua au kutambua dalili hizo. Kwa nini? Kwanza ni ngumu kuzigundua, pili hazijioneshi mapema na ndio maana inashauriwa mtu kupima kisukari walau mara mbili kila mwaka.

Dalili hizo hujitokeza kwa viashiria, mtu anapata kiu na njaa ya kila mara, anakonda, anapata haja ndogo (mkojo) kila mara na hasa wakati wa usiku, anapoteza kumbukumbu kila mara, macho kupoteza uwezo wake wa kuona au kuwa na uoni hafifu.

Vingine mtu ana vidonda hasa miguuni na anachelewa kupona, huku akisumbuliwa na maumivu ya kichwa kila mara.

Kwa wanaume wanakosa au kupungukiwa nguvu za kiume na wanawake wanaharibikiwa mimba kila mara, wanakosa hamu ya tendo la ndoa, wanakuwa na maambukizi ya fangasi katika sehemu za siri na kupata maambukizi ya UTI sugu.

**ATHARI ZINGINE**

Ugonjwa wa kisukari, mbali na athari za kiafya, pia zina athari mbalimbali katika sura ya uchumi binafsi kwa mgonjwa na katika sura pana, inagusa maendeleo ya Taifa.

Kitaalamu imethibitika kwamba, endapo mgonjwa hajajua jinsi ya kudhibiti ugonjwa wa kisukari, ni rahisi kwake kupata madhara kama ya ulemavu, upofu, figo, moyo na shinikizo la damu.



Mtu akipimwa kisukari.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Maeneo mengine ya athari hizo, ni katika mishipa ya fahamu na damu, upungufu wa nguvu za kiume, kuharibikia mimba, matatizo la viungo na misuli.

Katika sura pana ya kitaifa, pale ulemavu unapotokea, mgonjwa hataweza kuendelea kufanya kazi au utendaji wake ukawa duni. Hapo ina maana, inasababisha kupungua nguvu kazi za uzalishaji.

Pia, katika sura nyingine ndani ya uchumi ni hasa kupitia matibabu na dawa, inaelezwa gharama za mahitaji ya dawa na sindano za insulin na mahudhurio ya kliniki, mzigo unaobebwa na serikali na hasa katika hospitali za umma, ni mkubwa sana, kwani sehemu kubwa ya huduma kwa umma inatolewa bure.

> **Dalili hizo hujitokeza kwa viashiria, mtu anapata kiu na njaa ya kila mara, anakonda, anapata haja ndogo (mkojo) kila mara na hasa wakati wa usiku, anapoteza kumbukumbu kila mara, macho kupoteza uwezo wake wa kuona au kuwa na uoni hafifu.**

Kutokana na hilo, kuna mambo manne muhimu anayoshauriwa mgonjwa wa kisukari kuyazingatia, ili imsaidiee kuishi vizuri, ilhali anaumwa ugonjwa huo.

Mosi, anapaswa kujifunza yote yanayohusu kisukari; dalili zake na nini cha kufanya iwapo anakuwa amezidiwa.

Pili, kukubali hali ya kuishi na ugonjwa huo, kwa sababu si wa kupona; suala la tatu, anatakiwa kujifunza namna ya kuishi na ugonjwa huo.

Jambo la nne, ni kwamba anayeumwa kisukari anatakiwa kuwa msikivu katika kufuata ushauri na maelekezo ya daktari, pia mshauri wa lishe. Endapo mgonjwa atayafuata hayo, anajinasua kutoka katika afya hatari.

# Wanafunzi wafuatwa waliko kupewa darasa la kisukari

IMEBAINIKA kuwapo imani potofu nchini inayowafanya watu wabweteke kuhusiana na kusambaa kisukari kitaifa, kwamba zaidi inawapata wenye umri unaozidi miaka 30.

Ni jambo linalotajwa kujenga maana kwa jamii, wasione umuhimu wa kuwachunguza watoto walioathirika na maradhi hayo.

Chama cha Ugonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA), hivi sasa kinaonya kwamba, hiyo ni imani potofu kwa sababu inawezekana watoto wengi walio na kisukari, wasigundulike kupoteza maisha.

Pia, chama hicho kinaeleza inakuwa nafasi nzuri kuelimisha kuhusu ugonjwa huo na inapaswa kubadilika kwa kuwa uchunguzi kwa watoto kuhusiana na ugonjwa huo, ni jambo muhimu kwa maendeleo endelevu kimaisha. Ili kuingiza 'mkono' wake kuondokana na mawazo hayo potofu, TDA imekuwa katika mpango maalumu wa kupima kisukari na kuelimisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa kufanyiwa uchunguzi.



Wanafunzi wakielimishwa wanayopaswa kujua kuhusu ugonjwa wa kisukari. **PICHA: MTANDAO.**

Mtazamo wa chama hicho ni kwamba, hilo litawasaidia katika kujenga uelewa sahihi kuhusu ugonjwa huo, sambamba na mengine yasiyo ya kuambukiza, ambayo chanzo chake ni mtindo mbaya wa maisha.

Elimu hiyo ilitolewa katika shule za sekondari za wasichana za Kisutu na Jangwani za jijini Dar e Salaam, ikiwa ni sehemu ya TDA kuelimisha umma programu zake kuelekea Siku ya Ugonjwa wa Kisukari Duniani, inayoadhimishwa kila mwaka Novemba 14.

Mratibu wa Shirikisho la Vyama Vinavyopambana na Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza (TANCDA) mkoa wa Dar es Salaam, Happy Nchimbi, anasema mkakati wa mwaka jana ulilenga kuiwezesha jamii kuwa na uelewa wa kutosha, kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza, hususani kisukari.

"Kasi ya watu kuugua magonjwa yasiyo ya kuambukiza imeongezeka kwa kiwango kikubwa katika miaka ya karibuni na hali inaonyesha kuwa kwa sasa yanasababisha vifo vingi kuliko magonjwa ya kuambukiza," anasema Nchimbi.

Anayataja magonjwa mengine yasiyo ya kuambukiza, mbali na kusukari ni shinikizo la damu, maradhi ya moyo, selimundu, kiharusi, pumu na matatizo ya kinywa.

Nchimbi alieleza dhamira ya uelimishaji kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Hapo anagusia umma kubadili tabia za ulaji vyakula vyenye mafuta mengi, sukari na wanga.

Meneja Mradi wa Ugonjwa wa Kisukari kwa Watoto, Hariet Mganga, anasema tatizo la kisukari kwa watoto nchini kwa sasa ni kubwa na linahitaji mikakati ya kudumu, katika kukabiliana nalo.

Anatoa mfano kuwa katika kliniki 34 za kisukari walizozisajili nchini, wanawahudumia watoto 2,488 wenye ugonjwa huo na mtoto anapogundulika kuugua kisukari, inakuwa rahisi kukidhibiti.

* Makala hii imetolewa katika tovuti, ikitambulishwa imeandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanaopambana na Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza Tanzania (TJNCDF) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza (TANCDA)

MAZINGIRA

# Walinda misitu wilaya 16 waingia 'darasa tosha' la misitu na mkaa

## Kila mmoja aaga na ahadi kuendeleza kwake

**Na Christina Haule, Morogoro**



Mkaa uliozalishwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

SERIKALI imeombwa kuandaa mwongozo utakaoelekeza halmashauri nchini kuandaa bajeti kwa ajili ya usimamizi misitu ya vijiji kuwa endelevu.

Maofisa wa Misitu, Maliasili, Ardhi, Kilimo, Maendeleo ya Jamii kutoka wilaya 16 nchini, wanasema, hiyo ni kufanya mifumo mbalimbali iliyo thabiti ya kuhifadhi misitu kutumika vyema, ikiwamo Mfumo wa Mradi wa kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS).

Ni ombi lao, baada ya kumaliza ziara ya siku tatu iliyoandaliwa na Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS) maarufu 'Mkaa Endelevu' iliyofanyika katika vijiji vya Matuli na Mlilingwa mkoani Morogoro.

Mmoja wa maofisa hao, ambaye ni Ofisa Ardhi na Maliasili wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Damas Mumwi, anasema iwapo kutakuwapo maagizo kutoka juu kuhusu uwekezaji wa misitu, ni dhahiri itakuwa endelevu.

Anasema, hilo litafanya misitu ya vijiji na maliasili kuangaliwa na halmashauri pekee na kuna uwezekano ikamalizika na kuishia isiwe endelevu.

"Tumeona maendeleo yaliyopatikana kupitia usimamizi wa shirikishi wa misitu (USM) kwenye vijiji," anasema na kuongeza:

"Nashauri kama serikali kupitia wizara husika, kuona inatoa mwongozo kwa halmashauri kutenga bajeti ya USM, kama ilivyofanya kwa vijana, kinamama na wenye ulemavu, ili shughuli za uhifadhi ziendelee kuwa bora Tanzania nzima," anasema.

Ofisa huyo anaitaja misitu kuwa ni rasilimali muhimu katika kuchochea maendeleo, ila kinachokosekana ni uwekezaji kama TTCS ilivyofanya Morogoro.

Mwingine anayeunga mkono mada hiyo ni Kaimu Ofisa Ardhi na Maliasili wa Wilaya ya Mvomero, Sadoyeka Kyaruzi, anayesema uwekezaji katika sekta hiyo, utaisaidia serikali kutatua changamoto zinazowakuta wanavijiji.

Kyaruzi anasema, katika wilaya yao kuna vijiji vitano vilivyopo kwenye mradi, ambako kumekuwa na mabadililo makubwa ya kiuchumi, kijamii na maendeleo.

"Naomba kusisitiza, bila kuwapo kwa maelekezo kutoka juu kuhusu utengaji wa bajeti kwa ajili ya USM, ni vigumu kupata matokeo chanya kwenye sekta hii," anasema.

Ofisa Misitu Wilaya ya Tunduru, Paul Onesmo, anaahidi kubeba elimu mahali hapo kwenye ziara na kufikisha wilayani kwake, ili kuhakikisha mradi kama huo wa mkaa endelevu, unatekelezwe na wananchi wake.

Onesmo anasema, iwapo watafanya maamuzi, watakuwa na uelewa kuhusu USM, ni dhahiri kuwa misitu itakuwa salama na kuchangia maendeleo.

> **"Nashauri kama serikali kupitia wizara husika, kuona inatoa mwongozo kwa halmashauri kutenga bajeti ya USM, kama ilivyofanya kwa vijana, kinamama na wenye ulemavu, ili shughuli za uhifadhi ziendelee kuwa bora Tanzania nzima," anasema.**

Solomon Benjamin, Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili Ruangwa, anasema wilayani kwao wameshaanza kunufaika na rasilimali misitu, hivyo anaamini ni wakati muafaka wa kusambaza elimu ya mkaa endelevu, kwa kushawishi utengaji bajeti katika usimamizi wa misitu.

Ofisa Misitu Msaidizi Wilaya ya Songea, Hadija Bakari, anasema ziara hiyo imeonyesha matokeo chanya kwake, hivyo atatumia kila njia kushawishi halmashauri kutenga bajeti katika USM itakayosaidia kuboresha misitu na pengine kutumia mfumo wa mkaa endelevu kama sehemu ya uhifadhi.

Bakari anasema, pamoja na ushawishi huo anatarajia kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa misitu kwa dhana ya endelevu.

Gravas Mwalyonbo, ni Ofisa Misitu wa Wilaya ya Namtumbo, anasema ni mradi unaopaswa kusambazwa katika wilaya zote zenye misitu ya vijiji, kwani unapunguza uvunaji haramu wa rasilimali misitu na maliasili.

Anasema halmashauri zinapaswa kuweka kipaumbele katika sekta ya misitu na maliasili kama ilivyo kwa elimu, afya, miundombinu na kilimo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Morogoro, Florence Mwambene, anasema mradi huo umesaidia kuondoa changamoto nyingi katika vijiji vilivyo kwenye mradi wilayani humo.

Kwa mujibu wa Mwambene, katika vijiji vya Mlilingwa, Matuli, Diguzi na Tununguo wameboresha maisha yao kupitia mradi wa uhifadhi ukiimarika zaidi.

**KIONGOZI TFS**

Meneja Misitu Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Benadetta Kadala, anasema kiujumla mradi umeonyesha matokeo chanya ila kinachohitajika ni kuwepo kwa mipango endelevu baada ya mradi kuisha.

Ofisa Misitu Mkuu Idara ya Misitu na Nyuki, Wizara ya Maliasili na Utalii, Seleboni John, anasema yeye kama mtaalamu wa misitu ameona manufaa na kuahidi kufikisha kwa wakubwa zake kuangalia namna ya kusambaza mradi huo.

John amewataka maofisa hao kuandaa taarifa sahihi kuhusu walichojifunza ili wakurugenzi na wafanya maamuzi katika ngazi zao waweze kusukuma mbele zaidi.

Mkurugenzi Msaidizi wa TFCG, Emmanuel Lyimo, anasema msingi mkubwa waliotumia kutekeleza mradi huo ni ushirikiano, hivyo kuwaomba maofisa hao waliopata kujifunza kutumia njia hiyo kabla ya kuingia katika utekelezaji.

TTCS ni mradi unaotekelezwa katika vijiji 30 vya wilaya za Kilosa, Mvomero na Morogoro chini ya usimamizi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (Mjumita), Shirika la Kuendeleza Nishati Asili (TaTEDO) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswis (SDC).



Mmoja wa wachoma mkaa katika kijiji cha Msimba Wilaya ya Kilosa, akionyesha matanuri ya asili ya kuchoma mkaa yanavyofanya kazi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA




Wanafunzi wakishiriki kampeni ya kupinga ukatili kwa watoto. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Ijue kampeni '155' inayopambana na adui wa ngono, wabakaji watoto

- Afande Nzuki: Hiyo sindano nzuri kuwachoma
- Kila wasichana 3, mmoja amekatiliwa kijinsia

**Na George Mapunjo**

KAMPENI mbalimbali duniani zinaelezwa kuwa ni njia pekee na rahisi ya kuwawezesha watu kuungana kwa sauti moja kutetea haki na maslahi yao.

Pia, kupitia kampeni hizo zinazoanzishwa, zinakuwa na malengo na madhumuni yake, ikiwamo kusaidia, kuinua na kuendeleza jambo fulani.

Umoja wa Mataifa katika kutimiza majukumu yake, unadhamiria kutekeleza malengo kadhaa, la kwanza ikisisitiza kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2030.

Hivyo, katika mustakabali wa kukabili dhana hiyo, ni vigumu kuuondoa umaskini, iwapo kuna kundi maalumu bado liko katika ngazi ya chini kujikwamua kwa mengi. Vivyo hivyo, katika mustakabali huo nchini, Dira ya Maendeleo ya Taifa Tanzania 2025, inalenga kuwa na Taifa lenye uchumi wa kati.

Katika kujipanga kuelekea katika hatua hiyo, kuna msisitizo mahsusi kwa watu kuanzisha kampeni tofauti za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa, ili kusaidia kuwezesha huduma za kiafya na mahitaji mengineyo ya lazima kama maji, umeme, barabara na ajira.

**TGNP na 155**

Kampeni ya 155; ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili wa kingono inayoratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP, ilizinduliwa rasmi Februari 27, mwaka huu katika viwanja wa TGNP Mtandao, Mabibo, jijini Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo, mgeni rasmi alikuwa, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Mary Nzuki, ambaye ni Mkuu wa Dawati la Jinsia katika jeshi hilo.

Ni kampeni inayojikita katika uelimishaji jamii na kuwalinda watoto, ambao hawawezi kujilinda dhidi ya matendo ya ukatili wa kijinsia.

Kwa kurejea malengo yake, ni kampeni inayodhimiria kuelimisha jamii iliyoko katika mazingira hatarishi, dhidi ya vitendo vya kingono inayohusisha watoto kubakwa na kulawitiwa, mambo yanayowaharibia mwelekeo wa baadaye kimaisha, kutokana na ukatili huo.

Mkurugenzi Mkuu wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, anasema malengo ya kampeni ni kuibua mjadala katika jamii kuhusu hali halisi ya kingono, athari zake na umuhimu wa kuwalinda watoto na kuihamasisha jamii kubainisha viashiria vya ukatili wa kingono kwa watoto.

Anasema, hiyo inaweza kufanyika kwa watoto kutoa taarifa mapema, itakayosaidia kuzuia tabia na kujenga nguvu za pamoja na wadau wote katika kuweka mkakati wa pamoja wa ulinzi wa watoto, dhidi ya aina hiyo ya ukatili na kuhakikisha kila mmoja anakuwa mdau wa kampeni hiyo.

Lilian ambaye asasi yake ni mdau mkuu katika vita hivyo, anasema kampeni itasaidia kuokoa maisha ya Watanzania wanaokabiliwa na vitisho vya ukatili wa kijinsia, pia kufahamiana na wanaharakati wengine wenye ajenda zinazofanana.

Kupitia hiyo, anasema TGNP itaongeza mtandao wa uhusiano wenye tija na watu mbalimbali, kuishawishi jamii iondokane na tabia ya ukatili kwa watoto katika maeneo husika na kuwashirikisha katika shughuli za TGNP Mtandao.

Vivyo hivyo, anataja azma ya kuwa na mustakabali mpana wa kutembelea maeneo yenye changamoto zinazoweza kuleta madhara kwa watoto.

Kwa mujibu wa Lilian, hiyo ni kampeni isiyo na mwisho, inayolenga hatua ya jamii kufikia kutambua umuhimu wa kuheshimu haki ya mtu mwingine.

Mkurugenzi anasema, waliamua kuipa jina la '155' kwa sababu taarifa yoyote chanzo chake inatokana na mtu mmoja. Hivyo, kupitia mtu huyo taarifa inawafikia wengi.

Anafafanua kwamba, mchakato wa kufahamiana huko, taarifa inaanzia katika ngazi ya mtu mmoja na kisha inatanuka hadi kuwafikia watu watano na ndipo kunakuwapo mwendelezo wa ngazi hiyo ya watu watano zaidi, ikizidi kujiongeza kwa mtiririko huo. Hapo ndipo ilipozaa msamiati '155.'

"Tuliona ni njia rahisi kuwafikia watu wengi kutokana na ukatili kufanyika kwenye jamii hizi tunazoishi nazo na wahusika wanaweza kuwa watu wa karibu na mwathirika," anasema.

> "Tuliona ni njia rahisi kuwafikia watu wengi kutokana na ukatili kufanyika kwenye jamii hizi tunazoishi nazo na wahusika wanaweza kuwa watu wa karibu na mwathirika," anasema.

**AFANDE NZUKI**

Ni uzinduzi uliowashirikisha wanafunzi na wazazi, ili kujenga ukaribu kati ya TGNP Mtandao na wanajamii.

Mgeni rasmi, DCP Mary, aliipongeza TGNP Mtandao kwa kubuni kampeni ya aina hiyo, kwani ni njia bora ya kuwafikia watu wengi na kutoa elimu sahihi kwa jamii.

Anasema, ukatili wa kijinsia kwa watoto unazidi kuongezeka na kuleta madhara mengi ya kifamilia na taifa kwa ujumla.

Ombi lake ni kuwapo kampeni endelevu, akiwa na imani kwamba itakuwa anachokiita 'sindano tosha' ya 'kuwachoma' wote wanaoleta madhara ya ukatili kwa watoto.

Mkuu huyo mwenye dhamana na haki za kijinsia, anasema, dawati lake liko wazi kupokea malalamiko yanayohusu ukatili wa kijinsia wa aina hiyo.

Anasema, hadi sasa kuna wastani wa msichana mmoja kati ya watatu nchini, waliofanyiwa ukatili huo na wengine wanapata mimba wangali katika umri wa chini ya miaka 18.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2001, inatambua haki za msingi za binadamu kama zinavyotambuliwa duniani, huku kukiwapo vifungu vinavyoainisha zuio la ukatili kama kuteswa na jamii kuvunjiwa heshima.



DCP Mary Nzuki, akizungumza.

AFYA




Baadhi ya wadau wa lishe bora wakiandamana.

# TFDA inavyopigana kumnusuru mlaji kutoka chakula chenye hatari ya sumu

- Kila mwaka kinachukua uhai wa watu 420,000
- Tatizo kuu limejificha katika uelewa duni

**Na Yasmine Protace, Bagamoyo**



Sehemu ya vyakula vinavyochangia lishe bora. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

CHAKULA ni uhai na ili uhai huo ukamilike, ni sharti kinacholiwa kiwe salama, hasa kiafya. Ni hitaji lilili bayana na halipingiki, kuwa chakula ni hitaji muhimu kwa maisha ya binadamu.

Ustawi katika maeneo ya nchi una umuhimu huo unaosababisha suala la usalama wa chakula kupewa kipaumbele katika kulinda afya ya jamii, kuwezesha uhakika wa chakula na lishe.

Hicho ni kigezo muhimu katika uchumi na na biashara ya chakula kitaifa na kimataifa.

Hivi karibuni, katika mafunzo ya siku mbili yaliyotolewa kwa wanahabari na Mamlaka ya Chakula na Dawa( TFDA), Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Adam Fimbo, anasema kuwa chakula salama ni nyenzo muhimu katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Milenia, akitaja lengo namba moja, mbili na tatu.

Kwa mujibu wa Fimbo, ni malengo yanayojiekeleza katika kuondoa umaskini, kutokomeza njaa na kulinda afya ya jamii na ustawi wake.

Anasema, pamoja na umuhimu huo, bado chakula kisipokuwa salama, kinaweza kusababisha madhara ya kiafya, kama vile magonjwa na hata vifo, endapo mgonjwa hatapata matibabu sahihi.

"Ni vyema sisi sote tukatambua kwamba chakula salama ni kile ambacho kinaweza kuleta madhara kwa mlaji, hasa uchafu wa chakula," anasema.

Fimbo anasema, maradhi mengi yatokanayo na chakula kisicho salama, yanachangiwa na kiasi kikubwa cha uelewa mdogo wa jamii, kuhusiana na masuala ya usalama wa chakula .

Anafafanua kuwa, takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kuwa takribani watu milioni 600 duniani, sawa na mtu mmoja kati ya watu 10 huugua kila mwaka kutokana na kula chakula kisicho salama.

"Kati yao 420,000 hufariki na kati yao 125,000 ni watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano," anasema, akirejea ni kiwango cha nchii. Bosi huyo wa TFDA anaongeza kuwa, tatizo hilo ni kubwa zaidi barani Afrika kwa zaidi ya watu milioni 91, wanakadiriwa kuugua na kati yao 137,000 hufariki kila mwaka, kutokana na kula chakula kisicho salama.

Anasema, ni hali inayoonyesha kuwa, kuwapo tatizo kubwa la uchafuzi wa chakula, inayotokana na kutozingatia kanuni bora za usafi, kilimo, ufugaji, usindikaji, uandaaji na usambazaji katika hatua mbalimbali za mnyororo wa chakula. Anashuri kwamba pamoja na athari za kiafya, ni vyema jamii ikafahamu kuwa magonjwa yatokanayo na chakula yanazorotesha shughuli mbalimbali za uzalishaji mali, huku zikiongeza gharama za matibabu na kudhoofisha uchumi katika ngazi zote.

"Hivyo udhibiti wa magonjwa hayo ni jambo linalopaswa kupewa kipaumbele, ili kulinda afya ya jamii na kukuza uchumi," anasema.

Fimbo anasema kuwa maradhi mengi yatokanayo na chakula kisicho salama, huchangiwa kwa kiasi kikubwa na uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya usalama wa chakula, hivyo inashia jamii kutozingatia ipasavyo kanuni za upatikanaji salama.

Anaongeza kuwa baadhi ya mifano ya uelewa mdogo wa masuala ya usalama wa chakula miongoni mwa jamii ni kama vile kuandaa chakula katika mazingira yasiyo safi.

Fimbo anasema, kazi ya kudhibiti usalama wa chakula nchini ni mojawapo ya jukumu la kisheria na la msingi la TFDA, kwa kutambua na kuzingatia umuhimu wa usalama wa chakula katika kulinda afya ya jamii.

**TFDA inavyopigana**

Anaongeza kuwa, TFDA imeweka mfumo thabiti wa kudhibiti na kuhakikisha chakula kutoka kinachozalishwa ndani ya nchi na kinachoingizwa, vyote vinakidhi vigezo vya usalama na ubora kwa walaji wasidhurike kiafya.

Hadi sasa baadhi ya majukumu yanayotekelezwa na TFDA katika kuhakikisha usalama wa chakula nchini, ni kufanya tathmini na usajili wa vyakula vilivyofungashwa.

"Kusajili maeneo na kutoa vibali vya biashara ya chakula, kufanya ukaguzi wa chakula katika soko pamoja na ukaguzi wa maeneo ya kusindika, kuhifadhia na kuuzwa chakula," anasema.

Anaongeza kuwa, pia wanadhibiti uingizaji nchini na usafirishaji wa vyakula nje ya nchi, wanafanya uchunguzi wa sampuri katika maabara, kudhibiti matangazo ya biashara ya chakula, kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kuhakikisha usalama wa chakula.

Fimbo anaendelea kuwa, katika ngazi ya kimataifa ambako kuna Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kupitia kikao chake kilichofanyika Desemba 28 mwaka jana, kilipitisha azimio la kuadhimisha Siku ya Usalama wa Chakula Duniani, ifikapo Juni 7.

Anasema lengo ni kuikumbusha jamii kuhusu usalama wa chakula na wadau mbalimbali, pamoja na walaji, wafugaji, wakulima, wasindikaji na wafanyabiashara.

Lengo la mwisho analolitaja ni kuhakikisha usalama wa chakula katika mnyororo wa thamani kuanzia mazao ya chakula yakiwa shambani, hadi chakula hicho kinapomfikia mlaji.

## ...Afya ya binadamu imesimamia hapa

NI rahisi kutamka neno afya. Ni neno linalojenga dhana ya hali ya ukamilifu kimwili, kiakili na kijamii.

Kuwa na afya bora huchukuliwa ni nguzo na raslimali muhimu katika kuchangia maendeleo ya mtu binafsi, familia na nchi, hususan katika kuleta maisha bora na kupunguza umaskini.

Kwa mantiki hiyo, afya bora inalenga kuwa na ustawi endelevu kwa jamii, kwa kuzingatia mchango wa mtu binafsi kulingana na nafasi yake, uwezo na fursa zilizopo katika kuleta maisha bora.

Upatikanaji afya bora, unahitaji uwezeshaji wa jamii yenyewe iwe na uwezo wa kushiriki, kuamua, kupanga na kutekeleza mikakati yao ya kuwaletea maendeleo katika ngazi mbalimbali.

Ili kuwa na afya bora, ni vizuri kujiuliza maswali kadhaa yanayojenga msingi imara wa afya ya mtu binafsi au jamii.

Maswali hayo ni pamoja na unakula nini? Na kwa kiasi gani? Unakula aina gani ya vyakula? Unalala kwenye mazingira gani na saa ngapi? Unafanya mazoezi? Unakula mara ngapi kwa siku? Unakunywa nini? Unapata hewa safi unapokuwa kazini au nyumbani? Unapata muda wa kwenda hospitali mara kwa mara kupima afya yako?

Hayo ni maswali ya msingi katika kujenga afya bora, kwa kuzingatia elimu ya afya na uhamasishaji miongoni mwa jamii, unapaswa kuwa njia muhimu katika utoaji wa huduma za afya.

Njia hiyo inatumia utaalamu wa mawasiliano kwa kutayarisha na kuwasilisha ujumbe mbalimbali kwa mtu binafsi, familia na jamii kwa lengo la kubadilisha mienendo na tabia zinazochangia kuwepo au kutokuwepo kwa maradhi katika jamii.

Hali hiyo ya afya bora inapokuwa tofauti, maana yake ndio kuumwa. Misemo hiyo inayotumiwa kila mara.

Kuna suala la unene kupita kiasi, hili, linachangia mwili kuwa na mafuta ya ziada ambayo hulimbikizana hadi kiwango kinachoweza kuathiri afya. Hapo inafungua mlango wa kuanza kupata matatizo ya kiafya.



# Wakulima hupoteza zao la maharage kwa kuoza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Uyole, umebaini kuwa wakulima wadogo wa maharage katika Wilaya ya Mbeya, wanapoteza asilimia 25 ya zao hilo kila mwaka kwa kuoza kutokana na kutokuwa na nyenzo bora za kukaushia hasa nyakati za mvua.

Hayo yalisemwa juzi katika Kijiji cha Mshewe kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa Tari Uyole, Dk. James Mrengela, wakati taasisi hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Ciati zilipokuwa zinakabidhi mtambo wa kukaushia mazao kwa kikundi cha wanawake cha Zinduka.

Alisema mazao ya wakulima hao huwa yanaoza baada ya kuvunwa kipindi cha mvua kutokana na kutokuwapo kwa jua la kutosha la kukaushia mazao.

Alisema wengi wa wakulima hao hawana mbinu za kisasa za kukaushia mazao hayo na kwamba ndio maana waliamua kupeleka mtambo huo kwa kikundi cha Zinduka ambacho kinazalisha maharage kwa wingi kuliko vikundi vingine.

"Wakulima wa eneo hili wana misimu miwili ya kulima maharage lakini msimu wanaopata zaidi ni wa mvua, lakini tumebaini kuwa hawana nyenzo nzuri za kukaushia na ndio maana kipindi cha mvua mazao yao huwa yanaoza sana," alisema Dk. Mrengela.

Alisema mtambo ambao walikabidhi kikundi cha Zinduka una uwezo wa kukausha tani moja kwa siku na kwamba mazao yanayokaushwa kupitia mtambo huo hayana madhara yoyote kwa afya za watumiaji wa mazao hayo.

Mwenyekiti wa kikundi cha Zinduka, Witness Sikayange, alizishukuru taasisi hizo kwa kuwasaidia mtambo huo na kwamba utawasaidia kuokoa mazao yao ambayo huwa yanaoza wakati wa mvua.

Alisema kikundi hicho kilianza kwa kulima ekari 10 za maharage, lakini kwa sasa kina ekari 300 ambazo kinalima mara mbili kwa mwaka na kwamba baadhi ya mashamba hayo walipewa na Mbunge wa Jimbo hilo, Oran Njeza.

Alisema kikundi hicho ni cha wanawake pekee na wamefanya utaratibu wa kusaidia kuundwa kwa vikundi vingine viwili ambavyo kimoja ni cha vijana pekee na kingine ni cha wazee.

"Tunaamini huu mtambo unatuongezea chachu ya kuendelea kuzalisha zaidi, awali tulikuwa tunapoteza mazao yetu na sasa tumeshajaribu kuutumia na kupata mafanikio makubwa sana," alisema Sikayange.

Pia alisema maharage wanayozalisha yanapata soko ndani ya Mkoa wa Mbeya kutokana na mahitaji ya mteja wao mkuu ambaye anawawezesha baadhi ya miundombinu.

# H'shauri Mbeya hatarini kufilisika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya iko hatarini kufilisika kutokana na kukabiliwa na kesi 21 mahakamani ambazo endapo itashindwa itatakiwa kulipa Sh. bilioni 11 ambazo ni sawa na fedha zilizokusanywa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo jana kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani kilichoandaliwa kwa ajili ya kujadili na kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Chalamila alisema kuwa hadi sasa Halmashauri ya Jiji hilo inakabiliwa na kesi hizo mahakamani zikiwamo zinazohusiana na masuala ya watoa huduma na masuala ya ardhi ambazo kama itashindwa na kutakiwa kulipa itakuwa na wakati mgumu.

"Kitu kingine ambacho kinaweza kuigharimu halmashauri yenu ni kesi nyingi ambazo mnashtakiwa mahakamani, kesi hizi mkishindwa mtapaswa kulipa zaidi ya Sh. bilioni 11, kiwango ambacho ni kikubwa na kitayumbisha sana halmashauri hii," alisema Chalamila.

Alisema katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Jiji la Mbeya imepata hati ya kuridhisha, lakini kesi zilizoko mahakamani zinaweza zikaifanya hati hiyo isiwe na maana yoyote na badala yake zitalifilisi jiji. Hata hivyo, alisema pamoja na jiji hilo kupata hati safi, bado kuna baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo sio waaminifu kwa madai kuwa baadhi ya kesi zilizoko mahakamani nyaraka zake kuibwa na kupotezwa na baadhi ya watumishi wa serikali.

Alisema baadhi ya watumishi ambao walionekana kutokuwa waaminifu, waliitwa na kuonywa na kuwataka watumishi kuwa waaminifu na kushirikiana na madiwani katika kuhakikisha jiji linaepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

Awali Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi, alisema katika mwaka wa fedha 2018/2019 jiji hilo limekusanya vizuri mapato na kufikia asilimia 86 na hivyo kushika nafasi ya tatu kati ya majiji sita tofauti na miaka mingine.

Alisema miaka ya hivi karibuni jiji hilo lilikuwa linatajwa kuwa miongoni mwa majiji yaliyokuwa yanakusanya mapato kidogo kuliko kama ilivyokuwa idadi ya vyanzo vyake.

Alisema kwa sasa wanataka katika miaka ijayo kukusanya vizuri mapato na kushika nafasi ya kwanza ama ya pili kati ya majiji yote.

"Upatikanaji wa hati hii safi tuliyoipata tunaamini ni kutokana na kufuata vizuri ushauri wako, lakini pia usimamizi wako umetusaidia na sasa hivi tunataka tuwe na mikakati ya kuhakikisha tunaendelea kupata hati safi," alisema Mwashilindi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema baada ya ukusanyaji wa mapato kutokuwa mzuri mwaka wa fedha uliopita waliamua kuunda kikosi kazi maalumu kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato.

Alisema kikosi kazi hicho kilikuwa kinaongozwa na wataalamu wa fedha wa halmashauri hiyo na ndiyo maana wamefanikiwa kukusanya vizuri mapato hayo hasa yanayohusiana na mapato yatokanayo na ushuru wa huduma.



Wafanyakazi wa kampuni zinazopanua barabara ya Morogoro, wakipanda nyasi kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi eneo la Kimara Suka jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Chunya yakusanya 75% ya malengo

**Na Nebart Msokwa,**

CHUNYA

IKIWA zimebaki siku chache kabla ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 kufikia mwisho, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya imefikia asilimia 75.3 ya malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Bosco Mwanginde, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya mwisho ya mwaka.

Alisema walipanga kukusanya Sh. bilioni 2.8, lakini wamekusanya Sh. bilioni 2.1.

Aliwataka madiwani na watendaji wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanashirikiana kukusanya mapato kwenye vyanzo mbalimbali ili mpaka kufikia tarehe ya mwisho wawe wamefikia angalau asilimia zaidi ya 80 kama maagizo ya serikali.

Alisema endapo ukusanyaji wa mapato ya ndani ukiwa mzuri hata uwezo wa halmashauri unaongezeka hivyo akasisitiza kuwa ni lazima vyanzo visimamiwe vizuri na mapato yakusanywe.

"Mapato ya ndani ndio dira ya mipango ya halmashauri na utekelezaji wa miradi tunayoibua wenyewe, mapato haya yanatusaidia kuwa na uwezo mkubwa wa kujitegemea katika uendeshaji wa halmashauri, tujitahidi kuhamasisha wananchi kulipa kodi," alisema Mwanginde.

Pia alisema halmashauri hiyo ina vyanzo vingi vya mapato ambavyo vikisimamiwa vizuri vinaweza vikaiingizia serikali mapato ya kutosha kuweza kujiendesha kwa kiwango kikubwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, alisema vyanzo vikuu vya mapato ya halmashauri hiyo ni kilimo na madini na kwamba vyanzo vingine ni vidogo na vinaingiza mapato ya wastani.


Alisema mazao wanayoyategemea zaidi ni tumbaku, ambalo ni zao kuu la biashara kwa halmashauri hiyo na kuna zaidi ya wakulima 5,800 wa zao hilo.

Alisisitiza kuwa atahakikisha anasimamia vizuri mapato yanayokusanywa ili mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wawe wamefikia lengo kwa kiwango kikubwa.

"Tunavyo vyanzo vingi vya mapato na kwa sasa tutahakikisha tunasimamia na kukusanya kikamilifu mapato haya na pia kuyatumia kwa malengo yanayokusudiwa ili kuhakikisha tunaboresha huduma za jamii," alisema Kumbuli.

Hata hivyo, alisema halmashauri hiyo kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), imeanza mipango ya kuboresha baadhi ya barabara za vijijini zikiwamo zilizopo katika Kata za Ifumbo na Nkung'ungu.

Alisema lengo la kutaka kuboresha barabara hizo ni kurahisisha usafiri na usafirishaji wa mazao ya wakulima kutoka mashambani kwenda sokoni.





## Huduma za usikivu kupelekwa wilayani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema katika kipindi cha miezi sita ijayo, itahakikisha watumishi wa afya katika ngazi za wilaya wanajengewa uwezo wa utoaji huduma za afya ya masikio, pua na koo ili zitolewe kwa wananchi ndani ya wilaya zao badala ya kulazimika kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo alipozindua mpango mkakati wa taifa wa usikivu.

Katika uzinduzi huo, waziri huyo pia alizindua kambi ya matibabu na huduma ya uchunguzi wa afya ya sikio unaotolewa na Taasisi ya Starkey Hearing Foundation ya Marekani kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

Waziri Mwalimu alisema tatizo la usikivu nchini bado ni changamoto kutokana na serikali kutokuwa na takwimu sahihi, hali ambayo inasababisha kushindwa kutambua ukubwa wa tatizo.

Alisema pamoja na serikali kukosa takwimu sahihi za tatizo la usikivu nchini, pamekuwapo na utafiti ambao umekuwa unafanywa na wadau mbalimbali wa masuala hayo.

"Katika utafiti huo, zinaonyesha kuwa asilimia tatu ya mwanafunzi wana matatizo ya kusikia na usikivu, hii inamaanisha kuwa kati ya watoto 100, watatu wana matatizo ya usikivu," alisema.

Aliongeza kuwa watu wenye magonjwa yasiyo ambukiza kama vile matatizo ya sukari, takwimu zinaonyesha asilimia 24 wana matatizo ya usikivu.

Pia, alisema watu wanaofanya kazi katika maeneo ya uchimbaji wa madini na katika viwanda vya kutengeneza nguo, asilimia 50 wana matatizo ya usikivu.

Alisema serikali imekuwa ikiboresha maeneo ya kutolewa huduma za afya ya masikio, pua na koo ikiwa ni pamoja na kutengeneza wataalamu wa kutosha na kwa sasa, Hospitali ya Taifa Muhimbili wanatoa huduma hizo.

"Kutokana na kutokuwa na wataalamu wa kutosha wa masuala ya masikio, nchi yetu imekuwa ikisafirisha watoto kwenda India, kila mwaka watoto 13 ambapo mtoto mmoja hutumia fedha kati ya Sh. milioni 80 hadi 100," alibainisha.

Mwalimu aliwataka wananchi kujijengea tabia ya kwenda kufanya vipimo vya masikio, pua na koo ili kubaini matatizo kwa wakati.

"Lakini pia wananchi waepuke pia matumizi ya dawa bila kufanyiwa vipimo, matumizi ya vijiti katika kuchokonoa masikio, hali inayochangia katika kuharibu ngoma za masikio, lakini kwa vijana waache matumizi ya spika za masikio kwani ni moja kati ya sababu ya kuharibu masikio," Mwalimu alisema.

# Wanne mbaroni uhamiaji haramu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kujihusisha na biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu kutoka Ethiopia.

Imedaiwa kuwa watuhumiwa hao walikamatwa eneo la Chipogolo lililoko wilayani Mpwapwa wakisafiri kwa basi namba T 122 ATD aina ya Scania, mali ya Kampuni ya Premier Line linalofanya safari zake kutoka Mwanza kwenda Mbeya.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni pamoja na Charles Mzola (40) ambaye ni mkazi wa Morogoro na Dago Kundemba (22), mkazi wa Muheza, Tanga.

Kamanda Muroto alisema watuhumiwa hao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kusomewa mashtaka yao kutokana na biashara hiyo.

Alisema kukamatwa kwa watu hao kumetokana na ushirikiano wa jeshi hilo na viongozi wa serikali za mitaa na vikundi vya ulinzi shirikishi ambavyo vinasaidia kuwaibua wahalifu walioko mitaani.

Katika tukio lingine, jeshi hilo limefanikiwa kuwakamata Emanuel Fulgensi (18), mkazi wa Kizota na Mohamed Ngaliae (21), fundi pikipiki na mkazi wa Chinangali, Dodoma, wote wakituhumiwa kukutwa na pikipiki mbili aina ya Feco na T-Better zinazodaiwa za wizi zisizo na namba za usajili.

Kamanda Muroto alidai watuhumiwa hao pia walikamatwa na betri nne za magari, baiskeli, subwoofer na simu mbili za mezani.

Alidai watuhumiwa hawa wana kikundi chao cha uhalifu na jeshi linaendelea kuwasaka washirika wengine wa kikundi hicho kwa kuwa tayari limeshapata orodha yao.

Kamanda Muroto pia alisena jeshi hilo pia limefanikiwa kuwakamata watu 10 wanaotuhumiwa kujihusisha na kusajili laini za simu kwa kutumia vitambulisho vya watu wengine na kuzalisha line nyingi kwa kitambulisho kimoja bila ridhaa ya mwenye kitambulisho kisha kuziuza laini hizo kwa wahalifu wasio na vitambulisho.

Pia, alisema jeshi hilo katika msako wake limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa saba wanaodai wa kujihusisha na makosa ya uvunjaji, unyang'anyi na wizi wa kuhamahama katika maeneo ya Kibaigwa, Chamwino mkoani Dodoma, Kilosa (Morogoro), Kilindi (Tanga) na Dar es Salaam.

Kamanda Muroto alidai watuhumiwa hao wamekamatwa na vifaa mbalimbali vya kuvunjia, kukatia na pikipiki.

"Uhalifu huu haukubaliki kabisa mkoani Dodoma, tutaendelea na msako ili kuwanasa wahalifu," Kamanda Muroto alisema.



Mhandisi Idrisa Noorane wa Kampuni ya Ujenzi ya Mohammed Builder akiwaonyesha waandishi wa habari (hawapo pichani) maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kituo kikuu cha mabasi jijini Dodoma, ujenzi huo unatekelezwa na kampuni hiyo na awamu ya kwanza inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba mwaka huu. **PICHA: IBRAHIMU JOSEPH**

# Waziri awaagiza makandarasi kuweka umeme katika majengo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WIZARA ya Nishati imewataka makandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme maeneo mbalimbali nchini kuhakikisha majengo ya huduma za umma yanakuwa na nishati hiyo muhimu.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alipokagua na kuzindua mradi wa umeme katika Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma.

"Leo katika ziara yangu nimeanza na kuzindua umeme hapa Shule ya Sekondari Mbicha na nimesikia wanachangamoto ya kusambaza umeme kwenye vyumba vingine vya madarasa, nimeongea na makandarasi na yeye atoe mchango wake, nashukuru amekubali," alisema.


Alisema makandarasi wanaopewa kazi na serikali kusambaza umeme, wanao wajibu wa kutoa mchango wao kwenye jamii kwa kusambaza umeme kwenye majengo ya huduma za umma katika maeneo wanayotekeleza miradi.

Aliongeza kuwa kwa kufanya hivyo, watasaidia kuimarisha ushirikiano na umoja kati ya makandarasi na wananchi kwenye maeneo hayo ya miradi.

Aliyataja maeneo ambayo makandarasi hao wanaweza kutoa mchango wao wa kusambaza umeme kuwa ni vituo vya afya, zahanati, shule na miradi wa maji.

"Umeme ni biashara kwa sababu mtu akitaka kuunganishiwa umeme, lazima atalipa fedha na akiunganishiwa ataweza kulipa bili zake kila mwezi, itasaidia serikali kuongeza mapato," alisema.

Meneja wa Tanesco Wilaya ya Kondoa, Emily Ntazimila, alisema kuna jumla ya vijiji 84 wilayani humo. Kati yake, 29 vimeunganishwa na huduma ya umeme.



# HABARI ZANZIBAR



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akijaza fomu za kufungua akaunti Benki ya Afrika (BOA), katika Majengo ya Baraza la Wawakilishi Chukwani, (kushoto ) ni Meneja wa Benki hiyo Zanzibar, Juma Burhan Mohamed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wizara yatakiwa kuwa na mfumo bora usimamizi skauti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imetakiwa kuhakikisha kwamba katika mipango na taratibu wanazoziandaa ni vyema wakajipanga vizuri ili uwepo mfumo bora na endelevu wa uratibu na usimamizi wa shughuli za skauti.

Akizungumza katika maadhimisho ya miaka 107 ya Skauti uliofanyika Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema ni muhimu uwepo mfumo wa namna moja na unaotambulika rasmi katika kila ngazi inayohusika jambo ambalo litaongeza hamasa na mipango katika kukuza uzalendo, kuamsha ari na kuwakumbusha wanafunzi historia ya nchi yao.

Alieleza kuwa miongoni mwa mambo ambayo yanahitaji kusimamiwa vyema ni lazima kuongezeka kwa heshima, hadhi na thamani za nyimbo za taifa, wimbo wa mashujaa, bendera na nembo za taifa.

Alisisitiza kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inapaswa kuangalia kuona namna bora ambayo misingi wanayopewa vijana wa skauti wanakuzwa nayo ili wawe raia wema na wazalendo.

Dk. Shein aliwataka viongozi wa vijana wa skauti kuwa wamoja na kuepuka vitendo vyovyote vyenye kuashiria ubaguzi.

Alieleza kuwa kwa mnasaba huo shughuli za skauti zina fursa kubwa na nzuri kuendeleza hisia za umoja hasa miongoni mwa vijana na katika hali hiyo vijana hao watakuwa wanapewa urithi bora na kwenda na wakati.

Aidha, Dk. Shein alisisitiza haja ya kuwaandaa vijana hao ili kuwa wazalendo wa taifa, akibainisha maendeleo ya nchi na jamii yeyote huletwa na wazalendo.

Alisema uzalendo ndio unaohimiza mtu kufanya bidii, ari, hamasa na kuwa mwadilifu katika kazi za halali na hivyo kupata tija na manufaa.

Alisema uzalendo humuongoza mtu kuzilinda na kuzitumia vyema rasilimali za nchi kwa faida ya wananchi na kumwepusha kufanya vitendo vya ubadhirifu, rushwa na wizi wa mali ya umma.

Dk. Shein alibainisha kuwa baada ya Mapinduzi, Taifa lilipata maendeleo ya haraka ikiwamo uimarishaji wa miundombinu na upatikanaji wa huduma za kijamii, pamoja na wananchi kushiriki kwa moyo katika ujenzi wa nyumba za maendeleo, barabara na vituo vya afya.

"Kwa bahati mbaya ari na moyo huo umepungua sana hivi sasa, miongoni mwetu, mambo yamebadilika utaratibu wa kujitolea haupewi nafasi kubwa kama zamani," alisema.

Aliwapongeza vijana wa skauti kwa jinsi walivyo makini na wanaotunza nidhamu, akibainisha kuwa ndio msingi wa mafanikio ya kila kitu.

Alisema mafunzo yanayotokana na shughuli za skauti yanasaidia kuwafanya vijana kuwa raia wema wenye kutii sheria na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuhatarisha amani.

Alisema vijana wanaopata mafunzo ya skauti huwa wanaandaliwa vyema kuwa walinzi wazuri wa amani.

Naye, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema wizara hiyo kwa kushrikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, zitaendelea kushirkiana katika kuwaandaa vijana kufanikisha misingi ya kuanzishwa kwa skauti nchini.

Kwa upande wake Skauti, Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania, Mwantum Mahiza, alipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa maandalizi mazuri yaliofanikisha vyema maadhimisho hayo.

Alisema maadhimisho hayo yana dhamira ya kuwajengea vijana hao kuwa wazalendo, ujasiri pamoja na wenye kujitolea wakizingatia dhana ya uaminifu na uadilifu.

## Utafiti waonyesha ukuaji sekta ya utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale imesema kuwa zipo tafiti na ripoti mbalimbali zilizofanywa zinaonyesha mwenendo wa ukuaji wa sekta ya utalii Zanzibar.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Chum Kombo Khamis, wakati akijubu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarahan, aliyetaka kujua kama kuna utafiti uliofanywa kuhusu ukuaji wa sekta ya utalii. Naibu Waziri huyo alizitaja ripoti ya programu ya matokeo kwa ustawi wa mwaka 2014 na ripoti ya mkakati wa mageuzi ya kiuchumi na kijamii ya mwaka 2017. Alisema ripoti nyingine ni uimarishaji wa sekta ya utalii na kamisheni ya mwaka 2017 na ripoti ya maeneo mkakati ya uwekezaji wa mwaka 2019 na rasimu ya mpango jumuishi ya sekta ya utalii.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hufanya utafiti wa utokaji wa wageni kila mwaka," alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea na utekelezaji wa ripoti na utafiti ambao umezingatia uendeshaji na utengenezaji wa sekta ya utalii."

Alieleza kuwa wizara yake imeunda kamati maalumu ya kuandaa mpango wa muda mfupi wa uimarishaji wa sekta ya utalii katika kisiwa cha Pemba.

"Kamati imeshaanza kazi na inajumuisha wajumbe kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi," alisema.

## Serikali yaanda daftari la kuthamini mali zake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Muhammed Ramia, amesema wizara yake imeandaa daftari la mali za serikali la kielektroniki ambalo limezitambua mali na kuziwekea alama na kuzitia thamani.

Aliyaeleza hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarahan.

Alisema hadi kufikia Machi, jumla ya mali 200,000 zimetambuliwa na kuwekwa alama za utambuzi pamoja na kutiwa thamani.

Alieleza kuwa kazi iliyobakia ili kukamilisha daftari hilo ni utambuzi wa majengo na kuyawekea alama.

"Matarajio yetu daftari la mali za serikali litakamilika mwaka wa fedha 2019/2020," alisema.

Alieleza kuwa wizara yake ina utaratibu wa kufanya mapitio katika wizara na idara za serikali ili kuhakiki uwepo wa mali hali zake.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2018/2019 wizara yake ilizi-andikia wizara zote za serikali na kuzitaka kuwasilisha orodha ya vifaa chakavu ili vihakikiwe kuthaminiwa kabla ya zoezi la kuondoa kufanywa.

Pia alisema hadi kufikia Machi mwaka huu, mapitio ya mali chakavu za wizara 12 yamefanywa na kuhakikiwa.

Alisema wizara imeziondoa kwa njia ya minada na kukusanya jumla ya Sh. milioni 274.

Alisema wanakusudia kuhakikisha wizara ambazo mali zake hazijahakikiwa zinafanywa hivyo ili kuona serikali inapata mapato kutokana na mali chakavu.

# Bodaboda wataka kumuona Waziri Lugola

**Na Beatrice Moses**

BAADHI ya madereva wa bodaboja jijini Dar es Salaam wameeleza jinsi wanavyojipanga kuonana na Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, ili wamweleze kero zinazowakabili hasa kutoka kwa askari wa usalama wa barabarani wanaochochea ukamatwaji wa kuvizia.

Wakizungumza katika majadiliano yaliyofanyika kwenye warsha ya Waendesha Bodaboda na wajasiriamali wasindikaji iliyofanyika jijini Dar es Salaam, wamebainisha kuwa kuna mengi yanayowakabili ambayo yamekuwa kikwazo kwa maendeleo yao na kuzua changamoto kwenye kazi yao.

Dereva wa bodaboda jijini Dar es Salaam Msafiri Shabani, alisema wamekuwa wakikamatwa kwa kuviziwa kwenye mataa ambapo wakamataji wamekuwa wakirukia, hali ambayo uhatarisha maisha yao, abiria na watumiaji wengine wa barabara.

" Yaani hawa watu wanahusika kusababisha ajali kutokana na ukamataji wao, tukikutana na waziri tunamweleza pamoja na faini kubwa ambazo tumekuwa tunapigwa ambazo ni tofauti na zile zinazotajwa kuhusika na pikipiki, pia pikipiki kushikiliwa kwenye vituo kwa muda mrefu, usumbufu mwingi tumekuwa kama vitega uchumi vya watu fulani," alisema Shabani.

Akizungumza katika warsha hiyo iliyoandaliwa na Youth Partnership Countrywide, Shabani alisema kuna vikao kadhaa walishakaa na baadhi ya viongozi wa kikozi cha usalama wa barabarani walifikisha malalamiko yao, lakini hayajafanyiwa kazi, ndiyo maana wanajipanga kumuona Waziri ili kumweleza kero zinazowakabili.

Dereva mwingine, Omary Makusika wa Kinondoni, alisema madereva wa boda boda wamekuwa wakitajwa kwa mabaya mengi ikiwamo kujihusisha katika mapenzi na wanafunzi jambo ambalo linawachafua katika jamii.

"Yapo mazuri tunayoyafanya lakini wote tunajumuishwa kwa mabaya, mfano sisi tumekuwa na kampeni ya kuhakikisha tunadhibiti mmomonyoko wa maadili kwa wanafunzi kwa kuhakikisha ama hawakai vituoni au vijiweni, wengi tumekuwa tukiwalazimisha wapande magari waende shule ama nyumbani tunapowabaini kuwa wanajizubaisha vituoni ," alisema Makusika.

Fred Mtei wa Kibaha, alisema pia katika eneo analotoka mkoani Pwani kulizuka mabishano baaada ya madereva wa bodaboda kutakiwa kulipa Sh. 20,000 ili wapewe vitambulisho vya ujasiriamali .

Mkurugenzi Mtendaji wa YPC, Israel, Ilunde alisema kuwa wame andaa warsha hiyo ikiwa ni kutimiza lengo namba nane la maendeleo endelevu linazungumzia upatikanaji ajira na kazi za staha, hivyo wameona bodaboda inachukua vijana wengi.

Alisema hivyo wameona ni vyema kuangazia mazingira ya ufanyaji kazi wa makundi hayo, ili kuishauri serikali kuboresha sera na kuangalia ubora wa kazi zao ili watu wanaofanya kazi hizo waweze kuzifanya katika mazingira mazuri ambayo yatakuwa na matokeo yenye mafanikio kwa jamii na taifa kwa ujumla.

" Viwanda vya Tanzania itakuwa imara iwapo mazingira ya sekta hizi mbili yataangaliwa kwa makini, kilimo ni muhimu hivyo pembejeo zikipatikana mazao yatazalishwa kwa wingi wakati miundombinu ikiwa mizuri, mazao yatafikishwa kwenda kwenye masoko," alisema Ilunde.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Nicholas William, akifungua kongamano jijini Das es Salaam jana la lugha ya Kiswahili kwa nchi za Afrika. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# WMA yahakiki mizani 1,259 mikoa ya kusini

**Na Mwandishi Wetu,**
RUVUMA

MIZANI 1259 itakayotumika kupima ufuta imehakikiwa na Wakala wa Vipimo nchini (WMA) ikiwa ni maandalizi ya msimu wa ununuzi wa zao hilo katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma.

Hayo yalibainishwa na mameneja wa mikoa hiyo kwa nyakati tofauti jana, na kusema zoezi hilo la kushtukiza linakwenda sambamba na utoaji wa elimu ya vipimo sahihi kwa wakulima wa ufuta.

Meneja wa WMA Mkoa wa Mtwara, David Makungu, alisema mizani 575 imehakikiwa katika mkoa wake.

Alisema katika uhakiki huo wameweza kuvifikia vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) 270.

Makungu alisema mizani hiyo imepigwa chapa tayari kwa kutumika kwenye biashara ya ununuzi wa ufuta, huku mizani 36 ilionekana kuwa na hitilafu na ilifanyiwa marekebisho na mafundi wa mizani.

"Katika wilaya sita, Masasi ndiyo inaongoza kwa kuwa na AMCOS 51, ikifuatiwa na Nanyumbu (41), Tandahimba (11), Halmashauri ya Nanyamba (6), Newala (5) na Mtwara Vijijini inazo AMCOS (4).

"Kwa maana hiyo Mtwara ina jumla ya AMCOS 119 zinazohusika na ununuzi wa zao la ufuta kutoka kwa wakulima," alisema Makungu.

Meneja wa WMA Mkoa wa Lindi, Yunio Mbwambo, alisema katika mkoa wake jumla ya mizani 521 imehakikiwa kwa ajili ya ununuzi wa ufuta.

Alisema mizani hiyo imepatikana katika AMCOS 122 za Wilaya za Ruangwa (27), Nachingwea (38), Kilwa (24), Liwale (15), Lindi Vijijini (13) na Lindi Manispaa ikiwa na AMCOS tano tu.

Aidha, Mbwambo aliongeza kuwa katika uhakiki huo walikamata mzani mbovu mmoja uliokuwa unatumika na wahusika walikiri kosa na kutozwa faini ya Sh. 500,000 na mzani huo kufanyiwa marekebisho.

"Pia katika Wilaya ya Liwale tulikamata mizani mitatu yenye makosa na wahusika walikiri na kutozwa faini ya Sh. milioni 1.5 na hili nataka liwe fundisho kwa wengine wenye tabia ya kuchezea mizani kwa lengo la kujinufaisha binafsi.

"Ukaguzi huu wa kushtukiza unaendelea sambamba na utoaji wa elimu kwa wakulima wa ufuta ili wafaidi matunda ya jasho lao," alisisitiza.

Ruvuma jumla ya mizani 163 imehakikiwa na kupigwa chapa ya WMA tayari kwa ununuzi wa ufuta msimu huu. Meneja wa WMA mkoani humo, Hassan Halletu, alisema jana kuwa AMCOS 29 zimefikiwa na mizani yake kuhakikiwa, huku wakulima wa ufuta wakipata elimu juu ya vipimo na matumizi sahihi ya mizani hiyo.

WMA inaendelea na kaguzi za kushtukiza katika mikoa inayolima ufuta, tumbaku, pamba na kahawa.

# 'Usajili walinzi binafsi utachochea amani, utulivu

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi limesema mpango wa kuwasajili walinzi binafsi, unaotekelezwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Huduma za Kuunganisha Walinzi Binafsi (TPSIS), utachochea kasi ya kudumisha amani na utulivu nchini.

Mkuu wa Idara ya Kampuni za Ulinzi katika Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Narcis Misama, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na mwandishi wa habari kuhusu mpango huo uliozinduliwa hivi karibuni na TPSIS.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa TPSIS, Dk. David Rwegoshora, mpango utawahusu walinzi binafsi nchini nzima na kwamba pamoja taarifa zao kujulikana hadi polisi, itakuwa fursa kwa waajiri kuwapata walinzi wanaoaminika na watakaopitia mafunzo ya kudhibiti uhalifu kabla haujatokea.

Alisema kwa namna ilivyopokea maelezo ya mpango huo uliobuniwa na TPSIS, imebaini kwamba utalisaidia Jeshi la Polisi kukabiliana na uhalifu kirahisi zaidi.

Alisema polisi ipo tayari kuisaidia TPSIS kuwatambua na kuwafikia walinzi binafsi nchi nzima na kuwaingiza katika mfumo unaojulikana kama kanzi data wenye uwezesha kuwajua, mahali walipo na wanavyofanya kazi.

Kwa mujibu wa Kamishna Misama, TPSIS ilijitambulisha na kuutambulisha mpango kwa polisi, ulipobainika kuwa wenye manufaa hasa kwa walinzi na waajiri wao.

Akiutambulisha mpango huo jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Dk. Rwegoshora, alisema pamoja na kutoa mafunzo ya kudhibiti uhalifu kabla haujatokea, walinzi wataunganishwa na masoko mbalimbali ya ajira kupitia taarifa zao kwenye kanzidata.

## Oman yasema itafungua ubalozi ukanda wa Palestina

**MUSCAT, Oman**

OMAN imesema inapanga kufungua ubalozi mpya katika eneo linalokaliwa kwa mabavu na Israel Ukanda wa Magharibi na kwamba ujumbe wa wizara yake ya mambo ya nje utakwenda Ramallah kwa ajili ya ufunguzi huo.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters nchi hiyo ilitangaza uamuzi huo wakati Washington ikizindua mpango wa kiuchumi ambao inasema utakuwa ni msingi wa amani kwa Israeli na Palestina.

Lakini Wapalestina na nchi nyingi za Kiarabu zimesema hatua hiyo haina faida bila ya kuwapo kwa suluhisho la kisiasa.

"Kwa kuzingatia msaada wa Oman kwa ndugu zetu wa Palestina, imeamua kufungua ubalozi mpya kwa ajili ya Wapalestina katika kiwango cha ubalozi," Waziri wa Mambo ya Nje aliandika katika ukurasa wake wa kijamii wa Twitter.

Ujumbe kutoka Wizara ya Mambo ya Nje utaelekea Ramallah kuanza taratibu za kufungua ubalozi huo," ujumbe wa tweet uliongeza.

Taarifa zaidi zimeeleza kuwa Oman ilifunga ubalozi wake Gaza kufuatia shambulio la mabomu lililofanywa na Israel mwaka 2006 katika eneo la ardhi hiyo, lakini iliendeleza ushirikiano wa karibu na serikali ya Palestina.

Ofisa wa ngazi ya juu wa chama cha ukombozi cha Palestina, PLO, Hanan Ashrawi, alipokea kwa furaha uamuzi huo na utambuzi wa namna yeyote ule wa taifa la Palestina.

"Ni matumaini yangu ubalozi utasaidia kuwaelimisha serikali ya Omani kuhusu uhalisia wa vitendo vya uvamizi vya Israeli," alisema Ashrawi.

Oman kwa muda mrefu imekuwa ikifahamika Mashariki ya Kati kuwa haina upande kama vile Switzerland ilivyo kwa diplomasia ya kimataifa.

Nchi hiyo imesaidia kusimamia kwa siri mazungumzo kati ya Marekani na Iran mwaka 2013 ambayo yalisababisha makubaliano ya kihisitoria ya mkataba wa nyuklia uliosainiwa Geneva miaka miwili baadaye.

Oman imekuwa ikitoa ushauri kusaidia Israel na Wapalestina wakutane japokuwa haifanyi hivyo kama msuluhishi wa moja kwa moja.

Mwaka 2018, Waziri Mkuu wa Israeli, Benjamin Netanyahu, alifanya ziara ambayo ni nadra kutokea mjini Muscat na kujadili juhudi za amani Mashariki ya Kati na kiongozi wa Oman, Sultani Qaboos.

*VOA*

# Tamko la kibaguzi: Mbunge Jaguar akamatwa

**NAIROBI, Kenya**

MAOFISA wa polisi nchini Kenya wamemkamata Mbunge wa Jimbo la Starehe, Charles Kanyi maarufu kama Jaguar, anayedaiwa kutoa kauli za chuki dhidi ya wafanyabiashara wa Tanzania na Uganda waliopo jijini Nairobi.

Vyombo vya habari vya nchi hiyo vimeripoti kuwa Jaguar alikamatwa jana mchana akiwa anatoka kwenye viwanja vya Bunge.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa mbunge huyo alikamatwa kutokana na kauli yake aliyoitoa hivi karibuni kuhusiana na wafanyabiashara kutoka nchi jirani na Kenya.

Katika kanda ya video iliosambazwa nchini Kenya na Tanzania, mbunge huyo alisema hawatokubali watu kutoka nje ya Kenya kufanya biashara nchini humo.

"Wakenya ni sharti wafanye biashara zao bila kushindana na watu kutoka mataifa mengine. Raia wa Pakistan wametawala biashara za kuuza magari nchini humu, Watanzania na Waganda wanatawala katika masoko yetu. Tunasema imetosha iwapo hawatarejeshwa nyumbani katika saa 24, tutawashika na kuwapiga na hatuogopi mtu yeyote," alinukuliwa Jaguar na kuongeza:

"Kwa hivyo mimi naomba waziri aangalie na ahakikishe kuwa Wakenya wetu wanafanya biashara bila ya kushindana na wageni kutoka nchi mbalimbali, ukiangalia magari yanavyouzwa hapa Wapakistan wamechukua hiyo biashara, ukiangalia nyamakima Wachanise wamechukua hizo biashara, ukiangalia masoko zetu, Watanzania na Waganda wamechukua hizo biashara".

Licha ya Serikali ya Tanzania kuwaomba raia wake kuwa na utulivu na serikali ya Kenya kujitenga na matamshi ya mbunge huyo, bado gumzo linaendelea katika mitandao ya kijamii huku baadhi wakimtaka mbunge huyo aombe radhi kwa matamshi yake.

Wakati hayo yakijiri, serikali ya Kenya imewahikishia wawekezaji wa kigeni usalama wao na mali baada ya Jaguar kuwatishia kuwafukuza nchini humo.

Mbunge huyo Charles Kanyi maarufu kama Jaguar, alipa serikali saa 24 kuwatimua wageni walioko nchini vinginevyo angewatimua mwenyewe.

Msemaji wa Serikali ya Kenya, Cyrus Oguna, alisema kuwa matamshi ya Jaguar yamelaaniwa.

Kwenye taarifa kwa vyombo vya habari, serikali ilipinga matamshi hayo na kusema kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya Jaguar, bila ya kutaja ni hatua zipi.

Kwenye video inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii, Jaguar aliwaambia raia wa kigeni kufunga virago na kurejea kwao, na wasipofanya hivyo, atawalazimisha kuhama.

Hata hivyo, Serikali ya Kenya imejitenga matamshi hayo kwenye taarifa yake, ikieleza kuwa hayana nafasi katika mazingira ya watu wastaarabu kama Wakenya wanaoishi kwa amani na kupenda wageni wa mataifa mbalimbali.

*BBC*




Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo ambaye kwa sasa yupo India kwa mazungumzo na Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Narendra Modi, katika juhudi za kulinda uhusiano kati ya mataifa hayo. **PICHA: ALLIANCE**

# Vita vya kibiashara Marekani na China vyapamba moto

**WASHINGTON, Marekani**

WAKATI nchi zenye kustawi kiuchumi (G20), zikitarajia kukutana jijini Osaka Juni 28 hadi 29, mwaka huu, Rais wa Marekani, Donald Trump, anatarajia kuweka mfululizo wa vikwazo vipya vya kiuchumi dhidi ya Beijing.

Vikwazo hivyo vinaweza kuathiri mauzo ya nje ya China kuanzia Julai, na endapo vikwazo hivyo havitatosha, Rais Trump anapanga hatua nyingine inayohusiana na viwango vya ubadilishaji wa sarafu za dunia.

Rais Trump aliagiza Wizara ya Biashara ya Marekani kutayarisha sheria mpya ambayo Marekani inaweza kuwa pekee yenye uwezo wa kuhukumu, ikiwa hatua za sera za fedha zinazochukuliwa mahali pengine duniani zinaathiri maslahi ya Marekani.

Kwa mpango huo, Marekani inaweza kuweka ushuru wa forodha kama adhabu kwa nchi yoyote ambayo wanaamini ingeweza kudhoofisha sarafu yake, ili kufanya mauzo yake ya bei nafuu kuliko bidhaa za Marekani.

*RFI*

# Polisi wanasa madini kwenye mchele yakitoroshewa Kenya

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

JESHI la Polisi mpaka wa Namanga Wilaya ya Longido mkoani Arusha, limekamata madini ya aina mbalimbali zaidi ya kilo 36 yakitoroshwa kwenda Kenya.

Yalikuwa kwenye gari namba T 716AAC aina ya Scania Perfect, mali ya Charles Shoo, mkazi wa Arusha.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alithibitisha kukamatwa kwa madini hayo na kueleza kuwa yalikutwa kwenye gari lililokuwa limebeba mchele kuelekea Kenya

"Madini yamewekwa katikati ya maguni, mbwa maalumu wa Jeshi la Polisi walibaini hili," alidai Mwaisumbe.

Alisema kuwa madini yaliyokamatwa ni tanzanite kilo 24, rubi (3), green ganet (5) na mengine zaidi ya kilo 8.5.

Hata hivyo, mkuu huyo wa wilaya alisema hadi sasa thamani ya madini hayo haijabainishwa.

Aliwataka wale wote wenye tabia za kufanyabiashara za madini bila kufuata utaratibu, zikiwamo za magendo kuacha mara moja, kwa kuwa atakayebainika, atachukuliwa hatua kali za kisheria, kwa kuwa ni kuhujumu uchumi wa nchi.

"Jeshi lipo makini, tutawakamata wote wenye kufanya biashara za magendo," aalisema Mwaisumbe.

Kwa upande wake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alisema amepata taarifa hizo na zikikamilika, ataita vyombo vya habari na kuweka wazi.

"Nimepata taarifa hizo, ila hazijakamilika vizuri," aliongeza Kamanda Shana.



Mkazi wa jijini la Dar es Salaam, akipita karibu na boksi la takataka lililowekwa kwenye makutano ya Barabara ya Kenyatta na Kinondoni ambalo halijazolewa kwa muda mrefu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM aitaka TIB kukopesha wakulima

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Benki ya TIB kuelekeze nguvu zake kwa kukopesha wananchi wa kawaida wakiwamo wakulima wa pamba wa Kanda ya Ziwa.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dodoma, alipokuwa akifungua tawi la saba nchini la benki hiyo ambayo kwa sasa inajulikana kama TIB Corporate Bank Limited - (TIB-CBL).

Alisema hivi sasa serikali inahangaika na mikopo kwenye sekta ya pamba na kuishauri benki hiyo kujielekeza huko kwa ajili ya kuwakopesha wakulima.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 16 tu ya Watanzania wanaotumia mfumo rasmi wa benki hali aliyosema kuwa inaonyesha kuwa bado kuna changamoto kwenye sekta ya benki katika utoaji wa huduma.

"Mnatakiwa mlifanyie kazi hili, changamoto ya pili ya sekta ya benki ni tozo na riba kuwa juu zaidi ya mfumuko wa bei Benki Kuu imesaidia sana kwa kupunguza riba zake zinazotumika inapozikopesha benki za biashara na zile za hati fungani," alisema Majaliwa.

Alisema serikali ina taarifa kuwa baadhi ya kampuni huandaa taarifa mbili za fedha, moja hupelekwa benki na nyingine hupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Sasa sisi serikali tukizipata zile zinazopelekwa benki kwa ajili ya kukopa, tutazitumia hizo hizo kukudai kodi kubwa," alisema.

Aliitaka BoT iendelee na utaratibu wa kuzifunga benki zote ambazo hazina tija kama ilivyofanya mwaka jana.

Aliipongeza TIB kwa kufanikisha kukuza mtaji wake kutoka Sh. bilioni 206 mwaka 2015 na kufikia Sh. bilioni 409, mwaka jana.

"Niwapongeze pia kwa kukuza amana za wateja kutoka Sh. bilioni 110 mwaka 2015 hadi Sh. bilioni 338, mwaka jana," alisema Majaliwa.

Aliipongeza benki hiyo kwa kutoa mikopo kwa riba ya chini ya kati ya asilimia tisa hadi 15.

"Kiwango hicho ni kidogo kulinganisha na kiwango cha soko ambacho kuna baadhi ya benki kinafika hadi asilimia 22," alisema. Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TIB, Frank Nyabundege, alisema Tawi la TIB la Dodoma limepewa jina la Capital Branch (Tawi la Makao Makuu ya Nchi), likilenga kuwafikia wafanyabiashara wote wa mikoa ya Kanda ya Kati.

Alisema mpaka mwaka jana, TIB ilikuwa imetoa mikopo ya Sh. bilioni 224.35 kwa taasisi za serikali.

Alizitaja kuwa ni pamoja na TTCL, MSD, Tanzania Railways Corporation, Tanzania Civil Aviation Authority (TCIA), Urafiki Textile Mills, Camalec na Bariadi District Council.

Nyabundege alisema mikopo hiyo imesaidia kazi za taasisi hizo kuendelea bila kusubiri ruzuku ya serikali.

"Mwaka huu, TIB imesaini makubaliano ya kuzikopesha taasisi mbalimbali za serikali jumla ya Sh. bilioni 130," alisema.

# Ujenzi wa daraja la Salender mwezi ujao

**Na Elizabeth Zaya**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Mhandisi Patrick Mfugale, amesema ujenzi rasmi wa daraja la Salender (Tanzanite) unatarajiwa kuanza mwezi ujao.

Mfugale alisema hayo jana mbele ya Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliotembelea kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Alisema kwa sasa wanaendelea kukamilisha ujenzi wa daraja la muda la kupitisha mizigo kwa ajili ya kupitisha vifaa vitakavyotumika katika ujenzi wa daraja hilo ambavyo vyote vimeshawasili.

Mfugale alisema mradi wa ujenzi huo umeajiri wafanyakazi wapatao 460, huku 435 wakiwa wazawa sawa na asilimia 90 na waliosalia ni kutoa nje.

Alisema wanatarajia ifikapo Oktoba 14, mwaka 2021 daraja hilo liwe limeshakamilika.

Mhandisi Mfugale alisema daraja hilo lenye urefu wa kilometa 1.3, litasaidia kupunguza foleni katika Jiji la Dar es Salaam kwa asilimia 30.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe, Jasely Mwamwale, alipongeza serikali kwa utekelezaji wa mradi huo pamoja na kutoa ajira kwa idadi kubwa ya vijana.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, alisema miti iliyokatwa katika eneo la ujenzi wa daraja hilo, Rais John Magufuli ameagiza itumike kwa ajili ya utengenezaji wa vifaa vya sanaa.

**Alisema kwa sasa wanaendelea kukamilisha ujenzi wa daraja la muda la kupitisha mizigo kwa ajili ya kupitisha vifaa vitakavyotumika katika ujenzi wa daraja hilo ambavyo vyote vimeshawasili.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA



### PASIPOTI IMEPOTEA



**JULIAS MAHAGAIKO CHASAMA** anatangaza kupotelewa pasipoti yenye namba **TEA050433** iliyotolewa mwaka 2018 na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es Salaam.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu au awasiliane na Ofisi ya Uhamiaji
Taarifa polisi:**KAH/RB/3794/2019**

115290702


### KUPOTEA KWA CHETI



**Immanuel Christopher** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba P.3605-0050** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari Gataraye Research and Training Centre Yeyote atakaekiona atoe taarifa kito chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **TBT/RB/3299/2015**

115295602


### KUPOTEA KWA CHETI



**Julius Nyanda Golani** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S3014-0104** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Nundu. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kito chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MBA/RB/83885/2019**

115296002

### CHETI KIMEPOTEA



**DAVID DIRISHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0537-029** kilichotolewa na **SEKONDARI YA MTAKATIFU PAULO** mwaka 1991. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/84574/2019.**

115296902

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAMIAN J. SAMBULILA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USJILI **MC 965 BPK** AINA YA HAOJUE. YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MB/TR/RB/456/19.**

115296702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;127/2019**

**Ombi la MICHAEL P.NYONI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ELIZABETH FRANCES PALANGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/06/2019.

115296402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;137/2019**

**Ombi la (1)SOPHIA JOSEPH PANJA(2)STEVEN CHARLES NA EDWARD CHARLES Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CHARLES EDWIN MTOI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 26/06/2019.

115296502

### KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HASSAN BASHIRU KIPERA** anatangaza kupotelewa na Kadi ya PIKIPIKI yake yenye Namba za Usajiri **MC 625 ASQ.** Hivyo kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu . Taarifa Polisi **SO/RB/4446/2019.**
***Au apige simu Namba***
**0754 241 378.**

115297202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;132/2019**

**Ombi la WAMINGILA FRANCES Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu DEOSDEDIT VICENT GUNDE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/06/2019.

115296302

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMES THOBIAS CHUWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.990 CPD** AINA YA SCANIA NA T.778 CPC TRELLER. YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **TUK/RB/972/19.**

115296802

---

**IN THE DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO... OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late ENOCK PAUL MHEMBANO**

**And**

**In the matter of Application for letters of Administration by JEMIMA E. MHEMBANO OF P.O.BOX 2290 DODOMA**

**GENERAL CITATION**

**(Made under Rule 75 of the probate Rules, Cap 352 R.E 2002)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners

Objections to the grant should be filed on or before 25th /07/2019.

Dated at Dodoma this .....2019

RESIDENT MAGISTRATE

215295902

### KUPOTEA KWA GARI

**John Venance Kilawe** anatangaza kupotelewa na gari aina ya **TOYOTA KLUGER** yenye namba ya usajili **T 231 DJN** iliyopotea mnamo tarehe 10/5/2019 majira ya saa 19:30. yeyote atakaeiona atoetaarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi taarifa:
**STK/IR/4102/2018**

115292102


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## CHELSEA WARUHUSIWA KUMCHUKUA LAMPARD

**LONDO, England**

KLABU ya Chelsea imepewa ruhusa ya kuzungumza na kocha wa Derby, Frank Lampard, ili kuchukua nafasi ya kuifundisha klabu hiyo msimu ujao.

Lampard mwenye miaka 41, amecheza kwa miaka 13 Chelsea, sasa anapewa nafasi kuchukua mikoba ya Maurizio Sarri, ambaye amejiunga na Juventus baada ya kukaa Stamford Bridge msimu mmoja.

Chelsea maarufu kama 'The Blues' imepanga kuwapa Derby kiasi cha pauni milioni nne kama fidia kwa ajili ya kumchukua Lampard.

Wao Chelsea walipewa fidia ya pauni milioni 5 na Juventus baada ya kuruhusu Sarri kwenda kujiunga na miamba hao wa soka la Italia

"Wakati tunakaribia kuanza kwa msimu, ni matumaini ya klabu zote mbili kuwa Chelsea itafikia mwisho wa suala hili," ilisomeka taarifa ya Derby.

"Klabu haitotoa maelezo mengine hadi suala hili litakapofikia mwisho."

Lampard alianza kibarua chake cha ukocha msimu uliopita akifanikiwa kuiongoza Derby kucheza mechi ya mtoano ya kupanda Ligi Kuu ambayo walifungwa na Aston Villa.





# WAN-BISSAKA SAA ZAHESABIKA UNITED

**Manchester, England**

Manchester United inatumai kukamilisha usajili wa pauni milioni 50 wa Aaron Wan-Bissaka, kwa mujibu wa chanzo cha Sky.

Wan-Bissaka jana alitarajiwa kupimwa afya ndani ya saa 24 tayari kwa kujiunga na Manchester United kufuati miamba hiyo ya Old Trafford kupiga hatua nzuri katika mazungumzo ya kuipata saini ya beki huyo wa kulia wa Crystal Palace.

Beki huyo wa Palace ataigharimu pauni milioni 45 pamoja na pauni milioni tano zitakazolipwa baadaye. Wan-Bissaka anatarajiwa kusaini mkataba wa muda mrefu hapo Old Trafford na utakuwa usajili wa pili kwa kocha Ole Gunnar Solskjaer majira haya ya joto kufuatia kukamilisha kuipata saini ya Daniel James kutoka Swansea.

Beki huyo wa England U-21 atakuwa mchezaji wa nne ghali zaidi wa wakati wote kuwahi kusajiliwa akiwa nyuma ya Paul Pogba (pauni milioni 89), Romelu Lukaku (pauni milioni 76), na Angel Di Maria (pauni milioni 59.7).

Wan-Bissaka amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake hapo dimba la Selhurst Park akishuka dimbani mara 39 katika mashindano yote akiwa na Palace ambayo ilimaliza nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England msimu uliomalizika.

Kocha wa United, Solskjaer alikuwa tayari kusaka beki wa kulia kufuatia kuondoka kwa nahodha wa klabu hiyo, Antonio Valencia.

# Tottenham yakaribia kumnasa Ndombele

**LONDON, England**


KIUNGO wa Lyon, Tanguy Ndombele, anakaribia kujiunga na Tottenham, kwa mujibu wa ESPN FC.

Mazungumzo kati ya Spurs na Lyon yaliendelea vizuri wiki hii na klabu hizo zimekubaliana bei ya mchezaji huyo na wakati wowote atatangazwa kuwa mali ya Spurs.

Lyon wanataka kiasi cha euro milioni 80, lakini Spurs ambao ofa yao ya awali ya euro milioni 45 ilikataliwa sasa wamekubali kutoa kiasi cha euro milioni 60 kwa ajili ya mchezaji huyo.

Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu kadhaa Ulaya zikiwamo Manchester United, Juventus na Paris Saint-Germain, yeye mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kujiunga na Tottenham huku akimsifia kocha, Mauricio Pochettino.

Pochettino alivutiwa na mchezaji huyo Ndombele baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia msimu uliopita na aliisaidia Lyon kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.



HABARI MICHEZO




# CAPELLO:

## REAL MADRID IMEKOSEA KWA RONALDO

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Fabio Capello ameibuka na kusema kwamba miongoni mwa makosa waliyoyafanya Real Madrid ni kumuuza Cristiano Ronaldo.

Kipindi hiki uongozi wa Real Madrid ukijipanga kuimarisha kikosi chake kwa kuwasainisha mikataba nyota kadhaa hadi sasa akiwamo Edern Hazard, Luka Jovic na kinda Takefusa Kubo ili kuweza kurejea kwenye makali yake kama ilivyo awali, lakini Capello amesema maamuzi ya awali yanaigharimu klabu hiyo.

Capello amesema uamuzi wa kumuuza Ronaldo umeigharimu timu hiyo ambapo matokeo yake yalionekana msimu uliopita kwa Madrid kumaliza msimu huo bila taji lolote tofauti na misimu mitatu nyuma na walitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo.

Timu hiyo ilimuuza Ronaldo na baadaye kwenda kujiunga na Juventus ya Italia ambako huko alifanikiwa kutwaa taji la ligi hiyo pamoja na kuweka rekodi ya kutwaa mataji ya ligi kubwa tofauti barani Ulaya kwa nyakati tofauti.

## SILVA: NAONDOKA MANCHESTER CITY

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester City, David Silva, amesema ataondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England mwishoni mwa msimu wa 2019-20.

Alipoulizwa kama ataendelea kucheza hapo baada ya msimu ujao, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amenukuliwa na BBC akisema: "Hapana, msimu ujao ni wa mwisho kwangu kucheza hapa.

"Miaka kumi inatosha. Ulikuwa wakati muhimu kwa upande wangu.

"Awali City walikuwa wanazungumzia mpango wa kuniongeza miaka miwili, lakini niliamua kusaini mwaka mmoja, hivyo nitakuwa nimemaliza kipindi cha miaka 10 ya kukaa hapa.

"Nimemaliza mzunguko. Ulikuwa ni wakati mzuri zaidi kwangu. Sijioni kama nitaweza kuendelea kuichezea City kwa msimu mwingine zaidi. Miaka 10 inatosha kwa upande wangu."

Silva, ambaye alijiunga na City kutoka Valencia mwaka 2010, ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu, mawili ya FA na manne ya ligi, huku akiwa amecheza jumla ya mechi 396 kwa timu hiyo hadi sasa.

Akiwa ameichezea nchi yake ya Hispania mechi 125, Silva alishinda Kombe la Dunia mwaka 2010 na lile la Ulaya mwaka 2008 na 2012.

Mwaka jana aliiambia ESPN FC kwamba anataka kumaliza kipindi chake cha uchezaji soka katika klabu ya Las Palmas, ambayo ni ya nyumbani kwao katika Kisiwa cha Gran Canaria.

# Arsenal yashinda mbio saini ya Saliba

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal inatarajia kuinasa saini ya beki wa timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 19, William Saliba ukiwa ndio usajili wake wa kwanza wa euro milioni 25, kwa mujibu wa ESPN FC.

Arsenal na Klabu ya Saint-Etienne anayoichezea kinda huyo wameshamalizana na wakati wowote atatangazwa kuwa mchezaji mpya wa Arsenal katika kipindi hiki cha majira ya joto.

Hata hivyo, Saliba ataendelea kucheza kwa mkopo pale Saint-Etienne msimu ujao kwa ajili ya kujiimarisha zaidi kabla ya kutua rasmi kwa 'Washika Bunduki' hao wa jijini London.

Arsenal katika mbio za usajili huo imezipiku klabu kadhaa Ulaya ambazo zilikuwa zinamwania mchezaji huyo, Saliba, ikiwamo Tottenham na Paris Saint-Germain.




Mchezaji huyo anakuwa wa kwanza kwa Arsenal chini ya kocha, Unai Emery kusainishwa msimu huu, huku ikiwa imetengewa kiasi cha pauni milioni 45 kwa ajili ya usajili wa kipindi cha majira ya joto.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAGUIRE SASA ZAIDI YA VITA MAN CITY, UNITED

●●●Guardiola lengo Mwingereza, Solskjaer kujenga kikosi, Leicester yataka rekodi ya Van Dijk ivunjwe...

**Manchester, England**

Manchester City na Manchester United wameiambia Leicester wanaandaa pauni milioni 65 kwa Harry Maguire, Sky Sports News inalitambua hilo.

Mazungumzo kati ya klabu zote hizo za Manchester na Leicester yamekuwa yakiendelea kwa wiki kadhaa, lakini bado dili hilo halijakubaliwa.

Maguire inatambulika ni mwenye furaha kuwapo hapo Leicester na hajajaribu kulazimisha kuondoka, lakini amefungua mlango wa kwenda katika moja ya klabu sita inayoongoza Premier League.

Nafasi ya Leicester katika mchakato huo, mara zote haijawa na nia au uhitaji wa kumuuza na itazingatia tu ofa ya zaidi ya pauni milioni 75 ambayo ni rekodi ya dunia kwa beki iliyolipwa na Liverpool wakati ikiinasa saini ya Virgil van Dijk.

Maguire amekuwa moja ya hazina bora zaidi katika dirisha hili la joto baada ya kiwango chake bora Leicester na England.

Pep Guardiola yupo katika presha kubwa ya kuongeza angalau mchezaji mmoja Mwingereza katika kikosi chake kutokana na sheria ya Premier League kuhusu 'wazawa' na ameelekeza macho yake kwa Maguire, ambaye aling'ara kwenye Kombe la Dunia wakati England ikitinga nusu fainali.

Hata hivyo, City inakabiliwa na ushindani mgumu kutoka kwa mahasimu wao wa ndani kufuatia kocha Ole Gunnar Solskjaer kutaka kukijenga upya kikosi hicho kwa kuongeza wachezaji vijana wenye vipaji wa England.

Maguire alijiunga na Leicester akitokea Hull City mwaka 2017 kwa pauni milioni 17 na pia 'Mbweha' hao hawataki kumpoteza, na inajulikana kwamba tayari wameanza kuandaa orodha ya wachezaji muhimu wanaoweza kumrithi ambayo inamjumuisha beki wa Burnley na England, James Tarkowski.

Hata hivyo, Gary Neville anaamini Manchester United inakabiliwa na wakati mgumu sana katika dirisha hili la majira ya joto.

## KWA UFUPI

### NDOMBELE KUTUA KWA REKODI SPURS
Tottenham inakaribia kuipata saini ya kiungo wa Lyon, Mfaransa Tanguy Ndombele, 22, kwa rekodi ya klabu kiasi cha pauni milioni 60. Ndombele alicheza mechi 34 msimu uliopita wakati Lyon ikifuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kumaliza nafasi ya tatu Ligue 1. ***(Sun)***

### NAPOLI KUIREJESHA JEZI YA MARADONA
Napoli inaweza kuirejesha jezi namba 10 ya Diego Maradona kutoka kuistaafisha, wakati huu ikitazama uwezekano wa kuinasa saini ya mshambuliaji wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez. ***(Mail)***

### BUFFON, JUVE WATETA KUREJEA
KIPA wa zamani wa Italia, Gianluigi Buffon, 41, amepiga hatua katika mazungumzo yake ya kurejea Juventus akitokea PSG kwa mkataba wa mwaka mmoja, kwa mtazamo wa baadaye kuwa mkurugenzi. ***(Sky Italia, via Football Italia)***

### GOMEZ KUMRITHI HERNANDEZ
MSHAMBULIAJI wa West Ham, Mmexico Javier Hernandez, 31, anatazama uwezekano wa kuondoka klabuni hapo na kuhamia Hispania, na 'Hammers' hao wanaitaka saini ya straika wa Celta Vigo, Muuruguay Maxi Gomez, 22. ***(Evening Standard)***

### ARSENAL, SPURS KWA SALIBA
Tottenham ipo katika mbio moja na Arsenal za kuwania kuipata saini ya beki wa Saint-Etienne na Ufaransa U-19, William Saliba. 'Gunners' walitoa ofa ya pauni milioni 27 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, ambayo ilikataliwa. ***(Mirror)***

### MOURINHO AIKIMBIA NEWCASTLE
KOCHA wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho anaonekana kujiweka mbali mwenyewe katika nafasi ya kuwania kuinoa Newcastle United. ***(Mail)***

### NEYMAR APEWA MASHARTI PSG
Paris St-Germain inataka Neymar, 27, abaki katika klabu hiyo kama nyota huyo wa kimataifa wa Brazil anaweza kuimarisha kiwango chake. Mabingwa hao wa Ufaransa wanaweza kumuuza Mbrazil huyo lakini watahitaji zaidi ya euro milioni 222 walizoilipa Barcelona wakati ilipomsainisha. ***(Telegraph)***

### CITY YAIVAA JUVE KWA CANCELO
Manchester City imefanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Michezo wa Juventus, Fabio Paratici kuhusu uwezekano wa kuipata saini ya beki Mreno Joao Cancelo, 25, kwa pauni milioni 44. ***(TuttoMercatoWeb, via Star)***

### UNITED YAMTAKA BEN YEDDER
Manchester United inamtaka mshambuliaji wa Sevilla na Ufaransa, Wissam Ben Yedder, 28, na itaweka mezani kiasi cha pauni milioni 35.8 kinachohitaji ili kuvunja mkataba wake. ***(ABC de Sevilla)***

### EL SHAARAWY AKUBALI KUTUA CHINA
WINGA wa Roma, Mtaliano Stephan El Shaarawy, 26, amekubali kujiunga na klabu ya China, Shanghai Shenhua kwa pauni milioni 16.11. ***(Il Tempo)***

### UNITED YAZIFUATA JUVE, BARCA
MANCHESTER United inavutiwa na huduma ya mshambuliaji Mfaransa Mathis Rayan Cherki, anayeichezea Lyon ambaye pia anaivutia Real Madrid, Juventus, Barcelona na Bayern Munich. ***(Telegraph)***

### MIGNOLET AWINDWA PALACE
KIPA wa Liverpool, Mbelgiji Simon Mignolet, 31, anatakiwa na Crystal Palace. 'The Eagles' hao wanaandaa pauni milioni nane kwa ajili ya kumnasa Mignolet, ambaye amebakiza miaka miwili katika mkataba wake hapo Anfield. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

# MSENEGAL ALIYEIUA STARS AMNG'ATA 'SIKIO' MSUVA

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

MSHAMBULIAJI wa timu ya Taifa ya Tanzania ( Taifa Stars), Simon Msuva, amesema ndoto zake kwa sasa ni kucheza soka Ulaya na hafikirii tena kurudi kuzitumikia timu za nyumbani hususan za jijini Dar es Salaam, Simba na klabu yake ya zamani, Yanga, huku akifunguka kung'atwa 'sikio' na mfungaji wa bao la kwanza la Senegal, Keita Balde Diao kuhusu uwapo wa kusheheni vipaji katika kikosi cha Stars.

Kwa sasa Msuva amebakisha mkataba wa mwaka mmoja na klabu yake ya Difaa El Jadida ambayo inashiriki Ligi Kuu ya Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa, Msuva alisema anaamini uwezo wa kucheza soka Ulaya anao, na anamshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kujiunga na Difaa El Jadida ambayo imemwongezea uzoefu na kukuza kipaji chake.

Msuva alisema anaamini wachezaji wa Stars watakapopata nafasi ya kucheza Ulaya au nje ya Tanzania, watapata uzoefu na hatimaye kuja kulisaidia taifa lao katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Alisema anajiamini kuwa ana sifa za kucheza Ulaya na thamani yake si ya kucheza tena katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mimi ninafikiria Ulaya tu, nasikia nimetajwa na watu wa Simba, Yanga nao wanaona kama ninaweza kurudi kwao, kwangu hilo jambo halipo, sifikirii nyuma, nawaza kusonga mbele, nafikiria changamoto mpya, nafikiria klabu kubwa kama wanazokwenda wenzetu wa Afrika Magharibi," alisema Msuva.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Yanga aliongeza kuwa Tanzania kupata nafasi ya kushiriki mashindano haya ya Afcon, kunaweza kusaidia kuongeza wachezaji watakaosajiliwa nje na hili ndilo moja ya malengo wanayoyatarajia katika fainali hizi.

"Kwa mfano yule mchezaji wa Senegal aliyetufunga bao la kwanza (Keita Balde), aliniambia timu yetu ina vipaji, lakini hatuna uzoefu na katika mechi ile tulikuwa hatujui tufanye nini, wao waliona kama tuko mazoezini," alisema Msuva.

Aliwataka wachezaji wa Tanzania kuongeza nidhamu wanapokuwa ndani ya uwanja kwa sababu, mawakala huangalia vitu mbalimbali wakati wanatafuta wachezaji.

"Mimi sijawahi kupata hata kadi ya njano huko Morocco, ila wenzangu ndio wanazipata kupitia mimi, hii ni rekodi nyingine nzuri kwangu," alisema mshambuliaji huyo.

AMETUA...



Kocha mpya wa KMC, Mganda Jackson Mayanja (kulia), akitia saini mkataba wa mwaka mmoja jana wa kuinoa timu hiyo ya Halmashauri ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, akichukua nafasi ya Mrundi Etiene Ndayiragije aliyetimkia Azam FC. **MPIGAPICHA WETU**

# Gabriel, Chambua waifunda Stars

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa zamani wa timu ya Soka ya Taifa ( Taifa Stars), wamewataka nyota wa timu hiyo kuendelea kujiamini na kutambua kwamba wanaweza kufanya vizuri katika mchezo wa leo dhidi ya Kenya (Harambee Stars) na kutosikiliza maneno yanayosemwa na wadau wa mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, mshambuliaji wa zamani wa Simba, Emmanuel Gabriel, alisema kuwa wanajua ugumu wa michuano hiyo na kilichotokea katika mechi dhidi ya Senegal ni sehemu ya mchezo.

Gabriel alisema anaamini wanaweza na mchezo wa leo kwao waufananishe na fainali ya michuano hiyo.

"Naomba mwambie nahodha wa Stars, Mbwana Samata na jeshi lake wasikate tamaa, wapambane hadi mwisho, Mungu atawasaidia wasisikilize maneno ya kuwakatisha tamaa, wako vizuri na wasife moyo kwa kufungwa na Senegal, wamejitaidi sana," alisema Gabriel.

Aliongeza kuwa kwa kiwango cha soka cha Tanzania, wachezaji wa Stars walijitahidi sana katika mchezo huo na sasa wanatakiwa kuhakikisha leo wanacheza "kufa au kupona" ili washinde, na kwamba jambo muhimu kwa sasa ni kuwekeza kwenye soka la vijana," Gabriel alisema.

Naye Sekilojo Chambua, alisema kikosi cha Stars hakina cha kupoteza na wanastahili kupongezwa kwa hatua ambayo wamefikia.

"Waambie hawana cha kupoteza na wanaweza kufanya lolote kwenye mpira, cha muhimu ni kujiamini kwamba wao ndiyo timu ya nchi kwa sasa, waingie wajitume. Watulie wacheze bila shinikizo lolote litakalowafanya wawe na presha ya mchezo, kinachotakiwa kwao, ni kuikabili hali hiyo, waambie wasiogope kwa matokeo ya mchezo wa kwanza huo ndiyo mpira, tuko nyuma yao," alisema Chambua.

Taifa Stars inashiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika mwaka huu baada ya kuzikosa kwa miaka 39 na baada ya mechi ya leo, itarudi tena dimbani Julai Mosi kuivaa Algeria katika mechi yao ya mwisho ya Kundi C.

## ZFF yafungua dirisha la usajili

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefanya marekebisho ya kalenda yake ya msimu wa 2019/20 ambayo imegusa sehemu nyeti ikiwamo kufunguliwa na kufungwa kwa dirisha la usajili.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Rais wa ZFF, Seif Kombo alisema miongoni mwa marekebisho hayo ni tarehe ya usajili na uhamisho, ambapo rasmi dirisha hilo limefunguliwa juzi Juni 25 na likitarajiwa kufungwa Julai 31, mwaka huu.

Alisema awali dirisha hilo lilitarajiwa kufunguliwa Juni Mosi hadi 19, wakati Julai 11 hadi 20, mwaka huu ilikuwa siku ya kuwasilisha pingamizi.

**Kombo alisema kuchelewa kuanza kwa zoezi hilo kumetokana na uchaguzi mkuu wa shirikisho hilo pamoja na suala zima la ku undwa kwa kamati za shirikisho hilo.**

Kwa mujibu wa kalenda hiyo, kuanzia Mei 20-25, mwaka huu, kulifanyika mchakato kwa klabu kuwasilisha kwanza majina ya wachezaji waliowaacha na Mei 25-30 ilikuwa siku za kutoa kanuni itakayotumika kwa mashindano ya ligi msimu 2019/20.

## Karate watangaza kuchaguana Julai

**Na Shufaa Lyimo**

Chama cha Shotokan Karate Tanzania (Tashoka) kinatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu jijini Dar es Salaam Julai 27, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe juzi, msemaji wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Frank Mzunga, alisema awali uchaguzi huo ulipangwa kufanyike mwezi huu lakini ulisogezwa mbele ili kuwapa nafasi wagombea kujiandaa.

Alizitaja nafasi zinazogombewa kuwa ni nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Kaimu Katibu Mkuu, Mweka Hazina pamoja na nafasi za wajumbe.

Alisema ada ya kuchukua fomu kwa upande wa viongozi wote ni Sh. 50,000 isipokuwa ya wajunbe ambayo ni Sh. 20,000 na kwamba mwisho wa kurudisha fomu ni Julai 19, mwaka huu.

"Tunaomba wagombea wote wafuate taratibu za uchaguzi ili kuepusha usumbufu na uchaguzi ufanyike kwa uhalali," alisema Frank.

Michezo

Alhamisi Juni 27, 2019

Nipashe



Maguire sasa zaidi ya vita Man City, United

HABARI UK 30

KAZI IPO LEO...



Wachezaji wa Taifa Stars wakiwa mazoezini jana kwenye Uwanja wa Petrosport jijini Cairo, Misri kujiwinda na mechi ya Afcon Kundi C dhidi ya Harambee Stars leo. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# KOCHA HARAMBEE: MANULA KIKWAZO

- Awataka washambuliaji wake kuongeza umakini leo, Amunike aionya Taifa Stars, aitaka kwanza...

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

WAKATI Emmanuel Amunike akipania leo kukipa kikosi chake ushindi dhidi ya majirani zao Kenya (Harambee Stars), katika mechi ya pili ya Kundi C ya fainali ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019, Kocha wa Harambee Stars, Mfaransa Sebastien Migne, hofu yake ameielekeza kwa kipa wa Taifa Stars, Aishi Manula kuwanyima ushindi.

Taifa Stars itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Senegal na Harambee Stars nao wakikumbuka kupoteza mchezo wao wa kwanza kwa idadi hiyo ya mabao dhidi ya Algeria.

Akizungumza kuhusu mechi ya leo itakayochezwa Uwanja wa 30 June jijini hapa, Kocha Mkuu wa Stars, Amunike, alisema timu yake imejiandaa kupata ushindi katika mechi hiyo kwa sababu inaamini matokeo hayo ndio yatawaweka kwenye nafasi nzuri na si vinginevyo.

Amunike alisema mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa pande zote mbili kwa sababu ya wachezaji wake kufahamiana vema na kuhitaji kufuta makosa ya mchezo uliopita.

"Ni mechi itakayokuwa ngumu kwa kila timu, tunajuana, tunazungumza Kiswahili pamoja, hakuna ambaye amekuja hapa kwa ajili ya kufungwa, tutafanya jitihada zote kuhakikisha tunashinda, tunataka ushindi tu katika mechi yetu ya kesho (leo) dhidi ya Wakenya," Amunike alisema.

Hata hivyo, Mnigeria huyo alikataa kusema ni mfumo gani ambao watautumia katika mchezo wa leo, baada ya kucheza kwa mfumo wa kujilinda zaidi kwenye mechi iliyopita dhidi ya Senegal. "Wao walituangalia na sisi tumewaangalia na kuona wanavyocheza, siwezi kusema tutacheza mfumo gani, hili linabaki kwa bechi la ufundi, kikubwa ni nini tutafanya tutakapokuwa na mpira," aliongeza Amunike.

Naye Kocha Mkuu wa Harambee Stars, Migne, alisema mchezo wa leo utakuwa na upinzani kwa sababu timu zote zinahitaji kurejesha matumaini ya kubakia kwenye michuano hii inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, Caf.

Migne alisema atahitaji kuona wanashambulia zaidi ili wapate mabao ambayo yatawahakikishia kuondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo huo.

"Ni mechi itakayokuwa na changamoto nyingi, tunafahamiana, tunatoka ukanda mmoja, lakini ninaamini tutapata matokeo mazuri," alisema kocha huyo.

Aidha, Migne alimtaja kipa Manula kuwa ana kiwango cha juu kinachoweza kukidhi kucheza Ulaya na kwamba anaweza kuwa kikwazo kwa timu yake kupata ushindi katika mchezo wa leo, na kuwataka washambuliaji wake kuongeza umakini zaidi wanapokuwa na mpira.

Migne alisema mbali na kipa huyo, wachezaji wa Stars sasa wameimarika tofauti na walivyokuwa kabla ya kuanza mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo za Afcon.

"Golikipa wao ni mzuri, anaweza kucheza hata Klabu za Ulaya, anaonekana ni mzuri na ana uzoefu, amecheza mechi nyingi za klabu yake za Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu," alisema Mfaransa huyo.

Katika viwango vya ubora wa Fifa, Taifa Stars iko nafasi ya 131, Harambee Stars wako namba 108 wakati Algeria ni wa 70 na Senegal yenyewe iko nafasi ya 23 na kwa Afrika ni ya kwanza.

## CHAMA AJIFUNGA, KOTEI KAIZER CHIEFS

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mchezeshaji Mzambia Clatous Chota Chama maarufu kama Triple C ama Mwamba wa Lusaka, amesaini mkataba mpya wa miaka miwili kuendelea kuitumikia Simba, lakini habari mbaya kwa mashabiki wa klabu hiyo ya jijini Dar es Salaam ikiwa ni kuikosa huduma ya kiungo wao mkabaji, James Kotei kwa msimu ujao.

Wakati taarifa ya Simba kupitia mtandao wao wa Instagram jana mchana zikieleza kuwa Chama ameongeza mkataba wa miaka miwili na miamba hiyo ya mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam, Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini iliripoti kuinasa saini ya Kotei kwa mkataba wa miaka mitatu.

"Mfungaji wa mabao ya mwisho ambayo yalitupeleka kwenye hatua ya makundi na robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Clatous Chota Chama (Triple C) bado yupo sana Msimbazi. Mwamba wa Lusaka ataendelea kuwa sehemu ya kikosi cha mabingwa baada ya kusaini mkataba mpya wa miaka miwili," ilisema taarifa ya Simba jana.

Kwa uamuzi huo wa Chama, sasa anaingia kwenye orodha ya wachezaji wengine walioongeza mikataba na klabu hiyo, kipa Aishi Manula, Erasto Nyoni, Shomari Kapombe, nahodha John Bocco na msaidizi wake, Mohammed Hussein 'Tshabalala, Jonas Mkude na Meddie Kagere.

Hata hivyo, licha ya kuondoka kwa Kotei, tayari Simba imejiimarisha kwa kuinasa saini ya kiungo mkabaji kutoka Al hilal ya Sudan, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman, beki wa kati mwenye uwezo pia wa kucheza kama kiungo mkabaji Mbrazil, Gerson Fraga Vieira na mshambuliaji Wilker Henrique da Silva raia wa Brazil pia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >